**OORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais |
| 2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani. |
| 3.Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais |
| 4.Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu |
| 5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa |
| 6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa |
| 7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 8.Mhe. Hamad Masoud Hamad | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole. |
| 9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa |
| 10.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa |
| 11.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa |

| | |
|---|---|
| 12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni |
| 13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge. |
| 14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki |
| 15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni |
| 16.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando |
| 17.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi |
| 18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe |
| 19. Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni |
| 20.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |
| 21.Mhe. Omar Othman Makungu | Mwanasheria Mkuu |
| 22.Mhe. Issa Haji Ussi | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka |

| | |
|---|---|
| 23.Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake |
| 24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya | Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais |
| 25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake |
| 26.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi |
| 27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni |
| 28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 30.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 31.Mhe. Ali Abdalla Ali | Jimbo la Mfenesini |
| 32. Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 33. Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |
| 34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 35. Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 36.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 37.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 38.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |

| | |
|---|---|
| 40.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 42.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 43.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 44.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 47.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Jimbo la Kikwajuni |
| 49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa | Jimbo la Mkwajuni |
| 51.Mhe. Mgeni Hassan Juma | Nafasi za Wanawake |
| 52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 53.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad | Jimbo la Chambani |
| 55.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Jimbo la Mpendae |
| 56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Nafasi za Wanawake |
| 57.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 58. Mhe. Mussa Khamis Silima | Jimbo la Uzini |
| 59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 61.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |

| | |
|---|---|
| 62.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 63.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Rashid Seif Suleiman | Jimbo la Ziwani |
| 65.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 66.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 67.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 68.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 69.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 70.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 71.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 72.Mhe. Salum Amour Mtondoo | Jimbo la Bububu |
| 73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan | Jimbo la Dole |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim** **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

**(Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 12 Julai, 2011**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua*

**KIAPO CHA UAMINIFU**

**Mhe. Ali Mzee Ali:** *Bismillahi Rahman Rahym. "*Mimi Ali Mzee Ali naapa kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar katika kazi zangu za uwakilishi, na nitatumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitazihifadhi, nitazilinda na kuzitetea kwa dhati Katiba ya Zanzibar na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie."

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa anachukua nafasi yake karibu sana. Nichukue nafasi hii kumkaribisha rasmi Mhe. Ali Mzee Ali yeye si mgeni katika chombo chetu hiki, tumekuwa naye kwa vipindi viwili vilivyopita na bahati nzuri mara hii Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein amemuona tena na kumleta ili tuwe naye tuendelee na shughuli kwa mashirikiano makubwa. Naomba Waheshimiwa Wajumbe tumkaribishe mwenzetu huyu na yeye tunamuomba ashirikiane pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wenzake katika shughuli zetu kama ilivyo kawaida, karibu sana. *(Makofi)*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Pili wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia Tarehe 19 Januari, 2011 hadi Tarehe 28 Januari, 2011 Baraza lilipitisha Miswada miwili ya Sheria kama ifuatavyo:-

1. Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Uendelezaji, Ukuzaji na Uwekaji wa Viwango na Ubora wa Bidhaa na Usimamizi wa Huduma zinazolingana na hizo na mambo yanayohusiana na hayo.
2. Mswada wa Sheria wa Kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Vile vile katika Mkutano wa Tatu wa Baraza la Nane la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 23 Machi, 2011 hadi 04 April, 2011 Baraza lilipitisha Miswada minne ya sheria kama ifuatavyo:-

1. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu Nam. 6 ya Mwaka 2001, na kuweka Sheria mpya ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
2. Mswada wa Sheria ya Mikataba ya Amana na Mali Zinazohamishika na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
3. Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula (MTAKULA) Sheria Nam. 3 ya Mwaka 1988 na kutunga Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
4. Mswada wa Sheria ya Mtoto itakayotoa Haki na Maslahi Bora ya Mtoto.

Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 90(3) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la Mwaka 2011, naomba kutoa taarifa kwamba, Miswada hiyo imekuwa sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kupokea taarifa hiyo ya kazi ambayo mmeshaifanya.

Pili kuna tangazo ambalo limepitia kwa Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Juma Duni Haji kwamba ameleta wageni wetu hapa ambao ni Kampuni ya *Double Park* kutoka Afrika ya Kusini ikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Bwana Jeo Chueni na Dkt. Kingu Said Mtemi kutoka Tanzania, wamekuja na lishe ya *Jazia Mills*. Hiki ni chakula ambacho kufidia virutubisho vinavyokosekana mwilini na kinaweza kutumiwa na wagonjwa na hata wale wasio wagonjwa bila ya kuleta athari yoyote. Wageni wetu hao madaktari wapo juu sehemu ya wageni na kwa wakati wa kuanzia sasa watakuwa nje kwa wale watakaohitaji maelezo ya ziada pamoja na lishe ya Jazia. Nawaomba madaktari wetu hao, ndugu zetu wasimame ili waonekane na kuwasalimia Waheshimiwa Wajumbe.

*(Wageni walisimama kwa muda na kusalimia Waheshimiwa Wajumbe)*

*You are most well come* (karibuni sana). Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe.

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya mwaka 2011/2012. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 192

### Bustani Ya Migombani

**Mhe. Viwe Khamis Abdalla** – Aliuliza:-

Bustani ya migombani inapigiwa kelele sana kuwa haina hadhi ya kuitwa bustani, na hivi sasa imekuwa chaka la maovu kwa sababu inatumiwa na wala unga, wavuta bangi na vibaka.

(a) Je, ni lini Serikali itachukuwa hatua ya kutengeneza bustani hiyo.

(b) Kwa sababu Serikali imeweka Sheria ya *BOT* (*Build Operate Transfer*), kwa nini Serikali haitafuti mbia wa kuendeleza bustani hiyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 192 lenye vifungu (a) na (b) naomba nitoe maelezo machache yafuatayo:-

Mhe. Spika, Kamishna Mkuu wa Uingereza, Bwana John Kirk ambae pia ni mtaalamu wa mimea na wanyama, alianzisha Bustani ya Mimea iliyoko Migombani ambayo ni bustani ya mimea ya pekee kwa Zanzibar ambayo aliianzisha katika mwaka 1870. Bwana John Kirk kwa kuanzisha bustani hiyo kama ni eleo la majaribio kwa kuanzisha mimea ya kiuchumi ambapo bustani hiyo ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa wakati huo katika kuendeleza kilimo hapa Zanzibar. Baadae ukusanyaji wa viumbe wageni na wa ajili uliimarishwa na bustani hiyo ilitumika kama ni eneo la kujisomea na utafiti na Nasari ya miti ya kuuza.

Vile vile, bustani hiyo ni sehemu moja wapo ya maeneo ya Kihistoria ya Zanzibar inayounganisha na tamaduni zilizopita. Bustani hiyo hivi sasa ipo chini ya uongozi wa Baraza la Manispaa na Tume ya Mazao ya Zanzibar, lakini

kwa miaka ya hivi karibuni bustani hiyo imekuwa haishughulikiwi ipasavyo. Tatizo lililowazi zaidi uchimbaji wa mchanga, kusogelewa holela wa makaazi ya watu, ukataji holela wa  wa miti na mfumo mbaya wa mitaro ya maji machafu na ya mvua.

(a) Bustani ya Migombani au kama inavyoitwa kuwa ni *Botanical Garden* hivi sasa ipo chini ya Uongozi wa Baraza la Manispaa. Lakini lazima nikiri kwamba, kwa miaka ya hivi karibuni bustani hiyo imekuwa haishughulikiwi ipasavyo. Tatizo lililo wazi zaidi ni uchimbaji wa mchanga, kusogelewa kiholela kwa makaazi ya watu, ukataji kiholela wa miti na mfumo mbaya wa mitaro ya maji machafu pamoja na maji ya mvua.

Mhe. Spika, bustani hii ni miongoni mwa bustani ambazo zina historia kubwa na ya aina yake katika Manispaa ya Zanzibar, hasa kutokana na aina ya miti mbali mbali ambayo imepandwa katika bustani hiyo. Hali ya bustani hiyo kwa sasa imekuwa katika hali isiyo ya kuridhisha kama nilivyosema, na serikali kupitia Baraza la Manispaa, inatarajia kuifanyia matengenezo makubwa, mpango huo utaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Sambamba na hilo, serikali imeazimia kudumisha usafi katika eneo hilo labustani kwa kuandaa mkakati wa Manispaa Shirikishi ambao utashirikisha vikundi vitakavyojishughulisha na uzoaji wa taka pamoja na kuanzisha juhudi za kuongeza upandaji wa miti katika eneo hilo.

Mhe. Spika, tayari bustani hiyo imetembelewa hivi karibuni na Ndugu FREUX KINDA, Mwana mazingira Duniani kutoka Ujerumani tarehe 4 Julai, 2011 ambaye pia amehamasisha upandaji wa miti hapo *BOTANICAL GARDEN*. Aidha, vikapu vya kuzolea taka vitaongezwa na kuweka utaratibu wa kuondoa na utupaji wa taka katika eneo hilo. Kwa kushirikiana na Mradi wa *Chumbe Coral Reef*, tayari umeandaliwa utaratibu maalum wa kutenganisha taka na baadae taka hizo zitafanywa mbolea itakayotumika katika eneo hilo la *BOTANICAL GARDEN*. Mpango huu pia utawaongezea ajira binafsi vijana wanaoishi maeneo hayo na maeneo ya Jang’ombe. Namuomba sana Mhe. Viwe Khamis tusaidiane kufanikisha mpango huu.

(b) Mhe. Spika, si busara kwa sasa kwa Bustani ya Migombani kupewa mtu binafsi au taasisi zenye lengo la kuiendesha kibiashara kwa njia ya *BOT,* kwa sababu zifuatazo:-

- Bustani ya Migombani ni moja ya bustani pekee yenye miti ya asili ikiwemo miti mbali mbali ya hapa Zanzibar na mengine yenye asili ya Nchi Baridi ambayo inahitaji kuhifadhiwa zaidi kwa njia za kitaalamu na ndio maana bustani hio inaitwa *BOTANICAL GARDEN.*

- Bustani hio ni ya kihistoria ambayo Manispaa ina mpango wa kuiimarisha na kuirejesha haiba yake ya asili ya Jina la *Botanical Garden* ili kuwapa fursa wananchi wa watafiti mbali mbali kutembelea kujionea aina ya miti yenye asili mbali mbali duniani ili kuweza kukidhi haja ya sababu ya kuanzishwa kwake.

- Kuwapa taasisi binafsi au Taasisi nyengine za Serikali ambazo zenye malengo ya kibiashara zaidi kuna hatari ya kupoteza malengo yaliokusudiwa na azma iliyokuwepo sasa ya kuirudishia hadhi na haiba yake ya asili.

**Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri pamoja na mipango mizuri ambayo imepangwa na wizara yake kwa ajili ya kuishughulikia bustani ile ya *Botanic,* lakini bustani ile imeathirika sana na msingi ambao ni mpakani baina ya Jimbo la Kikwajuni na Jimbo la Mpendae. Sasa ili tuweze kuleta haiba ya kupendeza katika bustani ile, sijui tuna mpango gani wa kushughulikia ule msingi ambao ni wa muda mrefu uko pale na unaasiri hata uwezo wa watu kuweza kuvuka kutoka ng'ambo moja na kwenda nyengine na hakuna utaratibu ambao umechukuliwa.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:** Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa kwamba msingi uliopo pale hivi sasa hauko katika hali nzuri. Na ukweli wenyewe ni kwamba ule msingi umezidiwa na taka au uchafu na pia kutoshughulikiwa. Katika mipango yetu niliyoisema ya Baraza la Manispaa kwa mwaka huu, msingi ule utashughulikiwa ipasavyo, lakini kabla ya kuanza kushughulikiwa huko pia naona tutafanya *first aid* kwanza tuone nini tufanye kuusafisha angalau kwa sasa uweze kupitisha maji machafu.

**Nam. 91**

**Fidia kwa Wanannchi wa Bumbwini – Mfenesini**

**Mhe. Ashura Sharif Ali** - Aliuliza:-

Nia ya serikali ni kuwapatia wananchi wake huduma muhimu zikiwemo huduma za barabara. Kwa kuwa wakati wa utayarishaji wa ujenzi wa barabara, hatua nyingi huchukuliwa kama vile kutathmini mali za wananchi kwa mfano: mazao, miti na makaazi na hatimaye wananchi hao hulipwa fidia.

Je, ni sababu zipi zilizopelekea baadhi ya wananchi wa Mfenesini – Bumbwini kutokulipwa fidia za nyumba zao na ni lini wananchi hao watalipwa fidia zao ili waweze kumudu kujenga makaazi mapya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 91 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mheshimiwa swali lake naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapatia huduma nzuri wananchi wake likiwemo suala la huduma bora ya barabara. Katika ujenzi wa barabara yeyote ile hapa nchini, serikali huanza na kufanya tathmini ya makaazi na vipando ambavyo vitaathirika wakati wa ujenzi huo. Zoezi hili hufanyika baada ya wizara yangu kujua eneo ambalo linahitajika katika ujenzi wa barabara husika.

Mhe. Spika naomba ieleweke pia kwamba, karibu katika miradi yote ya ujenzi wa barabara suala la kuwalipa fidia wananchi wanaoathirika na ujenzi linakuwa ni jukumu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, wizara yangu imejiwekea utaratibu wa kutokumbomolea mtu yeyote makaazi yake kabla ya kumlipa fidia au vyenginevyo kwa makubaliano maalum na mhusika mwenyewe. Na kuhusu suala la vipando mara nyingi huwataka waathirika hao watustahamilie hadi pale fedha kwa ajili ya kulipa fidia zitakapopatikana.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wananchi wote wanaoishi eneo la Mfenesini hadi Bumbwini ambao nyumba zao zimebomolewa wameshalipwa fidia. Fidia hiyo ni kwa

wananchi ambamo barabara imepita na nyumba zao zimebomolewa. Aidha, kuwapa ambao pia vipando na miti nayo pia wamelipwa fidia.

Mhe. Spika, kunawezekana kukawa na watu ambao hawajalipwa fidia katika vipando vyao, lakini kwa upande wa nyumba tayari fidia imeshalipwa.

**Mhe. Ashura Sharif Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kutokana na majibu ya Mhe. Waziri anasema kuna watu ambao wamelipwa fidia ya nyumba zao, lakini mimi nina ushahidi kwamba kuna watu ambao hawajalipwa hadi hii leo na nyumba zao kweli hazikuvunjwa, lakini hazikaliki na wamehamia katika sehemu nyengine. Je, analijua hilo?

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, nyumba ambazo zimelipwa fidia ni zile nyumba ambazo zimeondoshwa au zimevunjwa kwa ajili ya kupitishwa barabara. Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba, yawezekana katika ujenzi huo unaoendelea kuna nyumba ambazo ziko pembezoni zimeathirika na ujenzi huu hizi hatujazilipa fidia. Napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba baada ya ujenzi huu kukamilika Wizara ya Miundombinu itafanya tathmini na kama kuna nyumba ambayo imeathirika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italipa fidia.

**Mhe. Ali Abdalla Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mimi naishi Michungwa Miwili na mimea yangu imeng’olewa muda mrefu, lakini ilipotiwa thamani sijui ni kiasi gani na sijui niende kwa nani. Je, mimi atanisaidiaje ili nipate haki yangu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, tahmini kama imefanywa na kumbukumbu zipo, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi haki yake haitopotea ataipata.

**Mhe. Subeit Khamis Faki:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza kwa sababu alipokuwa akitoa maelezo ya msingi alisema kwamba, kuna watu waliovunjiwa nyumba zao wameshalipwa na bado vipando kama nimemsikia vizuri. Sasa namuuliza, kama wamelipwa watu kwa nyumba zao vipando bado, tathmini ilikuwa ikionesha ni kiasi gani cha fedha ambacho kilitaka kutumika kwa ajili ya kuwalipa watu nyumba zao na fedha. Je, hivi vipando ambavyo bado havijalipwa ni lini wananchi watalipwa fidia yao ili wapate kujikimu katika maisha yao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:** Mhe. Spika, katika majibu yangu mama nilieleza kwamba, jukumu la kulipa fidia ni jukumu la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sote tunakiri na tunatambua kwamba kuna baadhi ya nyakati serikali yetu uwezo wake wa fedha unakuwa mdogo na miradi hii ya barabara ina umuhimu wake, si vyema kukosa mradi wa barabara kwa kisingizio cha kukosa fedha ya kulipia fidia.

Mhe. Spika, tumeeleza kwamba kipaumbele chetu katika ulipaji wa fidia ni kwa ajili ya nyumba au makaazi ya wananchi ili kuondoa usumbufu ambao wangeweza kupata wananchi wetu pale watapokuwa hawana sehemu ya kukaa.

Kwa upande wa vipando mategemeo na madhumuni yetu ni kulipa fidia kwa mali zote za wananchi ambazo zitaathiriwa na ujenzi wa barabara. Hivyo basi, upande wa majengo kama tumeweza kulipa fidia basi madhumuni yetu na upande wa vipando tutalipa fidia. Lakini Mhe. Spika, la vipando tunaomba wananchi wetu wafanye subira watusubiri na serikali yao ni serikali sikivu na yenye kuwapenda wananchi wake. Tunawahakikishia pale tutakapopata uwezo wa fedha tutalipa fidia hizi.

**Nam. 130**

**Uhaba wa Madaktari wa *X-Ray***

**Mhe. Salma Mohammed Ali** – Aliuliza:-

Katika Kisiwa cha Pemba kuna daktari mmoja tu wa usomaji wa picha za *X-Ray* ambaye anategemewa kutoa huduma hizo kwa hospitali zote za Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri hatua gani za utoaji wa huduma hii muhimu zinachukuliwa pale daktari huyu anapopata dharura yoyote inayokubaliwa kisheria.

(b) Ni lini madaktari wa *X-Ray* na wa kada nyenginezo wataongezwa katika Hospitali za Pemba ili kuimarisha huduma za afya kisiwani huko.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 130 lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba kwa muda huu yupo daktari mmoja tu mtaalamu wa kigeni anaehusika na usomaji wa

picha za *x-ray* kwa hospitali zilioko Pemba. Mtaalamu huyo anahusika zaidi kusoma picha zenye kuhitaji utaalamu mkubwa. Ikitokezea dharura kama hiyo picha zitapelekwa Unguja kusomwa na majibu yatapelekwa kwa *e-mail, fax* au simu.

Mhe. Spika, kwa muda mrefu wizara imekuwa na utaratibu wa kupokea madaktari wa kigeni wa fani ya kusoma picha (*Radiologist*) kwa hospitali za Unguja na Pemba. Karibuni tu wizara imempokea Daktari wa *Radiology* na yuko Mnazi Mmoja anafanya kazi. Nia ya wizara kuendelea na utaratibu wa kuwapokea madaktari wa kigeni hadi pale tutapoweza kujitosheleza kwa wataalamu wa fani hii.

(b) Mhe. Spika, wataalamu wa kada mbalimbali za afya wamepelekwa Pemba. Kati ya wafanyakazi 270 waliomaliza Chuo cha Afya Mbweni mwaka huu, asilimia 60 wamepangiwa kazi Pemba.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kama Mhe. Naibu Waziri alivyosema kuwa ni kweli Pemba kuna daktari mmoja tu wa kusoma picha za *x-ray*, na wakati mwengine hutokea mgonjwa akahitaji kwenda *x-ray* na kuhitaji kupata jawabu za haraka ili kuweza kuendelea na matibabu. Lakini kwa sababu msomaji ni mmoja siku nyengine hubidi mgonjwa achukue siku tatu kabla ya kupatikana jibu kwa kuondoka *x-ray* ile kutoka hospitali moja kupelekwa kwengine kule aliko msomaji.

Je, Mhe. Naibu Waziri haoni kuwa iko haja ya kutafuta wasomaji wa *x-ray* kwa haraka ili kupunguza maafa yasitokee Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kwanza napenda niwaarifu Waheshimiwa kwamba wasomaji wa picha ulimwenguni kwa ujumla ni matatu. Ni *field* ambayo kwa kweli madaktari hawaipendi kwa sababu sijui wanafikiri hailipi labda, halafu pia kwa kuogopa mionzi. Kwa hiyo, wapo watatu, hapa Zanzibar kila mwaka tunapojaribu kupeleka watu kuomba waje kwetu tunaomba lakini si mara nyingi tunawapata kuja kwa sababu huko tunakowaomba hawapo.

Mhe. Spika, hapa kwetu Zanzibar wengi tulishawishiwa twende tukasome nikiwemo mimi mmojawapo na nilipata kwenda kusoma. Kwa hiyo, hawapo wengi, Unguja yupo mmoja, kwa nchi nzima yupo mmoja, halafu tuna mtaalam mmoja kutoka nje. Kwa hiyo, wapo wawili na Pemba yupo mmoja. Si suala la kwamba hatutaki isipokuwa hata ule upatikanaji si rahisi.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri

kwamba wizara yake kwa muda mrefu inapokea madaktari wa kitengo hichi cha *x-ray*. Je, huoni kutokupeleka madaktari kule Pemba ni kutokuwafanyia haki wananchi wa Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, Pemba daktari wa kusoma picha yupo.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba wataalam wa fani hii ni wachache na amekiri kwamba Pemba yupo mmoja na Unguja yupo mmoja. Je, hii ndio mipango ya serikali kwamba daktari huyu awe mmoja tu. Hawana uwezo wao wa kusomesha wengine kwa kisingizio kwamba wanakataa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, kama nilivyokwisha kujibu maswali hayo kwa wengine napenda niseme kwamba watu hawa duniani hawapo ni wachache waliopo. Unguja tuliopo tu madaktari hatukutaka kwenda kusoma sasa tutawapeleka nani kama mtu hataki. Walioko nje hawapatikani hata tukiomba hawapo. Sasa waliopo wale waliopatikana ndio hao hao tunaowapeleka. Tunahakikisha Pemba wanakuwepo na Unguja wanakuwepo, Pemba yupo mmoja na Unguja yupo mmoja, hatuna jinsi nyengine.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuongeza maelezo. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya naomba kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe kwamba juzi kwenye hotuba yetu ya bajeti tuliyaeleza masuala haya kwa urefu sana na tukaulizwa maswali tukafanya uchambuzi. Juhudi za kuwasomesha wataalam wa *x-ray* zipo na tupo kwenye mipango. Tunaomba waheshimiwa watupe muda tujitahidi kuwatafuta na kuwapeleka.

Lakini sio mpango wa serikali kwamba tusiwasomeshe watu wa x-ray, mpango wa serikali ni kusomesha madaktari kama tulivyoeleza kwa urefu katika hotuba yetu ya juzi. Tulieleza kwa urefu kwamba kwa jumla kuna upungufu kwa wataalam wa aina zote ikiwemo hii ya *x-ray*. Tutachukua juhudi tuwaongeze, lakini pale tunaposema tusiendelee tu kujenga vituo vya afya visivyo wataalam jawabu lake moja na matatizo yake moja ni hili. Mkishajenga kituo cha afya mnatudai madaktari, tukikwambieni hatuna mnatwambia kwa nini. Waheshimiwa Wajumbe tushirikiane. Ahsante.

## Nam. 93

## Uuzaji wa Viwanja Kiwengwa

**Mhe. Ashura Sharif Ali -** Aliuliza**:**

Kwa kuwa miaka ya hivi karibuni kumezuka wimbi kubwa na mtafaruku wa viwanja katika kanda za pwani ya Kiwengwa kupimiwa wageni na kunyimwa fursa hiyo kwa wananchi.

(a) Je, Mhe. Waziri unalifahamu suala hilo.

(b) Kama unalifahamu Serikali itachukua hatua gani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati -** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 93 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika,

a) Nalifahamu suala hilo.

b) Katika eneo la Kiwengwa viwanja walivyopewa wageni, wananchi walilipwa fidia na viwanja hivyo vilikuwa kwa ajili ya uwekezaji. Hivyo Serikali inaendelea kufanya uhakiki ili kuangalia uwezekano wa kupima maeneo mengine mbali mbali kwa kuwapatia wananchi.

**Mhe. Ashura Sharif Ali:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri ni lini hasa wananchi hao watapatiwa viwanja vyao.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama kwamba serikali inafanya utafiti ili utakapomalizika utafiti huo iwapimie na iwapatie viwanja vyao.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba lipo tatizo hilo na duniani kote wazalendo hupewa kipaumbele.

(a) Je, kwa sasa ni Wazanzibari wangapi wanaomiliki maeneo ya ukanda wa pwani na ni wageni wangapi wanaomiliki maeneo hayo.

(b) Kwa mfumo wanaoendesha kwenye utoaji wa viwanja katika ukanda wa pwani. Je, Mhe. Naibu Waziri anakusudia kunambia kwamba Mzanzibari si muhimu kwa uwekezaji kuliko mgeni.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa sasa sitomueleza kwamba Wazanzibari wangapi na wageni wangapi ambao wanamiliki ardhi katika maeneo ya pwani. Lakini Wazanzibari wapo na wageni wapo ambao tumewapa ardhi hizo.

Mhe. Spika, jibu (b) Wazanzibari ni watu muhimu sana kupewa ardhi na hilo tumelifanya na mnaona kwamba wapo ambao wanamiliki mahoteli na sehemu nyenginezo.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba hivi karibuni kuna Mzanzibari sehemu ya pwani anataka kuwekeza mradi ambao utasaidia wananchi lakini mpaka leo hii anahangaishwa haki yake na kishalipa.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, taarifa hii ndio kwanza naisikia kama kuna Mzanzibari kaomba kalipa na hajapewa hakimiliki yake wala kupewa kibali cha kujenga hoteli yake.

Kuna Mzanzibari eneo la Nungwi aameomba zamani sana kujenga hoteli tumempa kibali lakini mpaka leo Serikali ya Mkoa na Serikali ya Wilaya inamzuia. Sisi kwa kuthamini hayo aliyoyazungumza Naibu Waziri wangu kwamba Wazanzibari na Watanzania tunawathamini sana katika kuwapa nafasi kujenga hoteli. Mwananchi huyu tunaendelea kumlinda na tumemruhusu aendelee na kazi zake za kukarabati hoteli yake. Huyu ni mwenzetu na huyu ni Mtanzania. Ahsante sana.

**Nam. 218**

**Mageuzi ya Kilimo**

**Mhe. Nassor Salim Ali –** Aliuliza**:**

Kwa kuwa kilimo ni muhimu katika nchi yetu na kinasaidia sana wananchi katika kupata chakula na biashara. Bahati mbaya Serikali ya Mapinduzi

Zanzibar haijatoa kauli ya kilimo kwanza kama vile Tanzania Bara na kilimo chetu bado ni cha kizamani cha jembe la mkono.

(a) Je, ni lini Serikali itabadili kilimo chetu na kuagiza vifaa bora vya kulimia kama vile *powertiller* ili wakulima wetu waondokane na vijembe kongoroka.

(b) Nchi nyingi duniani zina sera ya kilimo cha umwagiliaji *(irrigation).* Je, ni lini Serikali itatoa umuhimu wa kuhimiza kilimo cha umwagiliaji hapa Zanzibar.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili –** Alijibu**:**

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Nassor Salim Ali naomba uniruhusu nichukue fursa hii kumuamkia na kumkaribisha Profesa Mhe. Ali Mzee Ali tena kwenye Baraza hili.

Mhe. Spika, sasa kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 218 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Zanzibar pia tunao mpango wa kilimo unaofanana na ule wa Tanzania Bara wa Kilimo Kwanza na unaitwa MAPINDUZI YA KILIMO. Mpango huu umeshatolewa tamko na Serikali na umeelezwa ndani ya ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohammed Shein yupo mstari wa mbele katika kuyaongoza Mapinduzi hayo ya Kilimo.

Mhe. Spika, vifaa kama matrekta na *powertiller* vipo na vinatumika na Waheshimiwa Wawakilishi wakienda mabondeni watavikuta vifaa hivyo vinafanya kazi. Vifaa hivyo vimeanza kutumika Zanzibar baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 yalipoletwa matrekta ya Kichina na Marehemu Baba wa Taifa la Zanzibar Mzee Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar wakati huo. Kwa vile Serikali ilitoa umuhimu wa kilimo baada ya Mapinduzi tu.

Mhe. Spika, kinachofanyika hivi sasa ni kukiimarisha zaidi kilimo kiwe cha kisasa na hivyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imepanga kuongeza vifaa vingi na vya kisasa ili kukidhi mahitaji ya kuongeza uzalishaji kwa eneo na kuwarahisisishia kazi wakulima wetu. Tayari mipango hiyo imeshapangwa na itatekelezwa katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2015. Fedha za Bajeti ya Mpango huo tayari zimetengwa katika Bajeti ya Wizara yangu.

Mhe. Spika, suala la kijembe kongoroka haliwezi kuondoka kabisa kwa vile mfumo wetu wa kilimo mchanganyiko kwa kilimo cha juu na maweni zitaendelea kutumia zana hizo, ingawa zana za kisasa zitatumika kila inapowezekana. Kilimo cha kijembe kongoroka kinatumika na wakulima wadogo wadogo kila nchi kwa vile zana nzito haziingii kila mahala panapolimwa, kijembe kongoroka pia kina faida ya kutunza mazingira.

Mhe. Spika, Sera ya Kilimo cha Umwagiliaji Zanzibar imeanza tokea miaka ya 70 kwa msaada wa Mashirika ya Kimataifa, na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kutekeleza Sera hiyo mpaka sasa. Wizara yangu tayari imeshapima kitaalamu maeneo yanayoweza kulimwa kwa umwagiliaji yenye ukubwa wa hekta 8,521 Unguja na Pemba. Kati ya hizo kwa hivi sasa hekta 700 tu ndio zimo katika mpango wa mwagiliaji na hekta 2,000 zimo katika utaratibu wa kuziwekea miundombinu ya umwagiliaji.

Mhe. Spika, azma ya Serikali ni kuwa na hekta 5,850 za kilimo cha umwagiliaji maji ifikapo 2015. Mipango hiyo imeshaandaliwa na itaanza kuonekana katika bajeti ya Wizara yangu ya mwaka huu.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake alisema kwamba tayari kuna vifaa vya kilimo ambavyo wameshapewa wakulima. Je, ni wakulima wangapi ambao wamefaidika na vifaa hivyo.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali lake hilo. Kwa sasa hivi nitashindwa kumpa idadi ya mkulima mmoja aliyefaidika na zana za kisasa za kilimo. Lakini nataka nimhakikishie kwamba kila bonde la mpunga zana za kisasa zinatumika ikiwemo matrekta na *powertiller*. Tatizo lililokuwepo ni kuwa zana hizo kuwa chache na hazijakamilika ili tufikie malengo ambayo tunayahitaji.

Lakini kama nilivyokwisha eleza kwenye jibu mama kwamba hayo tumeyazingatia na tutayaeleza kwa ufasaha zaidi katika hotuba ya bajeti ya wizara yangu.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, kwa kuwa wakulima waliopo katika ukanda wa mashariki wa kisiwa cha Pemba kama vile Vitongoji, Muwambe na Micheweni huwa wanalima mazao ya msimu *(seasonal crops).* Kwa kuwa wanashindwa kuihami ile bei ya mazao yao yaani ku-*stabilize agricultural price,* hulazimika kuuza mazao yao kwa bei duni sana kipindi cha mavuno jambo ambalo haliwasaidii wakulima.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima wa ukanda ule wa mashariki wanaolima mazao ya msimu ili kuweza ku- *stabilize* ile *agricultural price* pale na hatimae kilimo kile kikawa cha maslahi kwao.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa swali la msingi kabisa. Mhe. Spika, tatizo la wakulima wetu kukosa thamani ya bei ya mazao yao si la ukanda huo wa wakulima wa Pemba aliozungumzia bali ni wakulima wote wa nchi yetu.

Mhe. Spika, Wizara imeliona hilo na tuna mipango mingi ambayo itakwenda sambamba ikiwemo kuwashajihisha, kuwapa taaluma na kuwasaidia wakulima wetu. Moja katika kusarifu mazao yao, pili ujenzi wa masoko ya wilaya ambayo yatakuwa na maeneo ya kuhifadhi mazao hayo, maeneo ya mnada, maeneo ya vyumba baridi kwa mazao ambayo yatahitaji vyumba vya baridi.

Mhe. Spika, jambo jengine serikali pia imezingatia kuwawezesha wakulima kupitia ruzuku ambazo zitatoka lakini hapo papo kuwajengea uwezo zaidi katika kuwapatia fedha ili waweze kuimarisha uwezo waliokuwa nao katika kupanda, kuvuna, kuhifadhi, kusarifu na kuuza kwa wakati ambayo bei itakuwa muafaka kwao.

Kwa hivyo, hata suala la miundombinu ya masoko nalo tumelizingatia na tutalizungumza wakati tutakapowasilisha hotuba ya bajeti ya wizara yangu.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika jibu lake mama alisema kwamba ukenda kwenye mabonde utakuta matrekta pamoja na *powertiller*.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba katika mabonde ya Kirombero na Pangeni vitu hivyo havipo. Kama havipo ana mpango gani wa kuwatafutia wakulima hao *powertiller* za bei nafuu pamoja na matrekta kuweza kuwakopesha.

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, najua Mhe. Mwakilishi anauliza swali hilo kwa sababu anawapenda wakulima wake, anao wengi jimboni kwake. Pia namshukuru kuwa mstari wa mbele katika utetezi wa wakulima na wananchi wa jimbo lake ambapo anatusaidia na sisi pia katika wizara yetu tuweze kuwatumikia ipasavyo wakulima wa jimbo lake.

Mhe. Spika, naweza kwa sehemu nikakubaliana nae Mhe. Mwakilishi kwa sababu sitaki kumkatalia yale aliyoyaeleza, ninaweza kusema yapo na kama hayapo, nakubaliana nae hayapo kwa sababu hayatoshi. Wakulima wamepatiwa

matrekta kupitia mradi wa *PADEP* na miradi mingineyo yao wanayamiliki na yamo katika mabonde, *powertiller* zimo maeneo yote anayozungumzia hayo. Mimi ni mwendaji sana katika mabonde hayo nimeshuhudia tunakwenda pamoja, lakini najua amekusudia kwamba hayatoshi na wananchi wanapaswa kuongezewa vifaa hivyo na pia kuwaandalia utaratibu ikiwezekana wa kuwakopesha.

Hayo yote yanazungumzika na tutayazingatia, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba haja ipo ya kuendelea kuwawezesha wakulima hao.

**Nam. 140**

**Kisiwa cha Pemba Kushirikishwa kwenye Zoezi la Kusahihisha Mitihani**

**Mhe. Rufai Said Rufai –** Aliuliza**:**

Kwa kuwa zoezi la usahihishaji wa Mitihani ya Taifa ya Zanzibar unahitajia mazingira mazuri na salama kwa wasahihishaji, ili kuifanya kazi hii ya Taifa vizuri. Kwa kuwa nchi yetu imeundwa kwa visiwa viwili.

(a) Je, ni walimu wangapi kutoka Pemba ambao hushiriki katika zoezi hili kwa kila mwaka.

(b) Kwa kuwa uzoefu unaonesha kwamba mitihani hii imeshawahi kusahihishwa katika Kisiwa cha Pemba. Ni sababu gani zilizopelekea zoezi hili kutofanyika tena kisiwani huko.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwanza kwa idhini yako naomba unipe fursa ya kumpongeza kwa dhati kwa niaba yangu na kwa niaba ya wapenda umoja wote wa Zanzibar Mhe. Ali Mzee Ali kwa kurudi tena Barazani. Kwa kweli Mhe. Rais hakufanya makosa anajua uwezo, umahiri na utendaji wake. Mhe. Ali karibu sana tujenge Zanzibar mpya.

Mhe. Spika, baada ya hayo, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 140 lenye sehemu (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kuwa kufanikiwa kwa zoezi la usahihishaji wa mitihani yoyote ikiwemo Mitihani ya Taifa ya Zanzibar linahitaji kuwepo kwa mazingira mazuri na salama ili wasahihishaji waweze kufanikisha kazi hiyo

muhimu ya Kitaifa. Pia skuli zinazofanya mitihani yetu zipo katika sehemu zote za visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika,

(a) Katika mwaka 2010, jumla ya walimu 36 kutoka skuli mbali mbali za Pemba walishiriki katika usahihishaji wa mitihani ya darasa la saba na ya kidato cha pili.

(b) Ni kweli kuwa mitihani yetu ya Taifa imeshawahi kusahihishwa katika kisiwa cha Pemba katika miaka ya nyuma. Sababu zilizopelekea kazi hiyo muhimu kutokufanyika huko Pemba katika miaka ya karibuni ni pamoja na kutokuwepo kwa taasisi ya elimu yenye nafasi ya kutosha ya kuwaweka wasahihishaji wote. Pia ukosefu wa umeme wa uhakika kwa miaka ya nyuma na ongezeko la gharama za uendeshaji.

**Mhe. Rufai Said Rufai:** Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba ni muda mrefu suala hili kwa kule Pemba limekosekana kwa sababu ya umeme na mambo mengine.

Je, Mhe. Waziri haoni sasa kwamba Pemba tunao umeme wa kutosha na maeneo ya wizara yake yapo ya kutosha. Hivi sasa si vyema na walimu wa kule Pemba nao wakapata faida kushiriki katika usahihishaji wa mitihani kule Pemba.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, nataka nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba kweli suala la umeme kwa Pemba sasa limemalizika. Lakini suala la nafasi katika taasisi zetu pia kipindi cha karibuni litamalizika kwa sababu kuna skuli zetu hizi mpya tunazojenga bila shaka zitakuwa na sehemu nzuri na kubwa ambazo zitaweza kutusaidia kuweza kufanya kazi hii kwa ufanisi.

Lakini Mhe. Spika, nilitaka niongezee. Mhe. Spika, Zanzibar ni kisiwa cha Unguja na Pemba na umoja na mshikamano wetu ni wa asili. Katika kipindi kama hichi Mhe. Spika, cha zama hizi za umoja wa kitaifa, taasisi za serikali haziwezi kupimwa kwa mshikamano wa visiwa hivi kwa kuangalia labda utendaji wa shughuli za taasisi zenyewe zinafanya vipi au zinafanya wapi.

Muhimu nadhani Waheshimiwa Wawakilishi tungetazama zile shughuli zetu ambazo tunazifanya za mipango ya kimaendeleo ni wapi na wapi zinapelekwa. Nadhani hii ingekuwa ni suala zuri kama Waheshimiwa Wawakilishi kulitazama, kuliko kutazama mitihani inasahihishwa Pemba au inasahihishwa Unguja. Mhe. Spika, mitihani kusahihishwa Unguja haiwezi kutusaidia iwapo

kama wanafunzi wetu itakuwa hawafanyi vizuri na wanafeli katika mitihani yao. Ahsante sana.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri amesema katika jibu lake la msingi kwamba ni walimu 36 ambao wametoka kipindi cha nyuma kutoka Pemba kuja kusahihisha mitihani Unguja.

(a) Je, Mhe. Waziri unaweza kulieleza Baraza hili kwamba ni walimu wangapi wanaotumika katika kusahihisha mitihani kwa kila mwaka.

(b) Kwa kuwa wale Wazanzibari waliopo katika kisiwa cha Pemba na wao ni walipa kodi ambapo kodi hii inasaidia sana katika kuleta maendeleo yetu na kupatikana hizo pesa za kuwalipa walimu katika kusahihisha mitihani. Je, haoni kwamba kusahihishwa mitihani katika kisiwa cha Pemba tutaongeza mori ya walipa kodi wa kule Pemba kuendelea kulipa kodi zao vilivyo ili pesa zipatikane kwa ajili ya kusahihisha tena mitihani.

**Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, idadi kamili ya walimu ambao wanasahihisha mitihani nitamletea Mhe. Mwakilishi, lakini asilimia kubwa ya walimu hao wanatoka katika Wilaya ya Mjini. Kwa sababu Wilaya ya Mjini ina skuli nyingi kwa hivyo na walimu bila shaka itakuwa ni wengi.

Lakini swali (b) Mhe. Spika, kama nilivyojibu swali langu lililopita la nyongeza. Ni kweli na ndio maana nikasema kwamba kutokana na yale matatizo ambayo yalikuwa yakitukwamisha kwa walimu kusahihisha mitihani yetu Pemba sasa yamepungua kwa kiasi fulani wizara haina tatizo na hilo.

**Mhe. Mohammed Mbwana Hamad:** Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inatayarisha mitihani ya darasa la saba na kidato cha pili. Kwa kuwa hakuna Baraza la Mitihani linaloeleweka kama vile Tanzania Bara Baraza la Mitihani la Taifa.

(a) Je, Mhe. Waziri Wizara yako inatayarisha vipi mitihani hiyo hivi sasa.

(b) Je, Wizara ina mipango gani kuanzisha chombo maalum kinachoeleweka ambacho kitasimamia mitihani Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, ni kweli katika Jamhuri ya Muungano kuna bodi ya mitihani, lakini kwa taarifa yake na kwa

hapa Zanzibar tumeanzisha idara mpya ya tathmini na upimaji ambayo ndio inayoshughulikia masuala ya mitihani na ataikuta kwenye bajeti yangu ina maelezo mazuri zaidi, ahsante Mhe. Spika.

**Nam. 216**

**Matengenezo ya Viwanja vya Mnazi Mmoja**

**Mhe. Nassor Salim Ali** – Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hivi karibuni ameelezea nia ya serikali kuvifanyia matengenezo makubwa viwanja vya michezo vya Mnazi Mmoja.

Je, wizara imejipanga vipi kuanza matengenezo ya viwanja hivyo, ili kupunguza tatizo la upungufu wa viwanja vya michezo kwa vijana wetu.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo** – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 216 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, viwanja vya Mnazi Mmoja viko chini ya usimamizi wa Baraza la Manispaa. Tatizo kubwa linalovikabili viwanja hivi ni kutuama kwa maji kwa kipindi kirefu kinachosababishwa na mvua pamoja na kuingia kwa maji ya chumvi kutoka baharini kunakosababishwa na hali ya kijiografia ya eneo hilo. Aidha, Baraza la Manispaa katika ziara ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hivi karibuni walieleza nia yao ya kufanya matengenezo makubwa ya kuhakikisha eneo hilo la Mnazi Mmoja linakuwa juu kupita usawa wa bahari ili kutoruhusu maji ya pwani kuingia eneo hilo.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa ahadi aliyoitoa Mhe. Rais ilipokelewa kwa furaha kubwa na wana michezo wa Zanzibar.

(a) Je, wizara ikiwa ni msimamizi mkuu wa masuala haya ya michezo, Mhe. Waziri anatuhakikishia vipi kuwa kiwanja kile kinatengenezwa ili kuondoa matatizo ya wana michezo wetu hapa Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, hivi karibuni Zanzibar ilijiondoa kuandaa mashindano ya Kagame Cup kutokana na tatizo la uwanja, hata baada ya kufanyiwa matengenezo Uwanja wa Amani. Je, wizara itatuhakikishia vipi

kwamba kipindi kinachokuja, mashindano ya Kagame Cup yatafanyika hapa Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:** Nakushukuru Mhe. Spika.

(a) Kwanza kama Mhe. Naibu Waziri alivyoeleza katika jibu mama kwamba viwanja vya Mnazi Mmoja viko chini ya Baraza la Manispaa, haliko chini yetu. Kwa hivyo, hivi sasa hatuwezi kutia mkono wetu mpaka hapo watakapofanya wenyewe. Kwa sababu hata tukitengeneza hivi sasa itakuwa ni kazi bure, kwa sababu bado panaingia maji. Kwa hivyo, tusubiri shughuli za kiufundi zimalizike chini ya Baraza la Manispaa na wakimaliza na kutukabidhi hapo ndio tutajua hatua gani ya kufanya. Hiyo ni (a) na

(b) Ni kweli kwamba kombe la Kagame mara hii lilikuwa lifanyike Zanzibar, lakini kutokana na matatizo ya kiwanja imebidi lazima tuahirishe. Napenda kumuahidi Mhe. Mjumbe kwamba mwakani tutakapokuwa tumeshamaliza kupanda majani, basi tutaandaa mashindano haya ya Kagame Cup. Kwa sababu majani ambayo yalikuwepo yalikuwa ni majani ambayo yalitiwa na Wachina ambayo hayana asili ya hapa, kwa hivyo yamekuwa hayahimili vishindo. Kwa hivyo, tutapanda yale yale majani ambayo ni *tradition* ambayo yanahimili vishindo. Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe usiwe na wasi wasi mwakani *Inshaallah* tutadhamini mashindano haya, ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri kajibu kwamba viwanja vile viko chini ya Baraza la Manispaa na kwa kuwa kila kukicha manispaa kazi yao ni kuimarisha bustani tu katika mji ule.

1. Je, atakubaliana na mimi kwamba kuendelea kukwama maji katika viwanja vile vya Mnazi Mmoja ni kurudisha nyuma vipaji vya vijana wetu.

2. Kwa kuwa nchi nyingi hufukia bahari ili kupata ardhi na kufanya shughuli mbali mbali zikiwemo za michezo. Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuwacha viwanja vile kutuama maji na kuwa vimekaa tu havitumiki kwa lolote ni matumizi mabaya ya ardhi.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Ahsante Mhe. Spika. Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi ni kweli uko mpango maalum wa kuunda kamati ili kufuatilia kiwanja kile. Pia kama nilivyojibu katika swali mama, kama Mhe. Rais alifanya ziara tukiwa pamoja na Wizara ya Habari,

Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Baraza la Manispaa kuhakikisha kwamba manispaa wenyewe wataanza kazi hiyo ya kuweka bomba kubwa kwa kuelekea kwenye usawa wa bahari ili kuondosha maji yale, ndipo wizara yangu itakapoandaa mpango maalum wa kukitengeneza kiwanja kile kwa maslahi ya wana michezo wa Zanzibar.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, niwaombeni radhi kidogo. Mnajua tumekuwa hatuna utamaduni tunapokuja kwenye mambo makubwa ya kihistoria ya kufuatana na ndugu zetu, wenetu na wengineo. Lakini leo Mhe. Ali Mzee Ali ambaye tumemkaribisha punde tu hivi baada ya kuapishwa, kumbe yeye alifuatana na vijana wake na naomba basi niwatambuwe kuwepo kwao watoto wetu Said Ali Mzee na Abdulrahman Ali Mzee ni wale pale, wamefuatana na mzee wao kumleta hapa, wamemsindikiza na tayari ameshaapishwa karibuni sana vijana.

**Mhe. Mjumbe fulani:** Na mama yao je.

**Mhe. Spika:** Tunaendelea. Mama yao hayupo. *(Makofi/Vicheko).*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa mwaka wa fedha 2011/2012

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah kwa kutuwezesha kukutana hapa tukiwa wazima, salama na amani.

Vile vile nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza mawili au matatu katika kuyatolea hoja au kuyajibu yale masuala ambayo yameletwa na wachangiaji wetu. Pia nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ambaye ni waziri wangu kwa mashirikiano mazuri na makubwa mno katika kuiandaa bajeti hii.

Mhe. Spika, niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Nugwi jimbo la dhahabu, kwa kunichagua mimi kuwa mwakilishi wao. Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwake kuiongoza nchi hii.

Mhe. Spika, vile vile nimpongeze sana Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais Maalim Seif Sharifu Hamad kwa kuteuliwa kwake. Pia nimpongeze Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi.

Mhe. Spika, nimshukuru tena Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuiteuwa timu ya mawaziri iliyokamilika pamoja na Manaibu Waziri. Naamini kwamba Mhe. Rais hakukosea hata kidogo, timu yake iko makini na imejipanga vizuri katika kulitumikia taifa hili, pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Spika, niongeze pongezi kwa Mhe. Rais kwa kukaa yeye pamoja na Mhe. Makamo wa Kwanza na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Spika, serikali hii kwa kweli imefikia katika malengo yanayotakiwa na Wazanzibari. Tukumbuke kwamba katika kipindi cha nyuma Wazanzibari tulikuwa na migogoro, tumegongana, tumechochana lakini tofauti zote *Alhamdulillah* tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sasa zimeondoka. Kilichosababisha kuondoka kwa tofauti hizo ni kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, tunakumbuka kwamba nchi hii imekomboka kwa sababu tu ya Mapinduzi yaliyofanyika mwaka 1964, ingawa wengi ilikuwa bado hatujazaliwa kama mimi, nilikuwa sijazaliwa wala sijakadiriwa, lakini yote yaliyofanyika *Wallah* tunayo na tumeyapata kwa historia ambayo tunaelezwa na viongozi wetu.

Mhe. Spika, wasingeweza Wazanzibari kuipindua nchi hii isipokuwa wamethubutu kuweza kufanya kitendo hicho kwa sababu ya mashirikiano, umoja wao ndio uliowasababisha kuweza kupindua nchi hii na kuuondoa ukoloni. Baada ya kumalizika Mapinduzi hayo, katika kipindi hiki cha kati kulitokea tofauti, lakini Waarabu wanasema Q*ul Hamal Yahuud Walaasil*. Kila jambo basi litarudi katika wakati wake au mahali pale. Leo Wazanzibari tuko kitu kimoja. Sawa sawa na ndugu wa baba mmoja na mama mmoja. Hili ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu sana.

Vile vile Mhe. Spika, niseme kwamba serikali iliyokuwepo katika awamu iliyopita ni serikali nzuri sana na ambayo imefanya mambo mazuri na hiyo ndio iliyoanzisha chanzo cha kujenga au cha kutafuta muelekeo wa Wazanzibari katika kujenga serikali hii ya Umoja wa Kitaifa. Lakini nathubutu kusema kwamba Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa nzuri zaidi.

Labda Mhe. Spika, nitowe mifano midogo tu Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataallah, wakati alipoiumba pepo yake, aliitengeneza pepo hiyo kwa mapambo mazuri, kwa kila kile ambacho tunakijua sisi na tusichokijua kizuri basi kakiingiza katika pepo hiyo. Baada ya kuimaliza pepo hiyo

akamuagizishia Malaika tul Rahman Jibril (AS) na akamwita akamwambia, Yaa Jibril Kundhur ila Janah, nenda kaiangalie pepo

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, samahani sana. Nilisema jana mapema kwamba tuna ufinyu wa muda na leo tunakusudia kumpa Mhe. Waziri muda wa kutosha. Namshukuru Mhe. Naibu Waziri ameshatoa pongezi, ameshatoa namna tulivyowamoja. Sasa nimuombe kwa muda mfupi sana aende kwenye hoja yenyewe ya kumsaidia Mhe. Waziri. Kwa sababu kuna waheshimiwa wengine kutoka upande wa serikali vile vile waweze kumsaidia Mhe. Waziri hatimaye hoja hii tuimalize kwenye hiki kipindi cha asubuhi, nashukuru sana. Mhe. Naibu Waziri tumia dakika kama kumi umalizie maelezo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa hilo, naomba niendelee. Mhe. Spika, nije kwenye bajeti yetu, bajeti hii imechangiwa na wajumbe wengi tu ambao wanafika 28, sitowataja mmoja baada ya mwengine, lakini tu nitajaribu kuyapambanua yale tu yaliyochangiwa na baadhi ya wachangiaji.

Mhe. Spika, nianze na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando, ambaye kaeleza mambo mengi, hususan katika kisima cha Kwa mzungu Kiheshange na kuhusiana na jenereta la kisima hicho pamoja na mengineyo.

Mhe. Spika, kisima cha Kwa mzungu tayari sasa hivi tumeshakifanyia matengenezo na tumeshakifunga *pump* siku ya tarehe 07/07/2011 na *pump* hiyo tayari inafanyakazi na wananchi wa maeneo hayo wanapata maji kutoka katika kisima hicho. Mhe. Spika, kuhusu suala la jenereta. Jenereta hili bado tunalishughulikia na liko kwa fundi, litakapomalizika tu basi jenereta hilo tutalirejesha katika kisima hicho.

Mhe. Spika, nije katika suala la majenereta ambayo yako Shirika la Umeme. Kwanza nataka nijibu kuwa majenereta haya yapo na yapo majenereta 32 na majenereta haya bado mazima hayana tatizo lolote na tumeyatumia katika kipindi cha nyuma, kutoka mwezi wa Agosti, 2010 hadi Machi, 2011.

Mhe. Spika, kama nilivyozungumza katika kipindi cha nyuma kwamba Zanzibar tuna upungufu wa umeme unaosababishwa na *cable* yetu iliyokuwepo baharini, kwamba *cable* ile sasa hivi tayari imeshazidiwa, kwa sababu ina uwezo wa kuchukuwa *megawatt* 45 hadi 40. lakini kutokana na kile kilichotokea katika kipindi cha nyuma, basi *cable* hiyo kwa sasa tunaiingiza umeme *megawatt* 38 hadi 40. Kwa kuisaidia nguvu *cable* hiyo na kuwapatia umeme wananchi wa Zanzibar wa kutosha, tulijaribu kuyatumia majenereta hayo katika kipindi cha nyuma ili kuziongeza megawatt angalau kufikia megawatt 55. Tulikuwa tunazalisha megawatt 15 baada ya megawatt 40

ambazo tunazipata katika *cable* ambayo inatoka Kiromoni, kwa hivyo tukaongeza megawatt 15 na zikawa megawatt 55. Kwa kipindi hicho ikawa kwa kweli Zanzibar hakuna umeme wa mgao. Lakini kutokana na gharama kubwa za majenereta hayo mafuta yake basi ilibidi tusitishe kwa muda kutokana na gharama hizo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nidhibitishe kwamba majenereta hayo yapo hayana matatizo yoyote, lakini kilichokwamisha kwa sasa ni fedha za kununulia mafuta ambazo zitatumika kwa majenereta yale. Gharama ya matumizi katika majenereta hayo kwa sasa kama tutayatumia basi itabidi lazima tulipe kwa kila *unit* Shs. 394/=, kiwango ambacho kwa kweli kitakuwa ni kikubwa mno kwa sababu kwa sasa wananchi wanalipa kwa kila *unit* Shs. 120/=. Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala hilo huo ndio ufumbuzi wake na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakapotujaalia kupata fedha basi tutayatumia majenereta hayo na tutahakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wananufaika na majenereta hayo kwa ajili kuwaongezea kiwango cha umeme.

Mhe. Spika, kuhusu uvamizi wa fukwe katika eneo la Maruhubi. Suala hili kwa bahati nzuri vile vile lilileletwa na Mhe. Mtando. Tumelizungumza katika Baraza hili kwa bahati nzuri baada tu ya kumaliza kikao ambacho tulilijadili suala hili siku hiyo, niliondoka mimi, kamati pamoja na Mhe. Mtando tukalifuatilia suala hili na baada ya kulipatia uhakika wizara yangu imetoa uwamuzi rasmi wa agizo ambalo alilolituma kwa mwekezaji huyo na kumtaka mara moja asitishe uvamizi huo wa ujenzi huo. Kwa hivyo, wizara yangu imejitahidi kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la uvamizi wa ardhi katika Mkoa wa Kaskazini. Mhe Spika, nathibitisha kwamba suala hilo kweli lipo na hususan katika maeneo yaliyotajwa ikiwemo Nungwi, Kendwa, Kidoti pamoja na Fukuchani kweli kuna uvamizi wa ardhi. Lakini suala hili nilizungumza kipindi cha nyuma katika kujibu maswali nilisema kwamba hilo lipo na kuna baadhi ya wajanja ambao huwa wanashirikiana na baadhi ya watendaji wetu wa serikali, wanashirikiana na kufanya uvamizi huu au nakufanya dhulma hii. Lakini wizara yangu kwa suala hili sasa hivi, kama alivyoeleza waziri wangu kwamba tumeshajipanga na tutalivalia njuga kikamilifu kulifuatilia suala hili na wale wote ambao wanashiriki katika kufanya dhulma hizi, basi *Inshaallah* tutawafanyia kazi.

Mhe. Spika, nije katika suala la nguzo za umeme. Nakiri kwamba kwa sasa hivi tunazo nguzo nyingi mbovu, lakini shirika langu tayari limeshawasilisha nguzo 2,700 na hizo zimeletwa kwa ajili hiyo. Lakini kwa sasa tumeanza kuzifanyia marekebisho line za HT, baada ya kumaliza marekebisho *line* hizi, basi tutaelekea katika *line* za LV na tutazifanyia mkarekebisho kama vile ambavyo

inavyostahiki. Naamini kwamba shirika langu linathamini sana wananchi na linapopokea taarifa basi liko karibu sana kuzifuatilia taarifa hizo na kujitahidi kuzifanyia kazi kwa kuendelea na matengenezo.

Mhe. Spika, naomba ikumbukwe kwamba shirika ni dogo na halina wafanyakazi wa kutosha. Sio kweli kwamba itatokea taarifa ya kuanguka nguzo Makunduchi iunguwe *transformer* Nungwi, iunguwe *transformer* kwengineko kwa wakati mmoja zote kisha masuala yale yote yafanywe kwa wakati mmoja, nawaomba sana wananchi wawe na subra ili pale linapotokea tatizo kwanza lirekebishwe huku, baadae lirekebishwe upande mwengine.

Mhe. Spika, nije katika suala la mita. Kuna Mhe. Mwakilishi katuuliza kwamba tumejipanga vipi katika ufungaji wa mita na mita za aina gani tunazotaka kufunga. Nimthibitishie tu Mhe. Mwakilishi kwamba kwa sasa hivi shirika langu rasmi litafunga mita za TUKUZA, hatufungi tena mita za kawaida na tutaendelea kufunga mita za TUKUZA kwa Unguja na Pemba. Kila utakapofikia muda na tutakapopata fedha za kutosha basi tutaziondoa zile mita za kawaida kwa sababu tumegundua kwamba mita hizi za kawaida kwa upande fulani zinatutia hasara shirika sana, pamoja na serikali na wizara kwa jumla. Hususan kutokana na wizi wa umeme uliokithiri, watu wengi wanatumia umeme kwa njia ambazo hazistahiki, hususan kwa kupitia mita hizi. Aidha kwa kuzisimamisha au kuzitoa sehemu zinazohusika za mita na kutumia njia ya moja kwa moja. Kwa hivyo, baada ya kuligundua hili, shirika langu sasa hivi litafunga mita za TUKUZA, mita hizi ambazo baada tu ya kufungwa na utakapozigusa tu kwa ajili ya kutaka kufanya wizi au jambo jengine lolote basi zitaturipoti na hutoweza kufanya kitu kama hicho.

Baada ya hayo Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kwa niaba ya Jimbo langu la Nungwi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia zote. Ahsante sana nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi).*

**Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Haji Faki Shaali):** Nakushukuru Mhe. Spika. Mhe. Spika, mimi dakika kumi zinanitosha. Awali ya yote mheshimiwa baada ya kukushukuru wewe kwa kunipa fursa. Naomba pia nichukuwe fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Mhe. Ali Juma Shamuhuna pamoja na timu yake yote ya wizara hii kwa majukumu mazito wanayotekeleza siku hadi siku.

Mhe. Spika, ni lazima tukiri kwamba mwenzetu huyu ana kazi nzito. Kwa sababu tatizo kubwa la nchi hii sasa hivi ni migogoro ya ardhi anayo Mhe. Shamuhuna, tatizo kubwa la nchi hii maji kayabeba Mhe. Shamuhuna, tatizo kubwa la nchi hii ni umeme kabeba Mhe. Shamuhuna, tatizo kubwa la nchi hii wananchi makaazi ni yeye Mhe. Shamuhuna. Kwa kweli mwenzetu

tumembebesha mzigo mkubwa lakini *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atavuka salama wa salmini.

Mhe. Spika, pamoja na mzigo mzito tuliombebesha mwenzetu, mimi nafarijika sana na jambo moja tu kutoka kwake, uzalendo wake aliokuwa nao. Kwa kweli mwenzetu ni mzalendo na mimi kwa kipindi kifupi nilichokaa katika serikali hii, jambo nililojifunza kutoka kwake ukiwacha huo uzalendo ni kwamba mtu aliyekuwa makini na sio mtu aliyekuwa goigoi.

Kwa hivyo, Mhe. Shamuhuna nimejifunza kutoka kwake kwamba ni kiongozi kwanza ana uzalendo wa hali ya juu, ana msimamo na wala sio mtu goi goi na imani yangu mimi inavyonambia kutokana na uzalendo wake na kwamba sio mtu goi goi, hata siku moja Mhe. Ali Juma Shamhuna hataweza kuyabadili maamuzi ya Baraza la Mapinduzi wala maamuzi ya Baraza lako tukufu la Wawakilishi ambalo tayari amefanya mwaka jana hawezi hata siku moja kufanya hivyo.

Lakini mimi ninavyofahamu Mhe. Ali Juma Shamhuna amesimama kidete kulinda maamuzi ya Baraza lako tukufu la Wawakilishi pamoja na maamuzi yaliyofanywa na Baraza la Mapinduzi kuhusu suala zima la mafuta, huo naona ndio msimamo wake na msimamo wa serikali yake.

Lakini jengine ambalo mara kwa mara Mhe. Ali Juma Shamhuna huwa anasema ni kwamba mwendawazimu usimpe rungu ni kauli yake ya mara nyingi anapenda kusema, kwamba mwenzawazimu usimpe rungu ukimpa rungu atapiga hana samahani atapiga tu. Nadhani katika suala la mafuta itakuwa msemo wake umesibu kwamba ni sawa sawa na mwendawazimu uliyempa rungu, kwa hivyo mimi napenda kuwatoa mashaka wote wanohisi labda Mheshimiwa uzalendo wake umepungua, labda suala la mafuta litayumba mimi napenda waelewe kitu kimoja tu.

Mhe. Waziri aliyepita Mhe. Mansour Yussuf Himid alikuwa anasimamia maamuzi ya serikali na waziri aliyekuwepo sasa anasimamia maamuzi ya serikali, kwa hivyo hata kama mtu hapendi jambo lile madam anasimamia maamuzi ya serikali hana namna lazima atalitekeleza ukiacha mtu ambae jambo hili ana uzalendo nalo na analipenda. Kwa hivyo mimi napenda kuwatoa mashaka wenzangu kwamba tujenge imani nzuri kwamba Mhe. Ali Juma Shamhuna ataweza kulisimamia suala hili kwa ukamilifu na ushahidi wa hayo mimi napenda kunukuu ukurasa wa 61 wa hotuba yake, nadhani wengine kwa bahati mbaya sana katika kuchangia tulikuwa hatupitii tena katika hiki kitabu.

Ibara 113 anasema hivi:-

> "Mhe. Spika, suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia limepewa kipaumbele, bado msisitizo umewekwa katika kuihusisha nishati hii kuwa ni muhimili mkubwa wa uchumi wetu na kwa kuwa uchumi sio suala la muungano, ushughulikiaji wa rasilimali ya nishati hii haupaswi kuwa suala la muungano"

Mhe. Spika, hivyo waheshimiwa wajumbe walitaka zaidi ya kauli hii atoe kauli gani kwa sababu hizo kauli zote tulizochangia nadhani ilikuwa tunaogolea ndani ya kauli yake, sasa mimi nawanasihi sana wenzangu sana kabisa kwa heshima zote nathamini michango yote ya wawakilishi waliyochangia nawaheshimu sana rai zao, naheshimu sana maelekezo yao. Lakini kwa kauli hii anaeleza bado msimamo wa Wizara yake na msimamo wa serikali kusema upo pale pale, kwa hivyo hapa hakuna kutetereka hapana kuyumba, mimi nawashauri wenzangu tuunge mkono hoja hii mia kwa mia.

Kwa dhamira yake hii nzuri tusimuangushe Mhe. Waziri, haifai hata kidogo kumuangusha kwa sababu kaonyesha msimamo thabiti wa kutetea maamuzi ya Baraza la Mapinduzi na maamuzi ya Baraza la Wawakilishi yaliyofanywa kuhusu uchimbaji wa suala la mafuta.

Mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa jambo jengine ukisoma vile vile katika kitabu hiki ibara ya 121 mpaka ibara ya 123 ya kitabu chake cha bajeti, kimsingi Mhe. Spika, Ibara hizi zinazungumzia suala la kuwatayarisha wataalam watakaoshika na suala la mafuta, inazungumzia suala la kupeleka watu masomoni na Mheshimiwa lazima tukubali uchimbaji wa mafuta ni tofauti na uchimbaji wa maji, maji ukishayachimba utaalam wake mdogo hakuhitaji sana wataalam katika ku-*suply* lakini mafuta ni tofauti, mafuta kuanzia utafutaji wake, uchimbaji wake mpaka hatua zote unahitaji hatua zilizobobea ambao kwa sasa hivi hatunao, alichokieleza Mhe. Waziri katika hotuba hii ni kwamba tayari sasa hivi ana juhudi za kuelimisha hawa watu hili jambo likija hawa wazalendo wawepo.

Mhe. Spika, lazima tukubali kama utaamua kuchimba mafuta katika nchi ukategemea wageni kutoka nje mia kwa mia mafuta yote utakayochimba yataporwa, lakini kwa hatua hii ya kuanza kuandaa wataalam kabla hatujaingia katika mchakato wenyewe nadhani tungeshukuru sana kwamba kweli maandalizi yapo na dhamira ipo, wakati mwengine bora uchelewe kidogo lakini ufanye jambo lenye uhakika kuliko kuharakisha ukaja kuchimba mafuta ukapata asilimia tano tu ya yale mafuta faida yote ikachukuliwa nje.

Mhe. Spika, tuna uzoefu wa nchi nyingi kuhusu suala hili, kuna nchi nyingi ukiziangalia hasa wenzetu warabu mafuta wamekuja wataalam hawana wataalam wa ndani mafuta yameporwa hata walipoandaa wataalam wao nusu

ya ile rasilimali imeshaporwa kwenda nje, sasa mimi nawanasihi wenzangu kwamba haya mafuta tuyachimbe lakini yawasaidie Wazanzibari wenyewe sio yachimbwe lakini yakasaidie watu wa nje. Vipi yatawasaidiwa Wazanzibari wenyewe kwanza ni huko kuandaa wataalam wetu wenyewe ambao watashirikiana na wageni katika mchakato mzima wa uchimbaji na utafutaji wa mafuta, lakini tuka- *rash* sana halafu mafuta yakaporwa itakuwa faida hatuna.

Kwa hivyo tumejifunza kutokana na makosa ya wenzetu hatujachelewa na inshaalla kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu chini ya uongozi wa Mhe. Ali Juma Shamhuna na Wizara hii *Inshaallah* atatuvusha salama na tatizo hili, kwa hivyo mimi nawanasihi wenzangu wote katika baraza hili ambao wanakerwa na uzalendo, uzalendo umewakaa lakini mimi ushauri wangu ni kwamba hili suala la mafuta ni suala la uchumi, suala la mafuta sisi ni la kiuchumi na tusilifanye kuwa la kisiasa.

Mimi nadhani suala la mafuta tuliache liwe la kiuchumi na ndio ilivyo hili suala sisi tumeyatoa mafuta kwa sababu ya kiuchumi sio kwa sababu ya kisiasa, sasa kama tutabakia na dhamira hiyo kwamba mafuta tunataka kuchimba kwa sababu ya uchumi hata wenzetu wa bara watatuelewa hawa wenzetu kweli wana sababu za kiuchumi. Lakini isionekane kwamba tunatoa mafuta kwa sababu za kisiasa nadhani itatuletea matatizo.

Mhe. Spika, baada ya mchango huo niseme naunga mkono hoja na nawaomba wenzangu wote waunge mkono hoja, nakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia katika hoja hii. Pili naomba nichukue fursa hii kumpa pongezi Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na watendaji wake, kwa kulitekeleza vizuri jukumu ambalo serikali imewakabidhi.

Kwa kweli kama walivyotangulia Waheshimiwa Wajumbe walivyosema, kwamba hii ni wizara ambayo inahitaji kutokana na ukubwa wake pamoja na unyeti wake, basi watu makini kama Mhe. Ali Juma Shamuhuna. *(Makofi)*

Naomba nichangie katika maeneo mawili tu Mhe. Spika, ambayo yamezungumzwa sana. Eneo la kwanza ni kuhusu suala la migogoro ya ardhi. Katika suala hili Mhe. Spika, naomba niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili, kwamba ni vyema tuipambanue migogoro ya ardhi, kwa sababu kuna migogoro ya ardhi ya namna mbili.

Kwa mfano, kuna migogoro ya ardhi ambayo inatokana na wananchi wenyewe. Kwa hivyo, mimi niseme kwa kiasi kikubwa unaweza kuita ulalamishi wa

ardhi. Vile vile iko migogoro ambayo inatokana na usimamizi wa ardhi, ambayo ndio inayosimamiwa na watendaji wa serikali.

Lakini naomba nilihakikishie Baraza lako tukufu Mhe. Spika, kwamba migogoro mingi ambayo iko katika Mahakama ya Ardhi, basi ni migogoro ambayo inayotokana na ulalamishi wa ardhi. Mhe. Spika, katika hili naomba niunge na maneno ya Mhe. Rashid Seif Suleiman, alieleza vizuri kwamba hube tuiangalie hii migogoro hakuna ambayo inayoweza kutatuliwa bila ya kwenda Mahakamani.

Mhe. Spika, kwa kweli katika migogoro inayokwenda Mahakamani asilimia 80 ni migogoro ambayo tungeweza kuitatua kama tungekuwa na taratibu katika majimbo yetu pamoja na maeneo yetu ya kuweza kuwasikiliza wananchi wetu na kuweza kusuluhishwa. Kwa hivyo, naamini asilimia karibu 20 tu, ndio migogoro ambayo ingeweza kushindikana na kuhitaji kwenda katika Mahakama ya Ardhi.

Kutokana na hali hiyo, basi niwaombe Waheshimiwa Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kwa sababu kuna mtindo. Kwa mfano, mtu anaweza kuja hapa na waraka wa 1930 akaja kulidai hili jengo la Baraza la Wawakilishi, kusema hili jengo ni la kwake kwa sababu waraka anao na suala hilo likawafikisha Mahakamani. Mhe. Spika, kesi za namna kama hii ziko nyingi Mahakamani, kwamba mtu katika kupekuwa amekuta waraka wa 1920 au 1929 ama 1930 anakuja na kudai na baadaye kwenda Mahakamani.

Kwa hivyo, mimi naomba kwenye hili Waheshimiwa Wajumbe niwaombe sana kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hebu hii migogoro tuisikilize, kwa sababu iko mingi ambayo tunaweza kuwasaidia wananchi wasiende Mahakamani.

Kwa kweli kutokana na migogoro iliopo hivi sasa, basi hata kama hiyo Mahakama yetu yote itakuwa inashughulikia migogoro au kesi za ardhi, basi bado zitaendelea kuwa nyingi, kwa sababu kesi ni nyingi sana.

Sasa katika hili la kuongeza uwezo wa watendaji au kuongeza watendaji, mimi nilikuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi ya Mahakama, kabla ya leo Mhe. Spika kututangazia kwamba ile Sheria ya Utumishi wa Umma. Kwa maana hiyo, ile Tume ya Utumishi wa Mahakama sasa inasita na tuliteua Mahakimu wawili wa ziada, ili kuongeza nguvu katika hili. Kwa hiyo, bado tatizo hili litaendelea. Lakini mimi niwaombe katika hili.

Kwa upande wa serikali nadhani kama tutaongeza nguvu, kwa sababu tulianza utaratibu huu wa kuondoa matatizo ya migogoro ya ardhi tokea miaka ya 1980 tulipopitisha Sheria 7 za Ardhi, yaani kuanzia mwaka 1989 mpaka 1994, ili

kutandika utawala mzuri wa ardhi. Lakini usimamizi wa sheria zile hasa ile *process* ya *judication* ilikuwa inahitaji fedha nyingi. Mhe. Spika, tutakumbuka tulipoanza utekelezaji wa sheria zile mwaka 1996 tukaanza kugomewa na wafadhili, hivyo utekelezaji wake ukawa mgumu.

Kwa hivyo, nadhani hivi sasa ni suala la kurudi katika utaratibu ule ambao tulioutandika, nafikiri tutakuwa na misingi mizuri ya kuweza kuitatua ile mizozo ambayo ipo hivi sasa katika ardhi na kuweza kuondokana na tatizo hilo.

Eneo la pili ambalo nilisema nichangie kidogo ni suala ambalo limezungumzwa sana kuhusu mafuta. Mhe. Spika, labda na mimi nianze kwa kuipa pongezi serikali. Kwa kweli kuipa pongezi kwa kuona mbali na kuchukua hatua hizi kabla hata haijapewa maelekezo na Baraza la Wawakilishi, kulisimamia jambo hili na mpaka kulifikisha kulileta mbele ya Baraza hili tukufu. *(Makofi)*

Jambo la pili naomba kwa dhati kabisa nilipe pongezi Baraza hili, nalo pia kwa kuona mbali na kusimama na serikali katika kuhakikisha kwamba tunaondoa uwezekano wa kugombana huko tunakokwenda. Mhe. Spika, kule Pemba kuna msemo wanasema "kimbia ugwe usigeona ng'ombe", yaani uanze kukimbia hatari kwa kuisikia na wala usisubiri mpaka ikafika ndio ukaanza kuikimbia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, katika hili ndio maana kidogo huwa ninapata shida ninaposikia kauli za hivi sasa, maana kuna mwana-*philosopher* mmoja *confusions* naomba kunukuu kidogo Mhe. Spika. "*at the time of building a common front a grain can tillte the skill*", maana yake ni kwamba wakati mnapo tengeneza msimamo mmoja, nguvu moja, basi ile punje moja inaweza ikawaharibia mezani ikatenguka. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba kila punje, basi ni muhimu iwepo katika upande unaohusika wa mizani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye suala hili nadhani nguvu ya Zanzibar si Mwakilishi mmoja mmoja wala nguvu ya Zanzibar si Wawakilishi peke yao. Lakini nguvu ya Zanzibar ni serikali, wawakilishi pamoja na wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe, kwamba suala hili lilianza baada ya kuzuiwa serikali tena wakati ule tumegomewa na wafadhili ikazuia *Antrim Resources* isifanye *exploration* baada ya kupewa leseni na kibali na *TPDC*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, *Antrim Resources* ilitoka Canada na sote tunajua. Vile vile tunajua wakati ule nani walikuwa vinara wa kuhakikisha Zanzibar inagomewa. Sasa kama wakati ule serikali ilikuwa jasiri ikachukua hatua hiyo, unapata shida leo

mtu anapokuwa na wasi wasi na ujasiri wa serikali na *resolve* ya serikali katika kulisimamia jambo hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi binafsi nilipata bahati ya kwenda Nigeria mwaka 2009. sasa nilipokwenda nilipata bahati ya kukuta na wale Wawakilishi wa *Niger Delta*, ambao wenyewe moja katika utambulisho wao ni kuvaa kofia nyeusi.

Vile vile nilizungumza nao kwani kiini cha mgogoro kitu gani, basi wakanieleza waliyonieleza, lakini moja wakaniambia hebu ukirudi tafuta kitabu cha Peter Mass ameandika kitabu hiki *Croad World* na sio *Croad Oil, the violent to leat of oil*.

Mhe. Spika, katika *Chapter* anaeleza uozo wa mafuta, naomba uniruhusu ninukuu. Lakini ameeleza umuhimu wa kuwa makini katika suala hili nasema hivi: "*Who own this, The discovery of oil usually on arth this caousion*, maana yake mkiyadundua tu suala la mwanzo linakuja nani mwenyewe, hili halina majibu kama hamkuwa na utaratibu makini basi mtapigana kuanzia nyinyi wenyewe kwa wenyewe, mtapigana kama mnao mfumo wa Ki-*Federal* baina ya *state* na *Federal Government*, pia mtapigana baina ya nyinyi na makampuni.

Lakini mwisho anasema au ushauri aliotupa *even in Norway and Canada countries with conhencive political institutions, this question required considerable time and effort to satile*. Mhe. Spika, anasema hata nchi kama Norway na Canada ambazo zina mfumo usiokuwa na matatizo wa kiutawala, basi jambo hili lilihitaji juhudi, muda na umakini katika kulitatua na kuliweka sawa.

Mhe. Spika, naomba yeyote atayekuwa tayari na kuwa na hamu ya kukisoma, basi ningesema na *compulsory reading* pengine kwa kila Mhe. Mwakilishi na ingetusaidia kufahamu suala hili. *(Makofi)*

Sasa serikali kuchelewa kwanza Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliuliza hapa na kusema kwamba tunayo Sheria ya Mafuta ile ya mwaka 1951 *Chapter* 108. Mhe. Spika, nadhani ningemjibu kwa ufupi tu hatuna sheria hiyo na tunahitaji kutunga sheria. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hatuna sheria hiyo, kwa sababu baada ya kuingia katika Muungano marekebisho yote ya Katiba yanakuja na Sheria inayoitwa *Consiqenso Transison Temporary Provision*, ambayo Sheria ile ndio inayosema kwamba sheria nyengine ambazo kabla ya Muungano zilikuwa si za Muungano utaratibu wake utakuwaje.

Kwa mfano, naweza kusema kwamba tunayo sheria kabla ya Masuala ya Usalama wa Taifa kuwa ni mambo ya Muungano mwaka 1984 Zanzibar tulipitisha Sheria ya Usalama wa Serikali na Siri za Serikali ya mwaka 1983. Lakini tulipoyaingiza ikatungwa Sheria Nam. 19 ya 1984, ambayo katika kifungu cha 5 ilisema, kwamba zile sheria ambazo zilikuwa zikitumika Zanzibar kwa masuala haya ya usalama, basi hazitotumika tena badala yake itakuwa inatumika Sheria ya Jamhuri ya Muungano. Sasa hili ni jambo la kawaida, kwa hivyo *Existing Law Decree No*. 1 ya 1964 pamoja na kwamba pale mwanzo ilii-*save*, lakini ulipokuja Muungano automatical sheria hii ilikosa nguvu. Sasa kwa nini imeingizwa kwenye mswada ili ifutwe, kwa sababu ni lazima iondolewe katika *Records* za Vitabu vya Sheria, ndio maana ipo katika mswada.

Mhe. Spika, nadhani kama Mhe. Ismail Jussa Ladhu atataka kulisoma zaidi kwenye hili, basi anaweza kwenda kwenye *Case* ya Seif Sharif Hamad *verses* SMZ, yaani hii ni Kesi ya Rufaa ya Jinai 17192, ambapo Mahakama ya Rufaa ilitoa ufafanuzi na shule ya kutoka katika masuala kama haya. *(Makofi)*

Lakini suala la pili sasa kwa nini sheria inachukua muda. Mhe. Spika, naomba tukubaliane kwamba kuwa na Sheria ya Uchimbaji wa Mafuta, maana yake tunaweka mfumo wa kuwakaribisha wawekezaji katika Sekta hii. Sasa unapowakaribisha wawekezaji katika sekta hii na hii si sekta ambayo serikali yenyewe itawekeze.

Kwa hivyo, moja katika jambo ambalo wanalihitaji wawekezaji katika sekta hii, kwa sababu si kawaida na labda kama anayo taarifa anaweza kunikosoa kwamba katika sekta hii au uwekezaji sekta hii watu kufanya kwa *Equite Financic*. Mhe. Spika, katika sekta hii wawekezaji mara nyingi wanachukua fedha za watu na sio fedha zao za mfukoni. Lakini la pili wanajua kwamba hii ni sekta yenye mzozo. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, jambo la mwanzo wanapokuja wanakitu wanaita *conditions presidency*. Kwa hivyo, *condition presidency* ile moja ni kwamba uwahakikishie na anayetakiwa afanye hivyo ni Mwanasheria Mkuu, kuwa mfumo wenu wa sheria au kuingia kwenu mkataba ni halali, *authority* mlionayo ni halali kwa mujibu wa sheria na mfumo wa nchi yenu, wao hawatopata tatizo wala kikwazo kwa sababu tu ya mfumo wenu wa sheria, yaani hiyo unaji-*commit* na kuwaandikia kuwa hampati chochote.

Mhe. Spika, wanakuletea maswali na wewe mwenyewe ndio unajibu, yaani unajiingiza na anayetakiwa atoe *grantee* hiyo ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sasa nasema kama wakati huu nitakuwa Mwasheria Mkuu wa Serikali kama hatujalitatua jambo hili kwa taratibu ambazo zikawa wazi, basi naamini hata Mhe. Mjumbe yeyote humu ndani hatoweza kutoa *grantee* ya kisheria, isipokuwa atatoa *grantee* ya kisiasa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hatua yote hii tunayofanya ni ya kisiasa, lakini tutafika pahala tutatakiwa tutoe grantee ya kisheria. Kwa maana hiyo, ni muhimu jambo hili kulitatua Kikatiba, pia katika misingi yote ya kisheria ndio itakayowawezesha wawekezaji kuja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama ingekuwa jambo rahisi Serikali ya Muungano inao uwezo mbona hawajaja kuchimba. Hivyo, kwa hizi block zenye matatizo hatokuja kutoka Bara wala Zanziabr mpaka tutakapolitatua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, unapokuwa na mgonjwa kitandani kama hamkuwa makini basi mnaweza mkamalizana nyiye wazima kwa kuuana na mgonjwa akakosa muuguzaji na atakapokufa akakosa labda majirani ndio wanaweza kumzika kwa kuondoka na hayo inakuwa si maziko, isipokuwa wamekwenda kumfukia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba kwenye suala hili ni vyema tuwe makini, ndilo jambo kubwa ambalo naweza kusema. Mhe. Spika, Wakojani wanao msemo “Mungu lete baa iondoe balaa”. Kwa kweli hali hii tuliyonayo ya mvutano wetu wa kimuungano hii ni balaa, sasa na ije hiyo baa ya marekebisho ya Katiba, ili hii balaa ipate kuondoka kwa salama.

Lakini hakuna njia ya mkato na labda Mhe. Waziri atakapokuja ataeleza juhudi tunazofanya.

Mhe. Spika, ninachoweza kusema serikali katika hili haiwezi ku-*negotiate* tena kwamba liwemo jambo la mafuta kwamba la muungano au sio la muungano hayo maelekezo yalishatoka hapa ndani ya Baraza hili na serikali haiwezi ku-*negotiate* tena itakuwa inakwenda kinyume na maelekezo ya Baraza hili, serikali inachofanya sasa hivi ni kutekeleza maelekezo ya Baraza hili, lakini mmetutuma hamkututomesha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kilichofanya Baraza hili ni kututuma serikali sio kututomesha na kutumika kuna mbinu na taratibu tukikosea mtakuja kutulaumu sisi tumekosea, kwa hivyo tuachieni tutumike na tunawahidi kuwatumikia na ninaamini hili jambo litafika wakati wake litakuwa.

Mhe. Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja na nawaomba wenzangu wote hili tulipitishe ili tuendelee kufanya kazi. Ahsante sana *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa katiba na Sheria:** Mhe. Spika, na mimi napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika Wizara hii. Napenda pia nimpongeze Mhe. Waziri wa wizara hii kwa maelezo yake mazuri ambayo aliyatoa katika hotuba yake, mimi nimeomba kuchangia kwa mambo mawili muhimu, lakini bahati nzuri mambo haya ameyagusia sana Mhe. Mwanasheria Mkuu sasa mimi nitaongezea tu mle ambamo kidogo amemuacha.

Mhe. Spika, kwanza naomba nije Mahakama ya Ardhi suala hili lilizungumzwa na wajumbe wengi walizungumza sana wakatoa maoni yao na wasi wasi wao, na mimi nasema kwamba wasi wasi wao ni kweli na maoni yao ni kweli kwamba kuna kesi nyingi sana katika Mahakama ya Ardhi kwa Unguja si chini ya kesi 350 na kwa Pemba nafikiri ni kesi 180 kama hivi.

Mhe. Spika, tutizame katika kesi zote hizi hakimu aliyepo kwa Unguja ni moja na Pemba ni mmoja, kwa hivyo ukichukua kila kesi kama itachukua wiki moja angalau kuimaliza inahitaji si chini ya miaka mitano kumaliza kesi hizi ambazo zipo, seuze kesi ambazo zinakuja leo kesho na keshokutwa. Kwa hivyo tuna tatizo hilo na tatizo hilo tumeliona na baada ya kuliona Mhe. Waziri wa wizara hii kwa kushirikiana na sisi tumeliona na tumejitahidi na tutazidi kujitahidi katika kulisawazisha tatizo hili, hivi sasa tumeshateua Mahakimu wengine wawili ambao watasaidia Mahakama hizi, mahakimu hao mmoja atakuwepo Pemba na mmoja atakuwepo Unguja ili kusaidiana na Mahakimu wenziwao hawa ili kuondoa hizi kesi ambazo ni nyingi sana naamini kwamba mahakimu hao hawatoshi, lakini kama unavyojua Mahakimu wanatoka katika Wizara yetu na hivi sasa tuna upungufu wa Mahakimu.

Lakini napenda kuwahakikishia waheshimiwa wajumbe kwamba pale ambapo tutapata ongezeko la mahakimu basi na Mahakama hizi za Ardhi tutazidi kuziongezea ili matatizo haya ya ardhi yaweze kuondoka, kwa hivi sasa kwa kuanzia tutakuwa na Mahakimu wawili ambao watafanya kazi hapa naamini kwamba watasaidiana sana na mwenziwao aliyekuwepo pale ili angalau kulipunguza tatizo hili.

Mhe. Spika, suala la pili limezungumzwa sana na Mwanasheria mimi ninachotaka kusema hapa ni kwamba mimi binafsi kila mwakilishi anajua msimamo ambao tumeutoa katika baraza hili tukufu katika mwaka 2009, msimamo ule ndio maagizo ya Baraza lako tukufu hakuna chombo chengine ambacho kinaweza kwenda kinyume na msimamo ule. Kwa hivyo ninachosema sisi kama ndio tuliopewa majukumu ya kufuatilia hayo tutaendelea kuyafuatilia, lakini katika ufuatiliaji kuna utaratibu wake na hasa katika haya mambo ambayo yaahusiana na masuala ya muungano, lazima tukae tutizame

njia na mbinu ili kuweza kupata hilo ambalo tunalihitajia na hiyo ndio kazi tunayofanya. *(Makofi)*

Sasa naomba kwa Waheshimiwa wawakilishi watuamini kwamba kazi hii sote inatukera, sote inatuuma kwamba hichi kitu ni chetu na hatutokubali hata siku moja kuporwa au kuchukuliwa na mtu mwengine, kwa hivyo tutaendelea kupigania suala hili mpaka hapo ambapo suala hili litakaa vizuri. Katika masuala haya kuna utaratibu mkubwa tu na mwingi wa kufuata ili kuhakikisha kwamba hili suala linakuwa kwa ajili ya Zanzibar, hatuwezi tena hapa kuzungumzia hapa kwamba liwemo katika orodha ya muungano, ni suala ambalo limeshazungumzwa na ambalo limeshapitishwa na Baraza hili hakuna mtu ambae atakwenda kinyume na hayo. Sasa hilo napenda sana waheshimiwa wajumbe walielewe hivyo. *(Makofi)*

Lakini kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu alielezea akasema kwamba kuna sheria wanaita *chapter 108* ambayo hii inazungumzia suala la *meaning* ya *oil* sheria hii kweli ipo na ni ya zamani na kweli haijafutwa, lakini tujue tu kwamba hapa nyuma kidogo suala hili lilikuwa katika orodha ya muungano kwa sababu lilikuwa katika orodha ya muungano kuna sheria nyingi ambazo zinasema kwamba kile kitu ambacho kimeingizwa katika mambo ya muungano kwa hivyo *automatically* kama kutakuwa na sheria Zanzibar au hata Tanganyika ikiwa ni suala la muungano kwa hivyo *automatically* sheria zile zinazozungumzia masuala yale kwa Zanzibar na Tanganyika zile zitakuwa hazi *apply*.

Kwa hivyo ni kusema kwamba sheria ile ipo katika vitabu vyetu lakini haiwezi kutumika, kwa maana hiyo ndio utaona kwa mfano kuna sheria nyingi tu kwa mfano sheria ya *immigration*, sheria ya polisi ile na sheria nyengine nyingi bado zimo katika vitabu vyetu vya sheria lakini haziwezi kutumika kwa sababu zimeshakuwa ni sheria za muungano, Kwa maana hiyo kuwemo katika kitabu cha sheria za Zanzibar kitu ambacho kinataka kufanywa unaweza kufanya sheria ili kuifuta ile na kuiondoa ile katika *low books* zako na hilo ndilo ambalo tunataka kufanya. *(Makofi)*

Lakini mimi nasema Mhe. Spika, kuna umuhimu wa kutengeneza sheria mpya ambayo italingana na matakwa ya siku hizi, italingana na hayo mambo ambayo yamekuwa na wawakilishi wetu ili sheria ile iwe kweli ya *maiming* ambayo inahusiana na Zanzibar, na katika sheria hiyo ndio tunaweza kuweka mambo mengi tu. Kwa mfano sheria ya kukodisha maeneo yale, sheria ya umilikaji au taratibu za umilikaji au taratibu za kukodisha kwa hivyo huo ndio utaratibu ulivyo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi kwamba hili suala bado ni suala la Zanzibar na suala ambalo limeshaamuliwa na Baraza lako tukufu la Wawakilishi, ni suala ambalo kamwe hata siku moja sio mimi wala sio Mwanasheria Mkuu mliotupa jukumu hilo kwamba tutarejea nyuma na kusema kwamba suala hili ni la muungano, hatutofanya hivyo hata siku moja. Hivi sasa tumo katika matayarisho ya namna gani tuweze kulipapatua zaidi suala hili kwa maslahi ya Zanzibar na kwa maslahi ya vizazi vyetu.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hilo pamoja na mambo mengi ambayo ameyazungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu napenda waheshimiwa wawakilishi wajue kwamba suala hili tunalo na tunalishghulikia kwa maslahi ya Zanzibar na katu hatutosema kama suala hili ama lizungumzwe ama liwemo katika orodha ya muungano au lisiwemo, ni suala limeshazungumzwa limeshaamuliwa kwamba hili sasa sio suala la muungano.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na mimi napenda nimshukuru Mhe. Waziri na labda niseme moja kwa niaba ya jimbo langu la Mgogoni, Mhe. Spika, jimbo langu la Mgogoni lina vijiji vitatu vinaitwa Kwale Kongo, Kinazini na Selem, vijiji hivi ni watoto yatima maana yake Kinazini kiko kati kati mkono wa kulia kuna kijiji cha mkono wa kulia kina umeme cha mkono wa kushoto kina umem lakini kile bahati mbaya. Kwale Gongo kijiji cha Mkono wa kulia kina maji, cha mkono wa kushoto kina maji lakini kile hakina maji na Selem ndio hivyo hivyo, ka hivyo namuomba Mhe. Waziri kwamba na vijiji hivi wavione ili angalau waongezee kuvuta umeme ama kutoka mkono wa kulia kufika kijiji hiki au vyenginevyo, *other wise* hivi vijiji vimekuwa *isolated* kabisa katika masuala haya ya maji na umeme. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba sana na vijiji hivi uvione katika bajeti.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda tena nimshukuru Mhe. Waziri napenda niwaombe waheshimiwa Wawakilishi kwamba suala hili tunalishghulikia kwa nguvu zetu zote, kwamba mafuta ni ya Zanzibar na hata siku moja hayatokwenda pahala popote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mungu wa utukufu na rehema kwa kutujaalia sote kufika hapa tukiwa wazima na siha, pili nikushukuru na wewe kunipa fursa hii na mimi kusema machache sana katika hotuba hii ya Mhe. Ali Juma Shamhuna Waziri wa Ardhi, Makaazi Maji na Nishati na Muwakilishi wa Jimbo la Donge.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria sikuona mimi haja ya kueleza ziada ya yoyote naamini wamefanya kazi nzuri sana na waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu watakuwa wamewafahamu vizuri, pia nina hotu yangu mimi yatakuwa yale ya kutomeza yale ninahofia kuja kuharibu utamu wa maneno ya viongozi wangu hawa wasomi.

Mhe. Spika, lakini kabla sijasema hayo machache naomba pia uniruhusu hasa kwa vile baraza lako liko kwenye jimbo la Kiembesamaki nichukue fursa hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki kwa kunichagua tena kwa mara nyengine kuwa Muwakilishi wao, ishaalla Mwenyezi Mungu atatujaalia uwezo wa kuweza kusimama nao na kuwatendea haki na kutimiza wajibu wetu kwa Chama cha Mapinduzi na hawa waliotuchagua.
Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya yeye na watendaji wake, mimi nina matumaini makubwa na vijana hawa wanaomsaidia bahati nzuri nimefanya kazi nao kwa miaka kumi na tunakotoka sipo tulipo leo naamini kwamba masuala ya maji, umeme usimamizi na utawala wa ardhi wataweza kuyasimamia ipasavyo na nchi yetu itapiga hatua kwa manufaa ya watu wake.

Mhe. Spika, langu ni moja tu ambalo nataka kulizungumzia ni suala la mafuta na gesi lakini kabla sijasema yale ambayo nataka kuyasema nirejee kulizungumza, maana haya tulizungumza kwenye jengo lile la Kikwajuni Mhe. Spika, jengo hili sijasema hasa suala hili na tunaambiwa kwamba siku ya kiama kila kitu kitasema mpaka makuta yataulizwa, nataka nirejee kauli yangu kwamba msimamo wangu mimi juu ya suala hili ni sawa na wengine wote humu ndani sijakubali kule, sikubali leo sikubali keshokutwa abadan masuala ya mafura na gesi asilia kuwa ya muungano hata kidogo. Ni dhambi hasa tukikubali hili ni dhambi ninaamini kule, ninaamini leo na mpaka kufa kwangu nitaamini hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wewe unaona mbali Mhe. Pandu Ameir Kificho anaona mbalii kwa maana kipindi chote cha mitihani ile ulikuwa Spika wetu na uliona mpira ulivyokuwa unachezwa mle ndani, ndio maana kwa kuona mbali kwako huku kwa upeo huo bado uko hapo, kwa maana wajumbe wako hawa na wengine sisi vijana wako tuna imani kubwa na busara zako. Nina sababu zangu za kusema hayo haikikuwa kipindi chepesi hata kidogo kilikuwa kipindi kigumu sana katika historia ya nchi yetu na historia ya baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar, hapo naungana na maneno aliyosema Mwanasheria Mkuu kwamba dhamira yetu ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar dhamira ya wawakilishi wananchi sio ya kutiliwa shaka hata kidogo.

Mhe. Spika, panya anatafuna waya hapa inaonyesha kilikuwa kipindi kigumu sana na ingekuwa hatujakabiliana na lile kwa umoja wetu wengine pengine tungekuwa hatupo hapa, kwa hivyo nirejee  kwa kusema na bahati nzuri nimeletewa Hansard yangu ya maneno yale niliyosema sitaki kuyarejea kwa sababu yaliudhi sana, kuna mengine makali kidogo humu. Lakini niseme kwamba nathibitisha tena kwamba haya nakubaliana nayo nimeyasama na nitaendelea kuyasema, lakini kabla sijaendelea jana Ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu  alisema hapa na akauliza je Zanzibar tumeolewa, katika hii ndoa ya Muungano hii kauliza sisi wake au waume.

Mhe. Spika, na wengine baadae sio kwenye kikao chako lakini baadae tukawa tunaulizana hii ndoa au ndoana, ndoa kwa wanadamu wenye fahamu lazima iwe na mafahamiano, lakini ndoana likishakukaa ndio lishakukaa, mimi ni mvuvi kwa upande mmoja huko kwetu Malindi huyu bwana ndio muwakilishi wangu mimi Mhe. Ismail Jussa Ladhu na kule wana nyimbo wanaimba wavuvi wanasema.
*"Ni mvuvi mashuhuri kila bandari avua, navua makarambisi na jodari la kupasua".*

Sasa Mhe. Spika, jodari la kupasua unafaa kula wewe maana yake ndio chakula cha Spika hicho, jodari la kupasuliwa lile lakini sasa jodari ndoana ikishakumkaa anakuja juu, ninaweza kufahamu hisia hizi za wawakilishi zinatokana kwa kwamba sasa lile dowana limeshakaa, kuna kazi kubwa sasa hivi ya kupapatua dowana lile. Mhe. Mwenasheria Mkuu amezungumza hapa lakini yeye kazungumza kwa lugha za uanasheria mkuu, mimi nazungumza katika lugha za ukwezi na ukulima za kimapinduzi mapinduzi kwa maana mimi sio msomi. Marehemu Mzee Karume Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema akisema tumejifunza tumetambua ndio kina sisi sasa dowana limeshatukaa Mhe. Spika.

Lakini nataka tukumbushane makubaliano yetu dhamira yetu kwa pamoja mwaka 2009 kuendelea juu ya suala hili kulikuwa na mambo ya msingi mawili makuu, moja kulitoa lile dowana lililotukaa hapa kwa maana kutoa masuala ya mafuta na gesi asilia kutoka kwenye orodha ya mambo ya Muungano ndio yalikuwa makubaliano yetu na dhamira yetu kuyatoa, narejea tena hili neno kuyatoa, lakini kuna la pili pamoja na mengine madogo madogo la pili lilikuwa kama alivyosema Mwanasheria Mkuu kuwa na utaratibu wa ndani utakaoturidhisha juu ya utekelezaji salama na maslahi kwa wananchi wa Zanzibar niwakumbushe maana yake.

Tulisema dunia kote huko kuna migogoro mingi wajanja wengi Mwenyezi Mungu amewapa neema hii tumelizungumza kwa sana kipindi kile lakini hawafaidiki nayo watu, kwa maana kutokana na umuhimu wa nishati hii kila

mtu anaitaka wakubwa wanaitaka, wajanja wanaitaka kama hamko tayari hamjajiandaa mtamalizika. Mtaanza kumalizana wenyewe kwa wenyewe halafu mtamalizwa na wengine sasa haya ni mambo mawili ya msingi. Sasa kwa migingi hiyo hiyo tukaleta sera ya taifa juu ya nishati katika baraza lako tukufu ambayo imeweka misingi mizuri sana katika utawala wa suala la mafuta ikiwemo baraza hili tukufu kuthibitisha mikataba yote ya utafiti na uchimbaji. Maana yake ni kwamba marufuku kwa serikali kuingia mkataba wa utafiti au uchimbaji bila ya ridhaa ya Wazanzibari wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, natoa mfano wa Norway na Kanada Mhe. Mwanasheria Mkuu Norway ukifungua mtandao basi ile mikataba iko kwenye mtandao kwa maana hawana la kuficha na ndio maana wako salama na wanafaidika, lakini tukiwa na hofu katika nchi zetu za kiafrika tukifanya mambo haya kinyemela nyemela na kwa haraka tutaumizana. Kwa hivyo hilo lilikuwa jambo moja la msingi sana.

Sasa Mhe. Spika, mtizamo wangu mimi naona kumlazimisha Mhe. Waziri kuja na tamko la kuleta sheria hapa ni kinyume ya makubaliano yetu hawezi kuleta sheria Mhe. Waziri hapa sio rahisi kwa misingi ipi, kwa sababu kwanza tulitoe ndivyo tulivyokubaliana baada ya hapo hatua nyengine hizi ndio zifuate hata akileta sheria leo kampuni ya maana yoyote duniani haiwezi kuja Zanzibar kwa sababu sheria yako haina mshiko, wewe huna mamlaka ya mipaka huna mamlaka ya utaifa atakuja nani. Tukitaka watamiminika majambazi sisi wenyewe tutakimbia hapa kampuni zisizokuwa na maana na hivi sasa wanakuja watudanganye tugombane na tumalizane wenyewe, kule Tundaua kule mafuta nayavyokuja wenyewe juu wataanza kumalizwa wale kwanza.

Kwa hivyo mimi nilitaka nikumbushe hayo Mhe. Spika, nikiendelea zaidi niungane na Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri wa katiba na Sheria kwamba dhamira ya serikali, dhamira ya Baraza la Wawakilishi haya sio ya kuzungumza tena Zanzibar imeshaamua kwamba masuali ya mafuta na gesi asilia sio masuala ya muungano tena hatutaki kusikiliza jengine hili sio la kuzungumza, ni sisi sasa kukubaliana utaaratibu wa kulitoa lile dowana kule na kuanza utaratibu wa nadani utakaoturidhisha. Utakaotupa mielekeo thabiti na usalama tuendelee na shughuli hii.

Mhe. Spika, hayo anayosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu bungeni kule wanazungumza kwamba mafuta haya hayawezi kuwa ya Zanzibar kwa sababu yapo mpakani tena wanaozungumza hivyo ni watu wazima tumeshawahi kujadili kwenye baraza hili, mimi sitaki kuwataja kwa majina tu. Lakini niseme nawaonea huruma tu washaishiwa, lakini hawa ni wale wenye fikra za miaka hiyo ya kuitisha tisha Zanzibar hii, kwamba wanaona kasimama bwana

mkubwa watu wanaanza kutetemeka huku hayo yamepitwa na wakati anayeogopa huku nani tena.

Kama wana akili akifungua macho na kulitizama Baraza hili wa kutetemeka ni wao kwa sababu mambo yale sasa hivi huku hakuna mtu anayesikiliza tena, lakini niwaambie tu yale ni maneno ya kuptosha ziko sheria za umoja wa kimataifa zinazosimamia utaratibu wa uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwenye nchi zilizokuwa na mipaka ya ardhi, mipaka ya bajari bahari ya ndani mpaka bahari kuu tena sheria hizo sio za leo wala jana ni za miaka mingi sana. Zimefafanua kwa undani vipi nchi zinaweza kuendesha biashara ya utafutaji na uchimbaji mafuta ndani ya nchi zao na kwenye mipaka, hasa kwenye mipaka ya bahari. Nilitaka kulisema hilo kwamba hilo halina mantiki tena.

Mhe. Spika, la mwisho jamani wakati tunalizungumza hili Baraza lililopita tulishikilia kutoa suala hili kwa utaratibu ambao ulikuwa umeshazoeleka kwa watu kukaa kuzungumza, kupelekeana mabarua ambayo maisha hayapati majibu. Lakini Mwenyezi Mungu ametuletea utaratibu sasa wa marekebisho ya Katiba.

Mhe. Spika, mimi nilidhani baada ya kulizungumza suala hili kwa kina ndani ya Baraza lako yengetoka mawazo na fikra kutoka kwa wawakilishi wananchi ya namna tutakavyoweza kuwaandaa Wazanzibari. Mwanasheria Mkuu ametwambia hapa kwamba marekebisho ya Katiba maana yake kwa sisi Wazanzibari ni kujadili upyama *articles of the union* yale makubaliano yetu ya mfumo pamoja na yale ya msingi.

Mhe. Spika, mimi nahofia kwamba isijeikawa kama tunalivyokuwa tunakwenda kuwaelimisha wananchi juu ya suala la Serikali ya Ummoja wa Kitaifa. Hapa kila mmoja tulikuwa tunafurahishana tukitoka mlangoni kila mmoja anakwenda na lake. Ikawababisha wananchi lakini kwa rehma ya Mwenyezi Mungu nay ale waliyoyataka Wazanzibari leo tuna Serikali ya Ummoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, ni lazima tuseme ukweli wengi tuliwakoroga wananchi wetu na tumebaki sasa tunajutia. Sasa badala ya kupoteza muda tunataka kumlazimisha Mhe. Ali Juma Shamuhuna kufanya jambo ambalo hana mamlaka nalo, wala haimo katika makubaliano yetu tutokea tukawaelimishe na kuwaandaa Wazanzibari namna watakavyoweza kujadili na kuzungumza upya makubaliano ya muungano na mfumo wenyewe. Waungwana kama mnaogopa mimi ndio nimeshalianza hilo. (*Makofi*).

Hapa mpango wa serikali moja hatutaki kulisikia. Mfumo huu butu wa serikali mbili sasa basi. Twende kwa jambo ambalo kila mmoja wetu analizungumza la

serikali tatu na mengineyo. Sasa baada ya kukaa tukawa tunatafunana, tunalana nyama wenyewe kwa wenyewe humu ndani, tunalana roho jamani tutoke tukafanye ya msingi. Wazanzibari wanataka kuandaliwa, waweze kukabiliana na hili jambo. Tutakuja kupigwa magoli ya kisigino. Jamani nakuombeni sana.

Mhe. Spika, nimalizie maana haya mambo mengine tukiyaanza ndio yale niliyokuwa naogopa ya kutomeza. Tumuache Mhe. Shamuhuna afanye wajibu wake ya kuyasema hapa Mawaziri wameshayasema. Ana kazi kubwa sana, aje ajumuishe hapa, tumpitishie vifungu vyake kwa salama. Wajibu wa serikali utasimamiwa na Mwanasheria Mkuu. Serikali hii ni ya Umoja wa Kitaifa na sote tunakumbuka Mhe. Hamadi Masoud msimamo wake. Mhe. Saidi Ali Mbarouk msimamo wake. Mhe. Abubakar msimamo wake. Hatari tupu, sasa hilo litapitaje kule Baraza la Mapinduzi, halikupita wakati ule litapita leo.

Sasa tumpe ruhusa Mhe. Shamuhuna, tubariki bajeti yake, tutoke tukafanye wajibu wetu. Wananchi wana matumaini makubwa kwa serikali yao hii. Wananchi wanataka kuona wawakilishi waliomakini, wanawaongoza. Tuende huko tukafanye wajibu wetu, kuwaelimisha wananchi majimboni kwetu juu ya nini maana ya muungano na utaratibu wa leo. Wapi twendapo nini cha kufanya ili sasa haya mnayoyataka humu ndani muweze kuyaamua nyinyi wenyewe.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja mia fil mia. Nakushukuru.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wangu. Spika akisema watu hunyamaza kimiya. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri ambao wametoa ufafanuzi mzuri si tu kwa niaba ya serikali lakini kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa muda wote mmekuwa wasikivu, mmekaa mmetulia. Nawashukuru leo kwamba mmo ndani mnasikiliza maelezo yanayotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wenzetu ambao ni wa ngazi ya mawaziri pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Umoja huu mwenendo huu utatusaidia sana katika kufikia maamuzi mazuri ya mambo yetu mengi. Hata yaliyokuwa magumu yanaweza kuwa ni mepesi sana. Nimkaribishe sasa Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati, karibu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe sikuelewa kama zana kumbe zipo nyingi sana angenambia mapema ningempatia msaidizi akamletea hapa. Mhe. Waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Nina hakika kwamba utakubaliana na mimi kwamba makofi haya yana ishara nzuri na Ishallah iwe hivyo. Lakini pia watu wanne waliomalizia hotuba zao sasa hivi alianza Mhe. Haji Faki Shaali, akaja Mhe. Mwanasheria Mkuu akaja Mhe. Waziri wa Katiba na sheria akamalizia katika wale watu wanne akamaliza Mhe. Mansour Yussuf Himid.

Mhe. Spika, kama ingekuwa si utaratibu wa kujibu hoja zilizotolewa nafikiri Mheshimiwa ungeniruhusu nikakae kitako. Nina hakika waliyoyazungumza watu wanne hawa sitaweza kuyazungumza vizuri kama zaidi ya hivyo walivyoyazungumza. Lakini kwa sababu natarajiwa nifanye hivyo basi nitafanya.

Kwanza nawashukuru sana sana na nadhani wananisikiliza *and the better listen me good* kwa lugha ya Kimarekani, wanisikilize vizuri ninayoyasema kwa niaba yao. Hao sio wengine ila ni wananchi wa jimbo la Donge. Wananipa *support* kubwa sana tokea kuanza mijadala hii, haijapata kutokea. Hii ni kwa sababu kama wengi walivyosema kwamba hii Wizara ni ngumu ni nzito na mimi nakubali. Lakini kwa niaba ya wajumbe nyote mliokuwepo hapa mkinisaidia hii Wizara naiweza na kwa uzito wake si dhani kama kuna mtu atapenda asinisaidie ili niiweze.

Mhe. Spika, nilikula kiapo wakati natawazwa kuwa Mwakilishi rasmi baada ya kupata kura nyingi katika jimbo langu na katika kiapo nilichokula nilisema kama alivyosema swahibu wangu leo ndugu Ali Mzee kwamba atalinda Katiba ya Jamhuri na Katiba ya Zanzibar. Na mimi nitafanya juhudi hiyo kwa sababu nilikula kiapo na sitokwenda kinyume na kiapo changu. Nitalinda Katiba ya Jamhuri na nitailinda Katiba ya Zanzibar. Kwa manufaa ya nchi zetu mbili Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar.

Nimesema Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu Jamuhuri hii ina nchi mbili na kama kiapo chetu kipya kinavyozungumza nchi mbili ziliungana na sasa kuwa Jamuhuri moja ya Muungano wa Tanzania. Sote tunajua na hili tumelizungumza sana kwamba Katiba zetu zote mbili zina migongano. Nataka nimkumbushe Mhe. Hamza Hassan Juma katika kipindi alichokuwa Waziri alijitahidi sana kushirikiana na Mhe. Mohammed Seif Khatib, kujaribu kuyaondosha migogoro ya Muungano.

Nilikuwa nikimwambia kwamba Mheshimiwa utajitahidi, utakuwepo, utaondoka, huyamalizi. Atakuja mwengine hayamaliziki kwa sababu wenzetu hawataki kuyaondosha. Lakini kama wenzetu wangekuwa na nia safi ya kuyaondosha matatizo ya muungano yangekuwa yameshaondoka. Mwenyezi Mungu ameleta neema yake tulikuwa tuna migogoro hapa ya CUF na CCM,

tulikuwa tuna migogoro hapa ya Serikali na Upinzani. Mwenyezi Mungu ameleta neema yake migogoro hii imeondoka.

Leo Mhe. Haji Faki Shaali, ameuzungumza sana wasifu wangu, miaka miwili iliyopita asingeweza kufanya hivi hata siku moja. Na angafanya hivi angejikuta anafukuzwa katika chama chake cha CUF. Mhe. Abubakar Khamis Bakary, kwanza hii nafasi aliyokuwa nayo asingekuwa nayo. Alikuwepo muda mrefu hapa mbona hakupewa hii nafasi ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, kapewa kwa kuja Sheria ya Ummoja wa Kitaifa. Amezungumza kwa umakini sana, nasema ombi lako limekubaliwa, tukitoka hapa tunakwenda Mgogoni na wenzangu kule juu wananisikia. Ili kuimarisha umoja wetu wa kitaifa.

Nilisema Katiba yetu ina mgogoro na moja katika mgogoro wa Katiba yetu ni suala la mafuta. Tumelizungumza sote hapa. Nisengeweza kusema vizuri zaidi kama alivyosema Mwanasheria Mkuu. Kama tulivyokubaliana sisi wenyewe tuliokuwepo katika Baraza la Wawakilishi lililopita. Nasema tusishindane kwa ukereketwa mmoja akawa mkereketwa sana na mwengine akamuona mwenzake msaliti. Sote wakereketwa na hasa sasa hivi tumezidi kuwa sote wakereketwa kwa sababu tupo katika Jumuia. ya Umoja wa *System* zetu za kisiasa. Tukitoka hapa kila mmoja akenda kwake anazungumza yake, lakini tukifika hapa na kwengineko kama hapa tunazungumza kauli moja.

Nataka nimnukuu Mhe. Waziri Kiongozi mstaafu. Alisema wakati anafunga mjadala huu tunaouzungumza sasa hivi alisema kama hivi:

> "Kwani miongoni mwetu nani kapewa turufu ya kumwambia mwenziwe wewe mkereketwa na mimi mkereketwa zaidi, wewe si mkereketwa, sote ni wakereketwa".

Alisema na mimi narudia sote ni wakereketwa katika jambo hili. Napenda kuahidi na kuahidi. kutokana na *reference* aliyonifanyia Mhe. Haji Faki Shaali. Katu sitorudi nyuma katika kulitekeleza suala la mafuta kama tulivyoamua katika Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Spika, suala la mafuta tumelizungumza. Samahani niruhusu nilianze hili kwanza kwa sababu hili ndio zito suala la mafuta, mengine yatakuja baadaye. Tulilizungumza suala la mafuta hapa tokea juzi kwa aina tatu tofauti.

- Tulilizungumza kwa mantiki ya kisiasa.
- Tukalizungumza kwa mantiki ya kiuchumi.
- Tukalizungumza kwa mantiki ya kisheria.

Mhe. Spika, Wallahi kisiasa *message sent,* nakupongezeni sana hakuna hata mmoja aliyechangia asitaje suala la mafuta tulitoe katika orodha ya muungano. Kama mlikuwa mnajua lengo lenu ni kuipeleka *message* Tanzania Bara kwamba suala hili litolewe tumeshafaulu. Tumeiyandika historia ya Malesia na Singapour na Ishallah wenzetu kule wanune, waseme bwana eeh! Wapeni mafuta yao kila siku zogo tu. Ndivyo Malesia walivyowaambia Singapour eeh! Bwana wapeni nchi yao hawa wadogo sana kila siku zogo tu, tunataka mishahara tunakata nini, wapeni nchi yao waendeshe.

Leo Singapour *three times much better* kwenye uchumi kuliko Malesia. Na hawa kama message wameipata mimi naomba dua Ishallah wanune na wakinuna watupe Zanzibar yetu na mafuta yetu. Kiuchumi nataasaf kusema hatukuliona mbali tumelizungumza tu mafuta yatatusaidia katika uchumi lakini tumeyasahau yale tuliyoyaamua. Tumesahau yale tuliyoyaamua tutafanya nini ili tulitoe, tukishakulitoa sasa litatusaidia katika uchumi.

Mhe. Spika, tukija kwenye upande wa Kisheria tandika ulale. Wanasheria wamezungumza vizuri sana leo. Ndio faida ya kuwa na wanasheria, sio tu wasomi lakini ni wanasheria wenye *experience* ya kutosha. Huo ulikuwa ni utangulizi wangu. Sasa narudi katika hoja.

Mhe. Spika, hotuba yangu imeshangiwa na watu 32 kwa kujadili na watu 12 kwa kuandika. Nakushukuruni sana mliobahatika kuandika na kuchangia na wale waliokuwa hawakubahatika najua walikuwa na shauku kubwa sana ya kuchangia. Michago yao isingekuwa tofauti ingeingia humu humu. Nasema mmewakilisha vizuri. Napenda niwataje waliochangia.

1. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano

2. Omar Ali Shehe
3. Mhe. Hamza Hassan Juma
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Ussi Jecha Simai
6. Mhe. Abdullah Juma Abdullah
7. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
8. Mhe. Fatma Mbarouk Said
9. Mhe. Mgeni Hassan Juma
10. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
11. Mhe. Salum Abdullah Hamaad
12. Mhe. Rufai Said Rufai
13. Mhe. Mussa Ali Hassan
14. Mhe. Assa Othaman Said

15. Mhe. Ali Salum Haji
16. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
17. Mhe. Hija Hassan Hija
18. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
19. Mhe. Hassan Hamad Omar
20. Mhe. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma
21. Mhe. Panya Ali Abdullah
22. Mhe. Moh’d Haji Khalid
23. Mhe. Kazija Khamis Kona
24. Mhe. Ali Abdullah Ali
25. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
26. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
27. Mhe. Rashid Seif Suleiman
28. Mhe. Abdullha Moh”d Ali
29. Mhe. Mwanasheria Mkuu
30. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria
31. Mhe. Haji Faki Shaali (MBM)
32. Mhe. Naibu Waziri WAMMN na
33. Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili.

Waliochangia kwa maandishi ni 12 nao ni:

1. Mhe. Thuwaibah Eddington Kisasi
2. Mhe. Makame Yussuf Hamad
3. Mhe. Farida Amour Mohamed
4. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
5. Mhe. Nasoor Hemed Madhrui
6. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
7. Mhe. Mohammed Said Mohammed
8. Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi
9. Mhe. Mtumwa Kheri Mbarouk
10. Mhe. Shadiya Mohammed Suleiman
11. Mhe. Salma Mohammed Ali
12. Mhe. Shawana Hassan Bukheti

Nakushukuruni tena sana kwa michango yenu na kama kuna mtu nimemkosea jina lake naomba anisamehe sana.

Mheshimiwa sasa narudi kwenye hoja na nimesema nitaanza na hoja ya mafuta kwa sababu hii ni nzito na ni ngumu. Lakini sasa imekuwa nyepesi na imekuwa laini kutokana na michango iliyotangulia.

Suala la mafuta, Mhe. Mwanasheria Mkuu alilizungumza vizuri alisema kwamba hili lilikuwa hakuna haja yakuchangiwa. Hili limekwisha changiwa na limeshamalizika. Kilichobakia sasa sisi tukae pamoja tushirikiane, tuelimishane ili tunapokwenda katika kujadili masuala ya muungano hiyo itakuwa ni nafasi nzuri. Akasisitiza hakuna haya ya kufanya papara.

Mhe. Waziri Mhe. Abubakari Khamis Bakari karejea hayo hayo, Mhe. Mansour kayazungumza hayo hayo tena kwa hamasa kubwa sana kwa sababu yeye ni kijana. Akatukumbusha maamuzi yetu akasema kwamba tuliamua hili suala tulitoe katika orodha ya Muungano na hivyo ndivyo ninavyokumbuka. Nimezipitia Hansard volume tatu na yote yaliyozungumzwa nimeyasoma na nimeyafahamu. Hata yale maazimia matatu la kwanza na la pili na la tatu. Nimeyafahamu.

Azimio la tatu lilikuwa lina mgogoro kidogo lakini baadaye Mhe. Spika, kwa utaalamu wake akalisawazisha, tukapita kura sote kuliunga mkono nalo lilikuwa la Bahari Kuu..

Mhe. Spika, tulitofautiana kidogo tulisema bahari kuu kwa sababu jambo la Muungano hili tushirikiane, lakini Mhe. Abubakar Khamis Bakary akasema bahari kuu iko Mashariki ya kisiwa chetu. Kwa hivyo, mpaka wake unamalizikia kwenye ***nautical** miles* 200 kati kati hapa hakuna mpaka kwa hivyo hili ni letu. Mhe. Spika, wengine wakachangia wakaunga mkono kwa hivyo hata hilo baadae Mhe. Spika, akalizungumza na sote tukaliunga mkono na katika hansard orodha imeandikwa tuliopiga kura tulikuwa watu 42 na sote tumeliunga mkono hakuna hata mmoja aliyelipinga.

Mhe. Spika, ni kweli hii kazi ilikwisha, mimi kazi iliyobakia sasa hivi kutekeleza yale tuliyokuabaliana. Kwanza kulitoa katika Muungano hatujakubaliana kwamba tuunde sheria mpya jamani. Mhe. Spika, wakati umefika wakuzungumza mswada wa sheria ili wakati ukifika tuunde sheria mpya. Kwa hivyo, sasa hivi hatuwezi kuunda sheria mpya wakati kuna Katiba, nazungumza wataalamu wa sheria kwamba Katiba ndio sheria mama.

Mhe. Spika, kuna sheria mama ya masuala ya Muungano Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema suala hili ni la Muungano. Mhe. Spika, sisi sote tumekubaliana kwamba tulitowe mimi nitalisimamia kwa nguvu zangu zote mpaka tulitowe suala hili. Mhe. Spika, hapa chakufanya sasa hivi tuweke misimamo wakati wakwenda kuzungumza mabadiliko ya Katiba hii iwe ndio ajenda yetu namba moja. Tunasema wasi wasi wetu kwetu hatutopata ile *two third majority* tunayoitaka ndio nilivyozungumza hivyo, kuna watu

wanazungumza pembeni pembeni na wengine wamezungumza hadharani hapa kwamba basi hatuwezi kupata two third wana nini basi tulitowe sisi wenyewe ili tuunde sheria yetu wenyewe.

Mhe. Spika, mimi sina pingamizi kama tukifanya hivyo na tukifanikiwa na bila ya matatizo mimi naunga mkono, lakini kwa ushauri uliotolewa na wanasheria wetu hapa leo ni mchimbaji gaji atakayekuja kuchimba mafuta na kuna migogoro kama hii ya kisheria na ya kikatiba katika nchi moja, hakuna labda chapa punga, kama kuna kampuni ya kichapa punga wanaweza wakaja na wallahi watapiga mapeto. Nasema *draft* ya sheria nimeiona ninayo tumeshaipitia mara mbili na bado tunasema hatujatosheka hatujatosheka tunatafuta ushauri wa watu wengine. *Caltax* katushauri si ndio tunasema ndio mkubwa huyo, *Taff gas* ametushauri, *Antrim* ametushauri hao ndio watu watatu tunaowaangalia kwa macho mawili kudhani wanaweza wakatusaidie kuchimba mafuta.

Mhe. Spika, mimi nasema wenzangu wamesahau nataka nizungumze suala la *Antrim* na suala la *TPDC.* Mhe. Spika, tulikataa kule kwa kauli moja kwamba suala la mafuta yetu tusiwashirikishe *TPDC*, tusitumie sheria ya *TPDC* kwa sababu inatubana. Leo tumezungumza hapa jana madhali *TPDC* wana pesa zetu basi tuchukue tukasomeshe watoto wetu. Mhe. Spika, ndio ule usemi unaosema “nguruwe haramu lakini mchuzi wake tunaunywa”, “baniani mbaya lakini kiatu chake ni dawa”. Kama tumeamua *TPDC* tusiwashirikishe katika mambo yetu ya mafuta basi mimi nitasimama kwa msimamo huo mpaka mtakaponipa kauli nyengine.

Mhe. Spika, Antrim mwaka 1996 walikuja timu nzima *Antrim* na *TPDC* kuja kuonana na Rais, wakati ule alikuwa ni Mhe. Salmin Amour Juma mimi nilikuwa Waziri wake wa Mipango na Vitega Uchumi. Kwa hivyo, sasa mafuta utaweza kuyaita vitega uchumi, utaweza kuita mipango kwa hivyo mimi nikaalikwa kwenye mkutano ule nilikuwepo nikashuhudia. Mhe. Spika, wakati ule Canada wametugomea miongoni mwa nchi nyingi zilizotugomea kutusaidia. Dk. Salmin Amour Juma akawaambia *TPDC* msiniletee watu wa Canada hapa kwa sababu wao wametugomea kutusaidia, akasimama mmoja akasema kama kawaida yao, mheshimiwa tunazungumza masuala ya *investment* usiyachanganye masuala haya na siasa.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Amour alinyanyuka akamwambia nenda zako na nyinyi nyote nendezenu watu wangu nyinyi bakieni. Mhe. Spika, wale wakafukuzwa na kutoka pale sisi tukakataa kushirikiana nao hawa watu wa *TPDC* kwa sababu wanatubana. Leo vipi tunazungumza tuchukue pesa zao tukasomeshe watoto wetu, tunazungumza mbona ripoti zetu hawatuletei. Kwa hivyo, mimi nasema tuwaachie wenyewe hayo tulizungumza tuachane sasa

vya kusema kama tunasema mafuta na gesi asilia ni suala la Muungano basi almasi na madini zote ziwe na Muungano. Mhe. Spika, baadae tukafika pahala tukasema tuache kusema suala hilo, hawa hawana almasi, hawana gesi wala hawana chochote hawa kwa sababu vitu vyao vyote vinaibiwa. Mhe. Spika, sisi katika matakwa yetu ni mafuta yetu na gesi asilia.

Kwa hivyo, msimamo uliopitishwa ni huo kwamba tusizungumze na *TPDC* katika suala zima la kutuchimbia mafuta na tusizungumze na *TPDC* katika suala lote la kisheria na kadhalika. Mhe. Spika, sasa Baraza hili kupitia kwa Mhe. Rais maana yeye ni sehemu ya Baraza kama tutapa maelekezo sasa twende huko mimi waziri wenu nitatekeleza kazi hiyo, lakini kwa sasa msimamo wangu hakuna TPDC, hakuna Antrim hakuna chochote. Tunataka mafuta yetu tuyamiliki sisi wenyewe huo ndio msimamo.

Mhe. Spika, lakini mimi ni waziri kuna watu walizungumza mbona umepata rasilimu hii umekaa nayo muda mrefu hivi kuna siri gani, unafanya nini wengine walikuwa wakali sana. Mimi ni waziri nina wakubwa zangu hawa watatu kuna mambo nitayaamua kwa sababu nimeelekezwa na katiba pamoja na sheria, lakini kuna mambo lazima ni-*seek consultation,* na nitakachozungumza na wakubwa wangu si lazima nikizungumze hapa ndio utaratibu. Nasema sheria ile bado ina mapungufu mengi kitaalamu na bado tunatafuta watu watusaidie kitaalamu ili wakati ukifika kwanza tutaipeleka kwa Makatibu Wakuu ile suala la kwamba tuletee kesho sheria hii iliyozungumza jana halipo.

Mhe. Spika, kwanza tuipeleke kwa Makatibu Wakuu ikitoka huko iende kwa mwenyewe Mhe. Rais *with or without changing* Baraza la Mapinduzi sote tuko hapa tutaizungumza ikishe tutaileta hapa tutaiogelea halafu tutamrejeshea mwenyewe Mhe. Rais aweke mkono wake. Kwa hivyo, sasa hivi sisi hatuna sheria tuna *draft* ya hiyo sheria ambayo tutataka kuipendekeza wakati ukifika.

Mhe. Spika, katika kutafuta utaalamu maana mimi sio mtaalamu wa mafuta Mhe. Haji Faki Shaali siku moja alinita mtaalamu wa ng’ombe, nikanuna nikenda nikasomea uchumi nikapata *first degree with flying colours* hivi sasa nimechanganya ng’ombe na uchumi. Lakini sio mtaalamu wa mafuta wala sio mtaalamu wa sheria, swahiba wangu Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi nampa mengi pale mimi sina hiyana. Siku moja nilimuuliza mbona wewe umesema ng’ombe huyu dume ni ng’ombe mzuri ataleta mbegu nzuri, nikamuuliza kwa kipimo kipi ulichokitumia.

Mhe. Spika, mimi nikamfahamisha vipi unampata ng’ombe dume ukampima kwamba huyu atatoa maziwa mengi, maana ng’ombe dume hatoi maziwa hivyo utampima vipi. Mhe. Spika, basi nikamuelimisha yeye akashangaa, akanambia

unajua wewe umenisaidia. Kwa hivyo, mimi kwenye ng'ombe niko na kwenye uchumi niko lakini kwenye mafuta siko. Kwa hivyo, mimi niliomba wataalamu mbali mbali wanipe taaluma ya mafuta kutoka siku ya kwanza unayachimba nijue utapita mikondo mingapi na utaanza lini kuyachimba.

Mhe. Spika, wakaniambia kama hivi ifuatavyo. Kwanza unafanya *arial survey* na *arial* survey itafanya kwa kutumia helkopta ni nzuri zaidi kuliko chengine na hawa tumewaruhusu tarehe 25 watazunguka na helkopta kwa muda wa masaa 4 Unguja na Pemba. Mhe. Spika, yale ambayo yako katika mamlaka yangu yakupata mafuta ninayaanza kuyafanyia kazi, mimi sijakaa tu.

Mhe. Spika, la pili ni kuwasilisha vifaa vya kufanyia utafiti, kazi hii itafanywa mwezi wa Agosti mwezi ujao. Kukusanya taarifa yaani *assessment data collection* itafanywa mwezi wa Septemba mwaka huu wa 2011, taarifa ya awali kukusanywa *asses bit data* itakamilika Disemba mwaka 2011. Mhe. Spika, Februari mwaka 2012 ni kuzi-*process* hizo taarifa zilizopatikana, April itakuwa ni kuzichambuwa hizo taarifa na hatimaye kuzi-*interpret*. Mwezi wa Oktoba, 2012 utafutaji wa mafuta ambao utachukua miezi minne kuyafanyia mapitio yakina itakuwa ni mwezi wa Februari mwaka 2013. Disemba ni kuandaa mpango wa maendeleo wa kuchimba mafuta pamoja na kuangalia mchango wake kiuchumi. Mhe. Spika, Septemba, 2014 kama *appraisal* inatwambia *economical viable* kuyachimba mafuta ndio tutachimba.

Mhe. Spika, wale walioniuliza hivyo Mhe. Shamuhuna wewe huna sururu huwezi kuyachimba mafuta hayo, sio sururu tu hata kwa mtaimbo siwezi kuyachimba. Mhe. Spika, alisema Mhe. Othman Masoud suala hili halitaki papara na wana malenga wanasema jambo zuri halitaki haraka. Mhe. Spika, tunaweza tuka-*rush* tukayapata mafuta kienyeji maana sio kwa mujibu wa sheria wala sio kwa mujibu wa katiba, tukayapata kienyeji. Mhe. Spika, watu wetu, wataalamu wetu, wachumi wetu bado hamjamaliza kusoma, itakuwa hatuna wataalamu wakuzungumza na hao watalaamu wachimbaji wa masuala haya. Mhe. Spika, itabidi tukakodi wataalamu wapi? Dar es Salaam au Kenya au Uganda.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tupeni muda tuaminini sisi wenzetu kwani hii kazi tunaifanya hatujalala, na kama kuna mtu anataka mafuta ya Zanzibar tuyachimbe mimi nafikiri nataka tokea juzi wala sio jana wala sio leo. Lakini twendeni kwa utaratibu wa kiutalaamu najua sote tunasema mafuta ndio ukombozi wetu, najua mnasema tumeukalia uchumi wetu najua mnasema hivyo na mimi ninakubali. Lakini ukiukalia uchumi ukiuacha uwive na inapofika tayari sasa hivi kuutumia basi utautumia vizuri kweli kweli na hapo ndipo utakapoiona raha ya uchumi wako. Mhe. Spika, chakula tunacho papara ya nini tutakuja chakula kibichi.

Mhe. Spika, nataka nimkariri Mwanasheria Mkuu alitwambia wale wanaosema kwamba Muungano wetu ni kama ndoa, moja akauliza katika ndo hii mume ni nani? Halikutoka jibu hapa. Mhe. Mwanasheria Mkuu tokea jana anatwambia na leo ametwambia tena kwamba huu Muungano wetu sio ndoa ni ndoana imetukaa hapa kwenye shavu kwa ndani. Mhe. Spika, kila unalolisema mkosa ni wewe, Mzanzibari ndio mkosa Mtanzania Bara sio mkosa, ukidai chako hupewi unaambiwa subiri wakati haujafika. Kwa hivyo, tukifanya ubabe kujikakamua tutakata mpaka na shavu na ndoana itatoka. Mhe. Spika, tuitowe ndoana pole pole na inshaallah itatoka.

Mhe. Spika, nataka nikupeni siri lakini hii sina hakika nayo lakini nitakupeni siri hii. Mhe. Spika, wenzetu wamefanya utafiti wa mafuta na gesi asilia mpaka leo wamevumbua gesi mafuta hawajayapata bado. Hivi sasa imeletwa meli yakutafuta bahari kuu na bahari kuu ni sehemu yetu tunatakiwa sasa hivi tujipange kwani hiyo meli iliyokwenda kuzinduliwa na Mhe. Pinda mpaka wake utafika wapi? Mhe. Spika, akiingia bahari kuu ni yetu shirika, je tumeshajitayarisha kwa hilo mbona tunapiga kelele kusakamana wenyewe kwa wenyewe tu, huyu nitakupa shilingi moja tu tisini na tisa ninazo nazuiya, huyu nitakupa hamsini na hamsini nazuia. Jamani katika hii taarifa ya vikao vya Baraza nimesoma mchango wa Mhe. Said Ali Mbarouk sijui kama mwenyewe anakumbuka.

Mhe. Spika, Mhe. Said alisema tusipokamatana tukenda kwa pamoja tukaelewana basi tutapoteza haki zetu. Mhe. Said alizungumza tena wakati ule yeye alikuwa ni mpinzani, lakini jinsi tulivyoiogelea suala hili tuliacha ile sera ya upinzani na sera ya serikali tukaliogelea kwa pamoja. Leo nashauri na naomba tukamatane kwa pamoja, tushirikiane ufafanuzi wa kisheria umeshatolewa mimi hatimae nitatoa ufafanuzi wa kiuchumi. Lakini tusipokamatana na tukawa kitu kimoja hivyo tunajipunguzia nguvu zetu, itafika wakati sasa tunakwenda kujadili suala la marekebisho ya katiba tunakwenda na tofauti zetu, na hapana shaka tofauti zipo hivi sasa hivi tofauti zipo miongoni mwetu. Mhe. Spika, wawakilishi wa CCM watazungumza ilani yao ya uchaguzi kwa sababu wana haki hiyo katika suala hilo, ilani inaelekeza vipi? Na wenzetu wa CUF watazungumza maelekezo yao yanazungumza nini.

Mhe. Spika, tusipoyaoanisha haya matatizo yetu na tofauti zetu hizi tulizonazo basi Serikali ya Umoja wa Kitaifa itakuwa ni kazi bure. Kwa hivyo, mimi nasema tujipe muda ili tuweze kukaa pamoja tuzioanishe kasoro zetu zote za upande huu na upande huu halafu tukae tuseme katika hili tunaacha hili na hili tunazungumza hapa. Kwa hivyo, tukifika kule *agenda* namba moja ni mafuta zitakazofuata ni nyengine lakini kwanza *agenda* namba moja ni mafuta. Mhe. Spika, tunazungumza mafuta mpaka tunakubaliana vyenginevyo tunaweka

mkutano hata mara sita au saba lakini tunazungumza na mafuta yatolewe katika Muungano mpaka tutakubaliana.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Juma Shamuhuna yuko leo Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kesho atakuja mwengine sio mimi Shamuhuna, alikuwepo Buruhani Saadati hapa akaondoka akaja Mhe. Mansour Yussuf Himid, alikuwepo Salim Hashim hapa akaondoka lakini bado mafuta, maji, majenzi na kadhali yako pale pale. Kwa hivyo, mimi nasema tuzungumzeni hoja na mijadala yetu tuielekeze katika hoja ni mafuta sawa, tunayafanya nini, tumekubaliana nini.

Mhe. Jussa ulikuwa kila wakati unanifuata na kuniuliza unayoyakusema ukaturidhisha, ndio haya nayasema yakuridhishe. Mhe. Spika, namwambie Mhe. Jussa arejeshe shilingi yangu kwenye bajeti. Pia na Mhe. Hija arejeshe shilingi yangu kwenye bajeti hii na wale wote walionipunguzia wairejeshe shilingi zangu katika bajeti munipe bajeti ili inipe nguvu nikafanye kazi.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri Wajumbe wamesikia kuhusu hilo sasa tuendelee na mengine.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, naomba nimalizie mchango wangu huu katika mafuta halafu ndio niende katika michango mengine. Naomba sana tuitizame Zanzibar yetu, tuutizame Uzanzibari na ikesha tuitizame nchi yetu tusiwasingizie waliotutuma, waliotupa kura wote walitaka tuwaletee maendeleo hawakutaka tuje tugombane kwenye Baraza hili. Maendeleo nyote mliyatafsiri kwamba mafuta ndio maendeleo, kuondosha umasikini ni mafuta na kadhali pia mafuta. Mhe. Spika, tukaifanya kazi hiyo nipeni bajeti yangu msininyanganye, mkininyanganya haitonisaidia mimi wala haitokusaidieni nyinyi. Hakuna waziri yeyote atakayekuja katika wizara hii kesho akakuleteeni rasimu ya sheria keshokutwa akakwambieni mkachimbe mafuta.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri makofi hayo Wajumbe wameshafahamu twende na hoja nyengine sasa.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, nakushukuru kwa hekima zako maana ungeniachia ningeendelea kudhani hawajafahamu. Nakwambia hata nimeacha kuangalia Mhe. Jussa anapiga makofi, kuashiria kwamba amefahamu, kwa hivyo nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba tena wale ambao walitaka maelezo yakina niwape ili waridhike nadhani sasa wameridhika.

Mhe. Spika, sasa naanza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye ni Mwenyekiti…

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri ikiwezekana wachukue kwa makundi.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, Mhe. Mshimba alizungumza zaidi kunipongeza mimi na kuipongeza wizara yangu, lakini kuna moja katika mchango wake binafsi alisema serikali inachukua hatua gani kuwa na vianzio vyengine vya umeme. Hilo nimelizungumza mara nyingi sana bado tuko katika utafiti, bado katika kuwaalika watu waje tuzungumze nao na tumeshazungumza na kampuni nne, umeme wa jua, umeme wa mawimbi ya bahari, umeme wa upepo wote hao tumeshazungumza nao na mwelekeo zaidi uko katika jua na upepo kuliko mawimbi ya bahari na kadhalika. Lakini bado tunazungumza kwa sababu sisi tunataka angalau tupate kilo walt 50. Kwa hivyo yeyote atakayeweza kilo walts 50 tutamfikiria. Mhe. Spika, lakini jengine la pili ni gharama za uzalishaji hivyo bado tuko katika mchakato huo na tunaomba mtupe muda.

Mhe. Spika, Mhe. Mshimba alizungumza suala la yule mfanyakazi wetu wa zamani lakini hili naomba sana Mhe. Mwenyekiti wangu ukubali suala hili tulipeleke kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa sababu hili suala lina matatizo ya kitaalamu, tukilipeleka huko tunaweza tukapata ufumbuzi.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe nadhani nimeshakujibu mahitaji yako ya mafuta, lakini suala lile la maji, nishati katika maeneo yake, tatizo nikisema nitakuja tuzungumze nikija Waheshimiwa Wawakilishi huwa siwaoni. Mhe. Spika, hili pia nalijibu la wale wawakilishi wengine waliozungumza mwakilishi mmoja alizungumza lile suala la Kusini Pemba, Mtambile kwamba hakuna maji. Mimi nawaahidi kila wale waliozungumza kwamba wana matatizo ya maji na umeme nikimaliza Baraza hili nitakwenda Pemba kabla ya Ramadhani kwenda kuyaangalia yale matatizo mimi pamoja na wataalamu wangu ili tutafute njia ya kuyamaliza. Hii sio Pemba tu lakini hata wale ndugu yangu Mhe. Mtando amezungumza kwamba ana matatizo ya maji katika jimbo lake, lakini taarifa niliyonayo kuna tatizo moja kwamba kisima kimeshawekwa na maji yanatoka labda mwenyewe huna habari. Kuhusu yale mengine tutakwenda pamoja kwenda kuyaangalia.

Mhe. Spika, kuna Waheshimiwa wengi sikuwaandika majina yao, lakini kuna waheshimiwa wengi walikuwa tatizo la bei kubwa ya umeme na wakashauri tuwape mikopo, tuwapunguzie bei. Lakini kuna waheshimiwa wengine walilaumu Shirika langu la Umeme wakasema tunajitahidi kulisaidia shirika lako, tuna nguzo zetu zimekaa muda mrefu sana lakini hazijatumika mpaka leo, wakasema hebu twambie kuna tatizo gani? Nasema wale waheshimiwa wenye

matatizo ya namna hiyo nimeshatoa agizo la kuliondosha tatizo hili, na mimi mwenyewe nitalifuatilia baadae ili nione kwamba limeondoka au halikuondoka.

Kuna waheshimiwa waliozungumza kuhusu mgogoro wa ardhi. Mhe. Spika, nayazungumza haya kwa jumla ili tupate nafasi yakuja kupitisha vifungu. Waheshimiwa wamezungumza masuala ya mgogoro wa ardhi, wamezungumza masuala ya hakuna majaji wa kuhukumu kesi za ardhi kwa hivyo migogoro inaingia na kuingia hata Mhe. Abubakar alizungumza idadi ya kesi zilizoko Mahakamani Unguja na Pemba ambazo hazijashughulikiwa. Lakini Mhe. Abubakar alisema na hilo mimi nalikubali kwamba bado nitaendelea kushirikiana ili kuongeza idadi ya Mahakimu katika sehemu zote zaidi ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Kaskazini Pemba tutaongeza Kusini Pemba na Mikoa mengine yote tuwe na Majaji na Mahakama ili masuala hayo yaondoke.

Mhe. Spika, kuna jengine la jumla kuna waheshimiwa hawa nawashukuru sana, kuna Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa, Mhe. Nassor Salim Ali na wale niliokuwa sikuwataja watanisamehe sio kama siwathamini lakini kuna waheshimiwa kwa jumla wanachimba visima kuwapatia wananchi wao maji. Hili ni jambo zuri la kuwaondoshea wananchi matatizo ya bidhaa muhimu sana, wasi wasi niliwaelezea waheshimiwa hawa na nitaendelea kuzungumza hapa na nitawaomba kwamba madhali zamu za maji zinaingiliana kwa masafa marefu sana.

Mhe. Spika, ukichimba kisima Kikwajuni mdhiramu wa maji unaweza ukafika Kisimamajongoo kwa wale wanaoijua jiografia ya Kikwajuni na Kisimamajongoo. Kama mnidhamu ule umebeba virutubishaji vya maradhi badala ya kuwapa wananchi maji safi na salama unawapa wananchi maji yatakayowaambukiza na kuwaletea maradhi. Nimesema mara kwa mara muwe mnapeleka *sample* za maji pale kwenye idara yetu kwa kuchunguzwa na pale itakaponekana kuna hatari tutatoa dawa tena bure kuhakikisha wananchi mnawapa maji ya salama. Kwa hivyo, sasa nasema kama kuna mwananchi anataka kuendelea kuchimba kisima naomba sana kwanza waje idarani ili tutafute hapo patakapochimbwa ni wapi. Hilo la kwanza.

Mhe. Spika, la pili baadae wafuate ule utaratibu wa kuleta *sample* mara kwa mara tufanye uchunguzi, hatukatazi kabisa wananchi kutusaidia kuchimba maji kwa ajili ya wananchi wao, sisi tunaomba mambo mawili tu kwanza mtuletee taarifa mapema na pili tuwe tunaelewana mko wapi ili tukufuatilieni kuchukua *sample* za maji yenu. Wale waliozungumza wana matatizo ya maji nimeshayatolea ufafanuzi tena wengine tumezungumza pembeni tukakubaliana, lakini ndio wana siasa maana waseme hapa wasikilizwe na wananchi wao wawasikie sio kosa hata kidogo. Lakini tumezungumza pembeni tukaelewana

kwamba mimi nitakuja na wengine nimeshawatumia maofisa wangu kwenda kuchunguza kwamba kweli sehemu ile haina maji na kama haina maji tufanye nini.

Mhe. Spika, jibu hili nimejibu pia la Mhe Jecha Ussi Jecha na suala la tangi nimembiwa *plate* za chini zimeshapatikana. Hawa mwanzo walidhani ni ile miguu ya tangi ndio iliyoharibika kumbe sio miguu ya tangi. Kwa hivyo, *plate* zimeshapatikana kazi ya kulirekebisha hilo tangi itafanywa mapema iwezekanavyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa ulizungumzia nyumba za maendeleo za Gamba kama ungejaaliwa ukaziona nyumba za maendeleo za kule Kusini basi usingezungumza Gamba za Gamba bado ni nzuri zinatizamika, lakini tunakubali ushauri wako. Tunakubali ushauri wako bahati mbaya sana fedha tulizonazo ni kidogo katika bajeti yetu. Tumefanya mapitio nyumba za Kengeja ambazo zilionekana hizi ndio aghasi na ni kweli. Nitakupa buku hili baadae uliangalie ili likusaidie kulinganisha nyumba zako za Gamba na nyumba za Kengeja hali iko vipi halafu utatambia bajeti ndogo tuliyonayo tukaanze wapi kwanza.

Mhe. Spika, vile vile alizungumza suala la *Five Star Hotel* itakayojengwa pale Mji Mkongwe na ukauliza mbona tumeanza kuvunja Starehe Club n.k. nasema haya majumba ya Mji Mkongwe yana daraja, daraja A,B na C ukitaka kufanya marekebisho daraja A, B na C kwa kiwango chochote inabidi upate kibali cha *UNESCO* mzungumze mkubaliane, lakini daraja zaidi ya hapa una mamlaka ya kufanya marekebisho yako wewe mwenyewe. Starehe Club haina daraja kwa bahati nzuri kwa sisi kwa bahati nzuri kwa hiyo Club yenyewe. Lakini takriban ilikuwa imeshatupwa na ina mambo mabaya sana yanayofanyika usiku hadi usiku ameshakufa mtu pale, pamoja na mambo mengine pamoja na kwamba haina daraja hilo ndio lililotufanyisha tuivunje ile Starehe Club ili tupate eneo la kutanua ile hotali inayotaka kujengwa.

Mhe. Spika, katika hili tumeshazungumza na *UNESCO* tumeshafanya mikutano mara tatu tumeshakubaliana kazi tatu walizotupa tuzifanye zimeshaanza kufanywa, *Environmental Impact Assessment* kufanya *assessment* ya Mji Mkongwe tumeshakubaliana kimsingi tukimaliza tunaanza ujenzi.

Mhe. Asaa Othman Said umesema unachukua asilimia tisini unaniachia asilimia kumi nakuomba unirejeshee kutokana na maelezo niloyoyaeleza na nilisema *Unless Use Wise* unanambia kwa kauli moja hapa na kauli ambayo itabidi tuipeleke Baraza la Mapinduzi tukajadili tena tufute kauli iliyotangulia mimi nitakuwa tayari kuunga mkono asilimia mia moja yale yote

mliyozungumza na nitatekeleza moja baada ya moja, kwa hivyo nilivyokuwa najibu lile suala la jumla la mambo ya mafuta nimekujibu.

Mengine tunayapokea na tunayafanyia kazi na nakuomba Mhe. Assa Othman Said nikija Pemba tukutane tukae pamoja tuzungumze matatizo unayoyazungumza yote, matatizo mengine yanazungumzika na yanatekelezeka. Kwa hivyo narejesha tena ombi langu kwako.

Mhe. Spika, kwa muongozo huo nataka nimalize kidogo hoja za Mhe. Hija Hassan Hija kwa zile za mafuta sina jibu jengine zaidi, ila nasikiliza maamuzi ya ukumbi huu. Kijiji cha Mkiang'ombe kisaidiwe maji hata kama ni solar tumepokea na tutalifanyia kazi. Kijiji cha Msengele hakijapatiwa umeme nimelipokea nitalifanyia kazi, nilikuwa naomba tu haya maeneo mengine ambayo hayajapata umeme na yanahitaji yapatiwe umeme tusaidiane Waheshimiwa wawakilishi, wabunge na Idara kuchangia masuala haya ili umeme uwafikie wananchi, shirika langu hivi sasa linakwenda katika njia ya *deficity*. Na bila ya kusaidiana hatuwezi kwenda vizuri.

Mhe. Spika, sasa baada ya maelezo haya marefu niliyoyatoa kwa wale ambao sijawagusa mmoja mmoja wataniwia radhi, lakini naomba kuweka msimamo kwamba wale wote walionielezea matatizo yao yawe ya umeme yawe ya maji nimeyaandika, kazi sasa itakuwa kwenye *field* mimi na nyinyi bega kwa bega tuangalie maeneo haya tuweze kutizama uwezekano wa kuyaondosha, sisemi wala siahidi kama nitayaondosha yote kwa pamoja lakini nia ninayo, uwezo ninao sina mpango wa fedha tu lakini tukishirikiana kwa pamoja atutayaondosha.

Mhe. Spika, sasa naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wa kina kabisa kwa mambo mbali mbali hasa yale masuala ya mafuta.

Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Kwa kuwa muda uliobakia ni mdogo naamini mnaweza kumaliza kupitisha kasma mbali mbali kwa dakika 15, lakini tuweke hakiba. Nimuombe basi Mhe.

Waziri ili atoe hoja kama muda utakuwa mwingi zaidi basi mpaka tumalize shughuli hii.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Spika, kwa kuwa muda uliyo mbele yetu hautoshi kukamilisha shughuli iliyo mbele yetu. Kwa hivyo, naliomba Baraza lako tukufu litengue muda uliyo kwenye kanuni ili tuweze kukamilisha shughuli iliyo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hoja ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## FUNGU 25 – WIZARA YA ARDHI, MAKAAZI, MAJI NA NISHATI

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0301 | Afisi Kuu Pemba | 61,600,000 |
| Kifungu 0501 | Idara ya Ujenzi | 5,000,000 |
| Kifungu 0701 | Hifadhi ya Mji Mkongwe | 21,900,000 |

**Mhe. Mbarouk Ali Mussa (Mtando):** Mhe. Mwenyekiti, katika mchangio wangu nilizungumzia suala la Mji Mkongwe hasa pale kwenye eneo la uendelezaji wa ujenzi katika Mambo Msiige. Katika majibu ya Mhe. Waziri hapa ametoa maelezo lakini sijaridhika na hayo maelezo aliyoyatoa. Suala langu la msingi lilikuwa ule ujenzi ambao unafanyika pale pamevunjwa kabisa, nilikuwa nauliza kuhusu hawa watu wa *UNESCO* uvunjwaji ule unapinzana na matakwa ya watu wa *UNESCO*.

Kwa sababu katika maelezo yake huko nyuma kwenye kitabu alieleza kwamba hata kutoa lile dirisha tu huruhusiwi katika eneo la Mji Mkongwe kwa sababu ni hifadhi ya Mji Mkongwe. Sasa ule uvunjwaji kabisa wa eneo lile, inagawa katika maelezo yake amesema kwamba, palikuwa panasababisha vurugu, kuna mambomengine ambayo si ya kawaida, lakini je, ule uvunjwaji wa lile jengo la

klabu ni uvunjwaji katika eneo la Mji Mkongwe. Je, hawa watu wa *UNESCO* wamefikiana nao vipi katika uvunjwaji wa jengo lile. Nataka kujua hilo.

**UTARATIBU**

**Mhe. Haji Faki Shaali:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri angesubiri katika matumizi, kwa sababu haya ni masuala ya mapato.

**Mhe. Mwenyekiti:** Unajua maeneo yote mawili haya yanakuja, kwa sababu urithi huu wa Mji Mkongwe majengo yake kutobadilishwa, kutafanywa kila kitu maana yake ni kuendelea kupata mapato na msaada mkubwa kupitia hiyo *UNESCO* ambayo ni *World Heritage*. Sasa nadhani hapa pia ni pazuri tunaweza kupata maelezo kwa Mhe. Waziri.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa najibu hoja nilisema kwamba majengo ya Mji Mkongwe yana madaraja, daraja la kwanza, la pili na la tatu. Hayo ndio yanayo-*fall* chini ya *supervision* ya *World Heritage.*

Jengo hili la Starehe Club ni *extension* iliyofanywa halimo katika jengo la Mambo Msiige. Lakini la pili hili jengo halina daraja na ndio maana tukalivunja. Lakini tumekwenda Ufaransa *UNESCO* jengo hili halikutajwa kabisa, yaliyotajwa ni majengo jengo lenyewe kubwa la Mambo Msiige na limetwaja eneo ambalo liko wazi. Lile limeshakubaliwa tumepewa maagizo tufanye. Kwa hivyo, majibu hayo ndio majibu ambayo ningependa niyatoe.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando):** Mhe. Mwenyekiti, nafikiri katika maelezo yangu nilikuwa naeleza kutaka kujua uvunjwaji ule, ingawa Mhe. Waziri anasema kwamba jengo hili halimo katika hayo madaraja yanayovunjwa, yanayokubaliwa au yanayokataliwa sina uhakika vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri angenipa hizi aina za haya madaraja. Ikiwa tunasema nyumba moja ambayo iko katika *World Heritage* tukitoa dirisha moja ni tatizo. Sasa hii nayo tunahisi imo mle mle lakini bado Mhe. Waziri anaonekana anapiga chenga kidogo katika kunijibu, hajanijibu vizuri katika hili. Nataka ule uhakika hili eneo ambalo linahifadhiwa ina maana kuna nyumba unaweza kuvunja, kuna nyumba huwezi kuvunja. Sasa hebu atupe ufafanuzi hizo nyumba ambazo unaweza kuvunja na zile ambazo huwezi kuvunja.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, narejea tena kusema yale niliyoyasema. Jengo la Starehe Club halina daraja, ni jengo lililopachikwa. Lakini la pili hili jengo halijakuwa *registered* katika

majengo ya Mji Mkongwe. Majengo yanayotakiwa upate kibali cha *UNESCO* ni majengo yaliyokuwa *registered* kama ni World Heritage ya Mji Mkongwe. Sasa hili halimo na ndio maana tulipokwenda kuzungumza ile sekta nzima ya Mambo Msiige hili halikuzungumzwa kwa sababu halijakuwa *registered* katika haya majengo ya Mji Mkongwe.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kwa maneno mengine kuvunjwa kwake hakutaathiri hiyo heshima yetu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, hakutaathiri hata kidogo na ndio maana tumepewa kibali.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando):** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri amekiri kwamba hili jengo halimo katika orodha hizi naomba tuendelee.

**Jumla ya Kifungu**

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa hii ili kupata ufafanuzi kidogo kwa Mhe. Waziri. Kwa sababu alichukua muda mwingi kuzungumzia suala la mafuta kwa hiyo kuna hoja nyingi ambazo hakuweza kutusaidia ufafanuzi. Sasa nakusudia kuzuia kifungu hichi sio kama sitokipitisha lakini nilikuwa nataka maelezo. Kwa kuwa eneo ninalotaka kulizungumza liko katika Mji Mkongwe na hii hofu yangu akishaniondoa naamini kwamba yale mapato tunayoyapata kutoka *UNESCO* tutaendelea kuyapata.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikizungumzia kuhusu maeneo ya Mji Mkongwe nilizungumza katika eneo la Kinu cha Taa ambapo hivi sasa pamezungushwa mabati na sina taarifa kamili, lakini nadhani Mhe. Waziri atakuwa nayo hiyo taarifa kwamba panataka kujengwa aidha jengo la hoteli au hoteli ndogo *(restaurant).* Eneo lile tunavyojua kwamba ni *open space* na hapa katika mchakato wa wenyewe Mji Mkongwe walipokuwa wakilitetea wakati palipokuwa panajengwa ile bustani walisema eneo lile halitakiwi kujengwa kitu kisichozidi zaidi ya mita nne.

Sasa yale mabati nilikuwa nataka nipate ufafanuzi kwa Mhe. Waziri kwamba je, panataka kuendelezwa tena kujengwa bustani nyengine ili iungane na iliyokuwepo au panataka kujengwa kitu chengine ambacho kitainuka juu kinaweza kikatuharibia yale masharti ya *UNESCO* tukaja tukakosa hizo fedha.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli sikupata kulizungumza suala la hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma. Lile eneo lililozungushwa mabati ni sehemu ya hoteli ya pili ukiacha hoteli ya Mhe.

Salum Hassan Turkey. Ile ni sehemu ya kiwanja cha Klabu ya Malindi. Klabu ya Malindi imewapa hii hoteli ya pili ili wajenge bustani kama alivyojenga Mhe. Turkey katika lile eneo la kwanza. Kwa hivyo, pale hapajengwi kitu chochote kitakachokwenda juu. *Purely* ni eneo mwenye hoteli ile ameliomba kwa watu wa Malindi na watu wa Malindi wamemkodisha na kwa hivyo itajengwa bustani na sio ujenzi mwengine wowote.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa ufafanuzi wa Mhe. Waziri naamini kwamba Mji wetu Mkongwe sasa hivi unazidi kuimarika hasa baada ya ile bustani ya mwanzo iliyowekwa na sasa hivi inawekwa nyengine.

Lakini swali langu liko hapa, maeneo ya *open space* ni maeneo ya serikali na yanatakiwa wananchi waweze kuyatumia kwa uhuru bila ya usumbufu wowote. Sasa maelezo ya Mhe. Waziri anasema Klabu ya Malindi ambao wao ndio wamiliki wa eneo lile wamekubaliana na yule mjenzi wa hoteli kwa ajili ya kuweka ile bustani.

Sasa kwa kuwa Klabu ya Malindi wanategemea kupata mapato. Je, hiyo bustani itakayokuwepo hawa wananchi wataruhusiwa kwenda kukaa kupumzika na kujisomea au watatakiwa walipe ada yoyote katika hili eneo ambalo kwa sasa hivi tunajua ni *open space.*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, bustani inayojengwa katika eneo hilo ni sawa sawa na bustani inayojengwa katika eneo la Turkey. Ni kwa *public use* na anayetaka atakwenda kama kujisomea au kufanya jambo lolote. Mapato ya eneo lililokodishwa yanakwenda kwenye Klabu ya Malindi kwa sababu wamekodisha.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0701 | Hifadhi ya Mji Mkongwe | 21,900,000 |
| Kifungu 0901 | Idara ya Ardhi na Usajili | |

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando):** Mhe. Mwenyekiti, katika michangio yangu nilizungumzia suala la uvamizi wa eneo la Chuo cha Utalii lakini Mhe. Naibu Waziri alitoa majibu hapa kidogo sijapata maelezo ya kutosha.

Kwa sababu eneo lile limevamiwa, nilikuwa nataka kujua zile hatua ambazo zimechukuliwa katika uvamizi ule na kurejesha lile eneo la chuo kutoka kwa yule mvamizi ambaye amevamia kulirejesha kwenye eneo la chuo. Je, ni hatua gani ambazo serikali imechukua hadi hivi sasa katika hili.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sasa hilo nafikiri twende kwenye sehemu ya matumizi. Kwa hiyo, hapa tuendelee. Kuwa macho sana ushike kwenye sehemu ya matumizi upate ufafanuzi.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0901 | Idara ya Ardhi na Usajili | 1,873,500,000 |
| Kifungu 1001 | Idara ya Upimaji na Ramani | 236,343,000 |
| Kifungu 1101 | Idara ya Nyumba na Makaazi | 100,000,000 |
| **Jumla ya Fungu** | | **2,298,343,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 25 - Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0301 | Ofisi Kuu Pemba | 691,223,000 |
| Kifungu 0302 | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | 600,000,000 |
| Kifungu 0401 | | |

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu ambao nilijikita zaidi katika suala moja tu la mafuta kuna masuala kadhaa niliyaombea ufafanuzi.Namshukuru sana Mhe.Wazirina Waheshimiwa wengine wametusaidia ufafanuzi mbali mbali. Lakini kuna mambo nilikuwa naomba niwekewe sawa ili tuendelee.

La kwanza nilihoji Mhe. Mwenyekiti, humu Barazani kikao hichi hichi kulikuwa na kauli za kugongana kwamba suala hili la mafuta na gesi asilia limeingizwa katika kero za Muungano au halimo. Nikataka kujua tukamate kauli ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais aliyesema si suala la kero za Muungano na linajadiliwa na viongozi wa juu, au tukamate kauli ya Waziri wake wa Nchi aliyetwambia siku ya tarehe 20 Juni mwaka huu kama *hansard* zinavyoonesha kwamba suala hili limo katika mambo ambayo yanasubiri kutatuliwa katika kero za Muungano. Hilo moja.

Pili Mhe. Mwenyekiti, nilizungumziwa vile vile serikali iliwahi kusema humu ndani kwamba hatuna sheria, nikaitaja sheria ya mwaka 1951. Nimesikiliza kwa makini sana leo ufafanuzi uliotolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu na pia Waziri wa Katiba na Sheria.

Nimekanganyikiwa kidogo kwa sababu moja katika *reference* zangu za kuitambua sheria hii ya mwaka 1951 ni maelezo yaliyotolewa na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria wakati huo akiwa Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni na Kiongozi wa Upinzani katika *hansard* ya tarehe 3 Aprili, 2009. Ukurasa wa 76 na 77 Mhe. Abubakar Khamis Bakary alisema sheria hii ya *Mining Decree* naitambua ni halali na akamuomba Waziri wa wakati ule Mhe. Mansoor Yussuf

Himid kwamba amuachie yeye dhamana ya ulinzi wa sheria hii kwa sababu yeye Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kazaliwa mwaka 1951 kama ilivyokuwa sheria hii.

Sasa kidogo hapa nimepata utatanishi. Kwa sababu mimi nilitegemea katika *reference* zangu moja kwa moja sheria hii niliyomwambia Mhe. Abubakar Khamis Bakary kwamba *authority* ni hii ambayo aliizungumza katika hansard hii ya mwaka 2009. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua tu hii misingi ya sheria imebadilika baada ya 2009 na 2011 kwamba sheria hii sasa si halali tena.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa ambalo pia sikulisikia pamoja na maelezo ya kutosha, nilihoji utekelezaji wa maazimio ya Baraza. Mhe. Mwenyekiti, nataka niweke wazi kwamba nimefuatilia sana mjadala huu lakini sikumbuki kwamba wengi wetu tulizungumzia kutaka *revise* au kukazia yale maamuzi ya Baraza. Tulisema utekelezaji sasa wa maazimio ya Baraza katika kikao cha 2009 ambapo mimi mwenyewe nayatambua ndio maana niliyanukuu katika mchango wangu.

Sasa ufafanuzi katika hili Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba azimio la pili lilitaka kuanzishwa kwa chombo kitakachosimamia utafutaji na uchimbaji wa mafuta. Ili niweke wazi Mhe. Mwenyekiti, naomba nirejee tena ifahamike vizuri.

Lile azimio la pili lilikuwa linasomeka kwamba wanaokubali pendekezo la kuishawishi Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwamba sasa wakati umefika kuunda chombo chake cha kusimamia utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi wanyanyue mikono.

Sasa nilikuwa nauliza Mhe. Mwenyekiti, kwamba hii sasa mimi nilikuwa sijaielewa, lakini kama tunajibiwa leo kwamba hoja hii haiwezekani kwa sababu ya matatizo ya kikatiba. Sasa kwa kusaidia hili Baraza lako mimi sikuwa mjumbe wako Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni ushahidi huo. Baraza lako lilipotoshwa kupitisha maamuzi ambayo ni kinyume na katiba. Naomba ufafanuzi huo Mhe. Mwenyekiti, halafu tuendelee.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, mgongano wa Kikatiba wa kisheria nilizungumza na hilo halina utata, inategemea *concentration* ya mtu anavyoizungumza, lakini mgongano upo wa kikatiba na hakuna asiyejua kati ya katiba yetu na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Moja katika masuala ya migogoro ya Muungano au migogoro ya kuendesha shughuli zetu za Muungano yanayotokana katika tafsiri na migongano ya katiba zetu mbili. Kwa hiyo, nadhani niliposema nimesema kwa uhakika na sikuwa na

makosa, kama kuna tafsiri nyengine iliyokuwa nzuri zaidi ya kulielezea suala hili niko tayari kusahihishwa na nitaitumia hiyo tafsiri iliyokuwa nzuri zaidi.

Lakini la pili, utekelezaji katika yale maamuzi ya Baraza la Wawakilishi lililopita yaliyoandikwa kwenye *hansard* kwamba utekelezaji uchukuliwe mara moja au kutekelezwa mara moja. Nasema maamuzi bado ni sahihi ninayaheshimu, labda katika maandishi tulikosea kuandika vizuri hilo si tatizo kwa sababu tunaandika tulichokisema. Lakini mimi nasema wakati ukifika nitatekeleza maagizo ya Baraza la Wawakilishi, agizo moja baada ya moja katika maagizo matatu iliyopewa.

Sasa kama kuileta sheria hii kwenye Baraza la Wawakilishi nilisema haidhuru maamuzi ndio hayo lakini kuna utaratibu wa kufuatwa. Tutaanza kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu, tutakwenda Baraza la Mapinduzi. Kamati ya Makatibu Wakuu wanaweza kutushauri, wanaweza kukataa, wanaweza kusema liahirishwe, halikadhalika Baraza la Mapinduzi. Maamuzi hayo yatakuwa bado ni sahihi kwa sababu wakati ukifika tutatoa agizo kwamba sasa leteni tulizungumze ili tutekeleze. Ahsante sana.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sijui kuna hoja ile kuhusu misingi na taratibu.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa Ladhu alikuwa anatoa *reference* ya *hansard* ya vikao vya Baraza vilivyopita, kuna moja aliyo-*quote* ni ya kwangu mimi. Matatizo ya *hansard* Mhe. Mwenyekiti, hilo ningeliomba sasa litekelezwe. *Hansard* kwa utaratibu ni kwamba unapomaliza kusema anapewa mwenyewe mjumbe kuhakikisha kwamba yale aliyoyasema ndio. Sasa kitendo hicho kilikuwa hakipo siku nyingi, sijui kwa matatizo tunajua, lakini kwa *hansard* kama hizi ambazo zina makosa makosa kidogo yanaweza yakaleta athari baadae.

Mimi nakumbuka kama kweli nilisema kwamba sheria ya 52 ipo wakati mimi nimeshazaliwa. Lakini kama nitakumbuka vizuri na Waheshimiwa Wajumbe watakumbuka, nilisema kwamba sheria hii inataka marekebisho ili iweze kuwa ni sheria sahihi.

Katika lugha ambayo tuliisema wakati huo, sasa ikiwa alichosema ndio kile tu nafikiri ama hakukisoma chote au hakufahamu, maana yake Kiswahili changu cha Kipemba na cha Kihindi ni tofauti, inaweza ikawa hivyo. Bado Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba sheria ya 52 *cap. 108* ipo lakini sheria ile kwa mujibu wa taratibu zetu haiwezi ikawa ndio sheria ya hivi sasa kutawala, ni lazima sheria ile inaweza ikafanyiwa marekebisho au inaweza ikafanywa nyengine kwa madhumuni ya hapa. Lakini ile peke yake haiwezi kutumika na huo ndio msimamo wangu kuanzia juzi mpaka leo.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, kama utanambia kwamba *hansard* zako zote tusizitambue zina makosa nitaiacha hoja yangu. Lakini kama siku zote zilitambuliwa kama ni rekodi halali nitaendelea kuing'ang'ania. Ili Kiswahili cha Kijini Makunduchi na cha Mgogoni kisigongane naomba niisome kidogo. Kwa sababu ni vizuri sisi wawakilishi na wananchi wakalielewa suala hili. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba ninukuu ukurasa wa 76 Mhe. Abubakar Khamis Bakary anasema "Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria zetu nyengine na hapa mimi naomba nitaje *special* sheria hii inaitwa *Mining Decree* ya mwaka 1951.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ina sheria inayoitwa *Mining Decree* ya mwaka 1951 na sheria hii ningelimuomba Mhe. Waziri anipe mimi niilinde kwa sababu maalum. Kwa sababu mimi nilizaliwa mwaka 1951 na hii Minin*g Decree* ni ya mwaka 1951, kwa hivyo mimi sitokubali sheria hii kumegwa ovyo bila ya sababu yoyote. Nitakuwa mlinzi mkubwa wa sheria hii ya *Mining Decree* ya mwaka 1951."

Kwa maana hiyo, *decree* ile inasema dhahiri katika kifungu kimoja nafikiri cha 7 au 8 kama hivi, kinasema kwamba mafuta ni mali ya Zanzibar haijafutwa mpaka leo. Halafu tena akaendelea kwamba imefanyiwa kanuni. Lakini niko hapo mimi kwamba yeye mwenyewe anaitambua haijafutwa. Sasa katika kunisaidia ufafanuzi leo alinambia kwamba sheria hii kwa misingi ya kisheria si halali. Ndio najiuliza hii misingi ya sheria Mhe. Mwenyekiti, alisaidie Baraza lako kupata ripoti sahihi. Ile ya mwaka 2009 na 2011 tumebadilisha misingi ya kisheria kwamba sheria hii sasa si sahihi tena kama alivyosema mwaka 2009 na kwamba haijamegwa.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kuna suala langu ambalo halijajibiwa niliuliza. Katika suala hili la mafuta *position* ya serikali ambayo tulikuwa tukiambiwa kwamba suala hili halimo katika orodha ya kero za Muungano na linajadiliwa na viongozi wa juu. Kwa sababu Baraza la Wawakilishi bado hatujafanya maamuzi kwa niaba ya Wazanzibari. Tukilipeleka kwenye Kamati ya Kero za Muungano maana yake linaendelea na mjadala wakati sisi huku hatutaki mjadala.

Lakini nilisema hapa ukiangalia tena *hansard* ya kikao hichi tarehe 20 Juni, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika kutaja kero za Muungano zilizobakia alitaja namba (2) utafiti na uchimbaji mafuta na gesi asilia. Kwa hivyo, naomba hebu wazo hili la Mhe. Abubakar Khamis Bakary kuhusu sheria ichukue nafasi yake, anataka nikamate *position* yake ya mwaka 2009 au hii aliyoitoa leo asubuhi. La pili katika hili la kero za Muungano

nikamate kwenye Makamo wa Pili wa Rais au nikamate kauli ya Waziri wake wa Nchi ili tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nitoe ufafanuzi. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nimkumbushe Mhe. Mwakilishi kwamba sikio halipiti kichwa. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba katika orodha ya mambo ya Muungano suala la mafuta na gesi asilia katika kero za Muungano liliulizwa. Lakini baada ya serikali kuliingilia na viongozi wakuu kuliingilia katika kulitafutia utatuzi wake, busara iliyotumika katika vikao vyetu vya pamoja kwamba jambo hili tulifunge mjadala wake na tusubiri maamuzi ya ngazi ya juu ya serikali. Kwa hivyo, tushike maamuzi aliyoyatoa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

**Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa Ladhu anauliza kwamba kauli yangu niliyotoa wakati huo na kauli yangu hii ipi ichukuliwe. Kauli hii wakati ni Waziri wa Katiba na Sheria ichukuliwe.

**Mhe. Ismail Jussa Ladhu:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na nafurahi kwamba nitajifunza kuheshimu zile kazi zetu ambazo tunazitoa tukikumbuka kwamba historia zote tunazirekodi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwa sababu moja tu, pamoja na hoja uliyoizungumza kwa hisia kali ya suala la mafuta. Naheshimu sana mchango wa ndugu yangu Mhe. Mansoor Yussuf Himid, nadhani na Mhe. Mwanasheria Mkuu aliposisitiza sana juu ya suala la kutoweka nyufa katika suala hili la kwenda pamoja.

Ingelikuwa si hilo Mhe. Mwenyekiti, ningelikuwa mkali sana, lakini kwa kuheshimu na najua Wazanzibari wanatusikiliza na wangependa viongozi wao wa Zanzibar kama ilivyoombwa hapa, kuanzia serikali, wawakilishi na wananchi tuendelee kusimama pamoja hatimae kulinda maslahi ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, nakubali tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Katika hili suala la *hansard* naomba Waheshimiwa Wajumbe tujifunze jambo moja. Kwamba chombo hichi ni chombo kikubwa na tunayo tabia ya kuzungumza kwa hamasa wakati mwengine, ukizungumza kwa hamasa maneno yanaweza yakateleza kidogo na yanarekodiwa basi maneno yale. Binafsi unapokuja kuoneshwa baadae unaweza ukasema mh, ndio maneno yangu haya, ukataka kuyakana. Kumbe umeyazungumza katika chombo rasmi cha kutunga sheria na ulikuwa unatumia haki yako kikatiba na kwa mujibu wa kanuni.

Sasa tuwe macho sana tunapozungumza kwenye chombo hichi, tuzungumze kwa utulivu, bila ya hamasa na twende kwenye pointi tunayoikusudia, ili tuhakikishe kwamba maelezo yale hata wakija watafiti baadae watasema kwamba hapana hapa huyu amezungumza kitu cha ukweli na bado kina uhai wake. *Of course* mambo yakibadilika inawezekana nguvu ya lile jambo likawa limebadilika pia, lakini angalau yale maneno yawe yana usahihi. Naomba tujifunze hilo nalo ni muhimu sana.

Unajua taratibu za kupitisha mafungu haya kwa mujibu wa kanuni zetu kila kifungu kinaweza kikahojiwa na watu watatu, yaani hoja tatu. Sasa kwa bahati mbaya hoja tatu hizo zote kachukua Mhe. Ismail Jussa Ladhu, moja ikajibiwa hapa, moja ikajibiwa hapa na nyengine hapa. Sasa kimsingi hoja tatu kwa mujibu wa kanuni ya 96 (3) zimeshamalizika kwa mujibu wa kifungu hichi. Sasa kama kuna kifungu kingine huko tuendelee.

Basi niwaombe radhi sana Waheshimiwa Wajumbe tujaribu kufuata kanuni yetu hii ili tuweze kwenda vizuri katika shughuli zetu.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0401 | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 130,754,000 |
| Kifungu 0402 | Mamlaka ya Maji Zanzibar | |

**Mhe. Ussi Jecha Simai:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Jana nilipokuwa nikichangia hotuba hii Mhe. Mwenyekiti, nilimkumbusha Mhe. Waziri kwamba katika kijiji changu cha Moga kuna ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu tangu mwaka 2008, watu wangu wanapata shida ya maji, lakini katika ufafanuzi suala hili sijalipata vizuri.

Suala la pili Mhe. Mwenyekiti, pia pale Chaani Kubwa kuna tatizo la maji ambapo kuna kisima ambacho kimechimbwa mwaka 2008 kwa kushirikiana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Mradi wa TASAF, hadi hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, *transformer* haijapatikana na wananchi wangu wanapata shida kubwa sana ya tatizo la maji. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aniambie ni lini tatizo hili litaondoka pale, ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ahadi ya Makamo wa Pili wa Rais nitaifuatilia kwake yeye mwenyewe au kwa watu wake, ili nijuwe kwamba kweli alitoa ahadi hiyo na kama kweli aliitoa, basi atatekeleza lini. Kisha nitakuja kumjibu Mhe. Mjumbe kwa maandishi.

Suala la Moga nadhani nakubaliana na yeye. Nasema kama nilivyosema wakati nafanya majumuisho wale wote ambao wanamatatizo ya maji kutokufika na umeme kutokufika, nilisema nitakwenda kuwapitia mmoja baada ya mmoja, ili

nihakikishe hilo suala naliona kwa macho yangu na nitafute njia ya kulitekeleza na kuliondosha.

**Mhe. Ussi Jecha Simai:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kuwa Mhe. Waziri ameniambia kuwa atafanya utafiti na aangalie kama kweli kule Moga kuna ahadi ya Rais, basi atalishughulikia suala hili. Lakini nataka nimkumbushe kwamba ninapozungumza suala la *transformer*, nazungumzia Chaani Kubwa ambapo kuna kisima kilichimbwa kwa msaada wa TASAF pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hadi hii leo *transformer* inashinda pale na wananchi wangu wanakosa maji.

Kwa hivyo, hili ndio nilikuwa nataka aniambie Mhe. Waziri, ni lini. Wakati ile miradi yote ya awamu ya pili imemalizika na sasa hivi tunasubiri awamu ya tatu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nimesema na naendelea kusema kwamba nikimaliza bajeti nitawapitia wale wote nimewa-*record*, wenye matatizo ya *transformer*, wenye matatizo ya maji na wenye matatizo ya umeme, ili tuyaangalie matatizo yao, uwezo ukiwepo yaweze kushughulikiwa.

**Mhe. Ussi Jecha Simai:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru naomba tuendelee.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilikuwa nikichangia sehemu hii na nilipochangia nisema katika Jimbo langu kuna Shehia ya Mtambwe Kaskazini tu ndio ambayo itapatiwa maji na ni vijiji vya Mtambwe Mkuu, Chekea, Kidundo, Mkia wa Paka na Chanjani. Lakini nilisema kuna vijiji vingi tu kama vile Makongeni, Kokota, Mitambuni, Kinazini pamoja na Mleteni na Malindini huko kote hakuna na jimbo ni hili hili moja. Kwanza nashukuru angalau kupata shehia moja, lakini ni vigezo gani vilivyotumika mpaka maji yakapelekwa katika shehia moja tu. Sasa hivi vijiji vyengine ambavyo havina kuna ushauri gani, naona Mhe. Waziri katika kujibu hakunieleza.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nilijibu swali la mwisho halafu nitajibu swali la mwanzo. Vigezo gani vilivyotumika mpaka shehia moja ikapelekwa maji na nyengine zikawachwa kama shehia sita. Kigezo ni uwezo wa idara au hiki kitengo cha maji, kutokana na bajeti ndogo tunayopewa.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tatizo la maji litaweza kuondoka kwa kutegemea zaidi misaada tunayopita tukiiomba hapa na pale. Kama nilivyoeleza katika bajeti yangu kuna misaada mingi sana inakuja na kwenye ramani hii kuna visima 30 tumeviweka, ambavyo tutachimba na wananchi watapata maji.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tatizo la maji kama ni kuondoka au kupungua sana, nilisema ifikapo mwaka 2013. Sasa siwezi kutoa jibu kwamba. Hili ninalojibu ni lile swali la mwanzo. Kwa nini eneo jengine wanapata maji lakini eneo jengine hawapati maji. Hilo halitawezekana kwa Zanzibar nzima Unguja na Pemba, kwa kipindi kimoja wakati mmoja iweze kusambaza maji mji mzima, hilo halitawezekana. Lakini watakaopata washukuru, waliokuwa hawajapata, pole pole mpaka mwaka 2013 sasa hapo ndipo tuje tuulizane maswali wakati umefika bado hatujapata maji, ahsante.

**Mhe. Salim Abdalla Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa jibu zuri nililopata. Lakini Mhe. Mwenyekiti, ningeomba Mhe. Waziri ajuwe kuwa hata huko Mtambwe Kaskazini mimi binafsi nimetumia zaidi ya milioni 4, ili watu wapate maji. Huko Mtambwe Kusini hata juzi tumetumia zaidi ya milioni 2 pamoja na Mhe. Mbunge ili watu wapate maji. Mimi naisaidia sana mamlaka hii. Halafu unapokwenda katika mamlaka kutaka maji, utapiwa vipimo vyote ukinunua unatengenezewa na baadhi ya vifaa huviona viko.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tatizo ni tatizo halafu sisi Wawakilishi haionekani kuwa sisi tunavyofanya ndio juhudi ya mwisho kwenye serikali, lakini huonekana kuwa hatutetei watu. Kwa hivyo, wakati kachukuwa wizara angeniambia atafanya mpango gani zaidi ili kuona kuwa haya matatizo yameondoka kwa sababu lile jimbo nalijua mimi.

Mhe. Mwenyekiti, ukikosa maji katika kijiji kwenye Jimbo la Mtambwe, maana yake uteremke milima tena usiku ni adha kubwa sana, ni tofauti na hapa unaletewa kwa kununua kwa ndoo. Kwa hivyo, nikizungumza kitu basi kitiliwe mkazo wa hali ya juu. Namuomba Mhe. Waziri pamoja na kuwa anasema bajeti ni ndogo, lakini ana njia chungunzima za kuomba misaada huku na kule anisaidie ili vile vijiji vingine navyo vipate maji.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Salim Abdalla Hamad kwa juhudi aliyochukua kulisimamia jimbo lake na fedha nyingi sana alizotumia. Nataka nimwambie huo ndio utaratibu mzuri wa kuwatumikia wananchi wake na ni mfano mzuri alioutoa.

Labda nimpe habari tu, hata mimi juzi nilitumia milioni 13 kununua *ambulance* katika jimbo langu. Kwa hivyo, huo ni utaratibu mzuri. Sasa ameniomba nimtizame kwa jicho la huruma. Nasema kuna mradi mmoja bado wa mkopo wa Wachina utakuja. Namuahidi katika jimbo lake nitampelekea miradi mitatu.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa hii nafasi. Nilipokuwa nachangia nilizungumzia suala la uondoshwaji wa jenereta katika kisima cha Kiashange, jenereta limeondoshwa pale likiwa zima likapelekwa katika kisima kibovu. Mimi nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri atupe ufafanuzi hapa kuhusu uondoshwaji wa jenereta lile, baadae liliondoshwa kabisa katika maeneo lile sijui limeletwa mjini au sijui limepelekwa wapi linasababisha usumbufu kweli kweli. Kwa sababu unapozimika umeme sasa hivi wilaya nzima karibu inakosa maji kwa sababu kisima cha Kiashange kinatumika katika Wilaya nzima ya Kaskazini ‘A’. Mhe. Waziri anipe ufafanuzi juu ya suala zima la jenereta kuondoshwa kwake pale na lini litarudi pale.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli jenereta liliondoshwa na si kwa sababu nyengine yoyote isipokuwa kwa sababu liliharibika. Jana katika majumuisho yetu Wizarani nimearifiwa hilo na nikaambiwa *immediately* likimalizika litarejeshwa pale pale. Sasa hiyo *immediately* namuomba Mheshimiwa anipe muda nifuatilie ili nijue ile *immediately* maana yake nini. Lakini kwa lugha nyepesi haraka hara litarejeshwa hilo jenereta, halikuondolewa kwa sababu nyengine yoyote ila liliharibika.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando:** Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubaliani na Mhe. Waziri kuwa jenereta lile liliondoshwa kwa sababu liliharibika, kwa sababu mimi mwenyewe nilikwenda pale na jenereta lile kama jana tu umeme ulikuwa umezimika na lilifanya kazi, likaondoshwa pale kupelekwa kwenye hicho kisima kingine ninachokisema. Lilipopelekwa kule liliangushwa ndio uharibifu ulipoanzia.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kujua hii sababu ya kuondoshwa kwenye kisima kizima na kupelekwe kwenye kisima kibovu, halafu mpaka leo kama ni *immediately* litarejeshwa lina karibu mwezi wa nane sasa hivi, tangu kuondoshwa pale halijarudishwa. Basi aniambie Mhe. Waziri ni lini litakuwa limerudi jenereta pale ili unapozimika umeme waweze kupata maji.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, jenereta litarudi kabla ya kumalizika mwezi huu tulionao.

**Mbarouk Wadi Mussa Mtando:** Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Mhe. Waziri ameahidi kabla ya mwezi huu kumalizika litarudi, basi tuendelee.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0402 | Mamlaka ya Maji Zanzibar | 1,800,000,000 |
| Kifungu 0501 | Idara ya Ujenzi | 464,600,000 |
| Kifungu 0701 | Hifadhi ya Mji Mkongwe | 208,801,000 |

Kifungu 0801 Idara ya Nishati

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia idara hii kwa heshima sana na taadhima, niligusia mawili kwenye Idara ya Nishati. Kwanza suala la TPDC na fedha yetu iliyoko kule kwa sheria ilioko ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti naelewa fika na ninafahamu msimamo wa Wazanzibari, msimamo wa Baraza hili, maamuzi ya Baraza hili. Kilichonifanya mimi nihoji kwa nini zisidaiwe fedha zile, ni baada ya kuona tunashiriki kwa mzunguko. Katibu Mkuu wa wizara hii anashiriki vikao, nikajiuliza imehalalishwa wapi tena, kama kushiriki vikao ni halali kwa Katibu Mkuu wa wizara hii basi na ile fedha iwe halali kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili nilitaka nione au nielezwe sheria ile ambayo ndugu yangu Mhe. Ismail Jussa aliieleza wazi wazi, lakini leo imekuja fungwa na Hansard kwamba zinakuwa na matatizo. Nasema naheshimu sitaki niendeleze hoja hiyo, lakini namuomba sana swahiba wangu, mzee wangu mpenzi kabisa na anajua siku zote niko pamoja na yeye kwa suala la Uzanzibari na yele tunayojuana mimi na yeye hebu atusaidie hapo, atusaidie ni kwa vipi Katibu Mkuu anaruhusiwa yeye kama yeye kushiriki huku na hili tumeshakubaliana basi. Mhe. Mwenyekiti, naomba hilo.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, sikuona maandishi yoyote kwenye Hansard katika maamuzi tuliyoamua kwamba Katibu Mkuu asihudhurie vikao vya TPDC. Nakubali kulikuwa kuna maamuzi ya jumla kwamba sisi sote tusishiriki kwenye TPDC na kwa hivyo tusiwaruhusu wao kutufanyia utafiti na kutuchimbia mafuta hata kama wataagiza wachimbaji wa kwao, hilo tulilizungumza.

Sasa kama uwamuzi ndio huo tafsiri yake kwamba Katibu Mkuu asihudhurie. Basi nimeusikia na nimeupokea na nitamuandikia rasmi kwamba asihudhurie.

**Mhe. Asaa Othman Hamad:** Mhe. Mwenyekiti, baada ya kauli thabiti tunayoisubiri naomba tuendelee.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana kuweza kunipa nafasi hii ili nipate ufafanuzi zaidi kwa Mhe. Waziri katika suala zima la mafuta. Mhe. Mwenyekiti, kwanza tunamuombea dua Mwenyezi Mungu ampe afya njema Mhe. Abdu Jumbe Mwinyi. Vile vile ampe afya njema Dk. Salmin Amour. Pia ampe afya njema Mhe. Rais wetu Mstaafu wa Awamu ya Sita Dk. Aman Abeid Karume, kwa kuwa na maamuzi magumu.

Namkariri Mhe. Lowasa, hivi juzi alianzisha mjadala bungeni, akasema Serikali ya Awamu ya Nne inashindwa kutoa maamuzi magumu.

Lakini kwa upande wa Zanzibar tayari Marais wetu watatu, Mhe. Abdu Jumbe, Mhe. Dk. Salmin Amour na Mhe. Dk. Aman Abeid Karume wamefanya maamuzi magumu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri na yeye awe mjasiri ajitahidi kutoa maamuzi magumu.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu liko hapa nataka Mhe. Waziri anisaidie ufafanuzi. Tumepata ushauri mzuri kwa Mwanasheria Mkuu, Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Waziri hasa katika suala zima la hoja yangu, mimi ndio ambaye nilijaribu kumtaka Mhe. Waziri kuwa lini atatuletea sheria na hili nililifanya kwa makusudi, kwa sababu ninaelewa ninachokifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengi ya Muungano sio ya mafuta tu. Mhe. Mwenyekiti, bandari ni suala la Muungano. Zanzibar imeanzisha Shirika la Bandari na Shirika la Bandari halikuanzishwa isipokuwa ililetwa sheria Barazani. Ndio maana Wazanzibari pamoja na wananchi wangu wa Kwamtipura wanajiuliza kwa nini serikali ilifanya maamuzi magumu ya kuleta sheria ya kuanzisha Shirika la Bandari, sasa hivi serikali ishindwe kufuata maamuzi magumu ya kuanzisha Mamlaka ya Mafuta hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana mimi hoja yangu ikawa bado maelezo yote waliotoa Waheshimiwa Mawaziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ndio maana nikawa bado sijapata uelewa mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, tunapozuwia vifungu hatukusudii kuwa sisi ni wakaidi, tunataka tupate ufafanuzi ili tujuwe hizi faida za sheria zetu.

Lakini kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa tunaapa kwa katiba mbili na Mhe. Waziri kakubali. Kwa hivyo, ina maana hii katiba moja inatupeleka katika maendeleo na hii katiba moja inaturudisha nyuma ndio maana haya maswali yanakuwa magumu na ndio maana tukamtaka Mhe. Waziri na yeye aweze kuwa na maamuzi magumu.

Mhe. Mwenyekiti, Mshauri Mwelekezi ambaye alitafutwa na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika suala zima la Uchimbaji wa mafuta. Yeye alipopewa ile kazi alitaka kuangalia katiba zote mbili na wale aliwalazimisha, akawaambia aah! Mbona kwa mujibu wa katiba hili suala ni la mashirikiano pamoja na Zanzibar, mbona Zanzibar hapa hatuoni maoni yao. Akaambiwa aah! Wewe katiba ya Zanzibar achana nayo, kwa sababu katiba ya Zanzibar mambo yake ya Zanzibar hayahusu mambo ya Muungano. Hata hivyo, alilazimisha akasema mimi kwa kazi hii siwezi kuifanya, mpaka niiangalie na

katiba ya Zanzibar. Wakamruhusu kuja hapa, akatufanyia semina. Hapa alituambia kwamba mimi suala hili bila ya kuangalia katiba zote mbili siwezi kulifanya. Tukampigia makofi makubwa sana pale Baraza la Wawakilishi la Zamani.

Sasa mimi ndio maana nikaja na ile *document* niliyotoa kwenye mtandao ambayo inamuonesha Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano anakwenda kuzindua meli ya kuja kuchimba mafuta. Je, kama sisi tunaogopa kufanya maamuzi magumu, hao wenzetu ujasiri huo wameupata wapi wa kufanya maamuzi magumu na hayo mafuta watayachimba kwa sheria ipi. Sisi ina maana tunaogopa kuishitaki Jamhuri ya Muungano, sisi tuogope kushtakiwa. Mhe. Waziri tunataka maelezo ya kina ili tuweze kujiridhisha na Wazanzibari katika hoja hii ya kuletewa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bado kwa uoni wangu mfupi nahisi bado tufanye maamuzi magumu tulete hii sheria, halafu tuangalie kwa sababu unapoleta sheria sio kama ndio utaanza kuchimba. Unapoleta sheria, Mhe. Waziri namshukuru sana amefuata *process* nyingi sana, tena nakupongeza kweli kweli. Kumbe umeshaagiza mpaka *helicopter* ije itafute mafuta, nakupongeza kweli kweli kwa jitihada zako. Lakini haya yote kama hatujawa na sheria, hawa bado kazi hii watakujakuifanya vipi.
Mhe. Mwenyekiti, nikipata maelezo ya kuridhisha *Wallah* nitakuunga mkono kwa asilimia mia moja ahsante.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama tulivyotangulia kusema kuheshimu amasa, maslahi, uchungu alionao Mhe. Hamza Hassan Juma na Waheshimiwa Wajumbe wengine. Lakini nadhani kama ni maamuzi magumu, nitangulie kusema kwamba maamuzi magumu serikali ilikwishakufanya. Ilipoleta hoja ya kuliondoa jambo hili mbele ya Baraza hili katika orodha ya mambo ya Muungano, haijawahi kutokea kuletwa jambo lolote mbele ya Baraza hili kulitoa katika orodha ya mambo ya Muungano isipokuwa suala hili. Kwa hivyo, nadhani Mhe. Hamza Hassa atakubali kwamba huo ulikuwa ni uwamuzi mgumu.

Lakini la pili, Mhe. Shamuhuna hana uwezo wa kuleta mswada mbele ya Baraza hili. Mwenye uwezo wa kuleta mswada mbele ya Baraza hili ni serikali au Baraza la Mapinduzi limuidhinishe Mhe. Shamuhuna. Baraza la Mapinduzi au serikali italeta mswada mbele ya Baraza hili kuhusu suala hili, baada ya kujirishisha kuwa sheria hiyo itakayoletwa hapa itaweza kufanya kazi kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma, tulipitisha sheria ya bandari na tulipitisha sheria ya Takwimu, lakini hakuna hoja iliyoletwa mbele ya Baraza hili kuyaondoa

mambo hayo katika orodha ya mambo ya Muungano. Sasa tujiulize kwa nini hili tukaamua tulilete mbele ya Baraza na sio la takwimu na sio la bandari, ni kwa sababu ya unyeti wa suala hili na ni kwa sababu ya ushauri huo ambao yeye mwenyewe Mhe. Hamza anakiri kwamba serikali ilitafuta washauri elekezi.

Sasa ni kwa kuzingatia yote hayo ndio maana tunasema kwamba ukifika wakati wake mswada utakuja mbele ya Baraza hili na serikali sio kuwa imekaa kimpya, maandalizi inafanya. Lakini kumtaka Mhe. Shamuhuna aseme kuwa lini atauleta mswada mbele ya Baraza hili, nadhani itakuwa sio sahihi kwa kweli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana yeye Mhe. Hamza na wawakilishi wengine na wananchi wote wa Zanzibar wakubali kwamba serikali ina ya dhati katika suala hili na haijanyamaza inaendelea kufanya matayarisho na maandalizi na utakapofika wakati muafaka mswada huo utakuja mbele ya Baraza la Mapinduzi. Lakini wakati huu tunajua kwamba hata tukileta mswada huu mbele ya Baraza hili na ukapitishwa, basi tunajua haitokuwa kwa manufaa ya Zanzibar, haitokuwa kwa manufaa ya wananchi na haitomsaidia Mhe. Hamza na haitomsaidia mtu yeyote kwa kweli. Namuomba Mhe. Hamza Hassa atuamini kwamba nia ya dhati tunayo ya kulitekeleza suala hili na tumo katika maandalizi ya kulitekeleza.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mwanasheria wetu Mkuu na mimi nadhani sio Mwanasheria Mkuu tu peke yake. Lakini pia ni *professor* wa Kiswahili, kwa mifano mingi aliyotutolea na anayoitoa katika vikao mbali mbali. Inakufanya mtu kama uko mbali kufahamu basi lazima utafahamu. Sasa nilikuwa nataka atusaidie jambo moja. Katika hoja yangu na ndio maana nikaja na kumbukumbu ya *document*. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wamo katika utafiti wa uchimbaji wa mafuta na hili ni suala la Muungano. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hizi semina mnazotupatia zinatusaidia sana, kwa sababu yule Mshauri Mwelekezi yeye alikataa sana akasema hii kazi siifanyi bila ya kwenda Zanzibar ili nipate katiba mbili mbona zinagongana.

Sasa je, hawa wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile meli ambayo ni ya gharama kubwa inayotengenezwa, ingawa haito igharimu Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu kwa mujibu wa mtandao unasema nafikiri Brazil ndio wataweza ku-*sponsor* utaratibu huu. Wao wana uhalali gani wa kuja kufanya huu utafiti wakati hatuna mashirikiano baina ya pande mbili. Mimi nilikuwa nataka nijuwe labda Mhe. Waziri wetu wa nishati anashirikishwa vipi katika masuala haya ya utafutaji na uchimbaji wa haya mafuta. Lakini vile vile kuna na gesi imeshafanyiwa utafiti hajashirikishwa

hata kidogo. Ndio maana nikasema sisi tunachelea sana sheria, lakini hawa wenzetu hii mamlaka ya kufanya mambo hayo yote bila ya ridhaa yetu Zanzibar wao wanaipata wapi.

Mhe. Mwenyekiti, najua katiba itakuja. Mhe. Mwenyekiti, katiba itakuja na hatujajua katika katiba itakuwa vipi, kwa sababu Zanzibar tuko milioni 1,300,000 na wenzetu Bara wako milioni 46,000,000 maamuzi ya ile katiba mpya yatakuja kwa kura za maoni. Je, tutakuwa na nafasi gani watu milioni 1,300,000 katika watu milioni 46,000,000 ndipo hapa mimi ninapochelea kwamba tunasema tusuburi Katiba mpya, matokeo yake Katiba mpya ikaja ikarudi suala hili likalazimika kuwa la Muungano. Sasa hapo je Serikali ya Zanzibar itafanya maamuzi magumu au itaendelea kuendelea *hewallah* bwana kwa kuwa Katiba inasema, kwa sababu tumeshatoa na tukeshatoa hatutii tena. Mhe. Mwenyekiti, tunataka maelezo. *(Makofi)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, ninamshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma, maana raha ukiwa na wasi wasi useme hapala ndipo na yeye ameusema wasi wasi wake na ninajua wako wengine pengine wanao wasi wasi kama wa kwake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kusema kwamba mashirikiano si ya Muungano tu, wakati mwengine hata ndoa pia ni mashirikiano, lakini wakati mwengine ukeshafunga ndoa ndio unajua kwamba hapa nimekosea. Kwa hivyo, niseme kwamba utafiti unaofanywa na Serikali ya Muungano, gesi iliyogunduliwa. Kwa kweli jambo la msingi kwanza tukubali kwamba chochote kinachopatikana katika mafuta na gesi asilia, mpaka hivi sasa lilivyokuwa jambo hili ni la Muungano basi ni cha kwetu pamoja, yaani chochote kinachopatikana kama gesi asilia.

Mhe. Mwenyekiti kuna mengi naomba nimfahamishe Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu, kwa kweli yako mengi katika mafao ya Muungano, ambayo tunastahiki tuyapate. Kwa mfano, kuna mapato yanayotokana na *TIKRA*, *TCRA* na mengine mengi na ndio maana ikaundwa Tume ya Pamoja ya Fedha, kwa ajili ya kuyachunguza yote hayo na kuleta taarifa kwa serikali mbili kwamba kila mmoja anastahiki kiasi gani, ili kuondoa tatizo hili kuanzishwa kwa *GFA* na ripoti hizo zimefanyiwa kazi na zipo serikalini zinasubiri maamuzi.

Kwa hivyo, siku yoyote hayo yaliyopatikana pamoja, Mhe. Mwenyekiti naomba nimhakikishie kwamba mimi ni Mjumbe wa Tume ya Pamoja ya Fedha na moja linalofanyiwa kazi ni hiyo Ripoti ya Madeni baina ya serikali hizi mbili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wiki mbili zilizopita tumejadili na hayo tunayosema ya gesi na mambo mengine, basi inayopatikana mpaka sasa Zanzibar iko *share* yake na hata kama mtu hataki au hakubali na hiyo ni haki yetu na tunayo haki ya kudai popote.

Kwa hivyo, suala la ushirikishwaji wa Serikali ya Zanzibar katika utafiti, mimi nasema ushirikishwaji unakwenda kwa misingi ile ile ambayo suala hili zima la Muungano lina matatizo yake. Kwa kweli matatizo yapo, lakini tunasema kwamba matatizo hayo hatutoyatatua kwa kusema kuwa unaleta sheria hivi sasa mbele ya Baraza bila ya kukubaliana hiyo misingi ya kuleta hiyo sheria ya kuyakamilisha ambayo yanayohitaji kuleta sheria kwenye suala hili.

Sasa ninachomuomba Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba kama wasi wasi wetu ni kile wenzetu wanachokipata cha Muungano ni kweli na mimi naomba kuwathibitishia yako mafao mengi ambayo tunapaswa tuyapate na utaratibu wake upo na serikali inayasimamia katika kuyadai.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili la mswada wa mafuta serikali inafanya maandalizi kama nilivyotangulia kusema na itakapofika wakati, basi mswada huo utakuja na utakuja katika wakati ambao utakuwa ni muafaka, yaani utakuwa na manufaa.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala hili labda nimtoe wasi wasi hoja yake nyengine kuhusu suala la Kura ya Maoni itakayokuja. Kwa kweli tulipewa kazi pia ya kulisimamia jambo hili, lakini moja katika msingi sisi tunachosema na tunalolisimamia na kukubaliana na wenzetu, basi Kura ya Maoni itakapokuja itapigwa kwa hesabu ya Bara na hesabu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Baraza la Kutunga hiyo Katiba yenyewe ni jambo moja ambalo ndio maana haya mazungumzo yakachukua siku nyingi na wenzetu, kwa sababu ni jambo moja ambalo tunalisimamia kwamba ni lazima kuwa na Sauti ya Zanzibar *two-third majority* na Sauti ya Tanzania Bara *two-third majority*, kwa sababu sisi hatuwezi kuruhusu hatima yetu ikawa mikononi mwa wenzetu na wala hatutaki hatima yao iwe mikononi mwetu. Kwa hivyo, kila mtu achukue kile anachokipenda na wala asilazimishwe na wala asiamuliwe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mhe. Mjumbe pamoja na Baraza lako tukufu, kwamba huu utaratibu wala usimpe shida na *Inshaallah* tutakapokuja baada ya kukamilisha huo mswada atauona jinsi gani wananchi wa Zanzibar watakuwa na kauli katika kuamua hatima yao kwenye Muungano, yaani imo mikononi mwao. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwa uzoefu nilionao muda mrefu Barazani nimepata kuchomekea suala langu, kwa sababu sikuweza kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Utawala Bora katika Kura ya Maoni na ameweza kunijibu Mhe. Mwanasheria Mkuu. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ili niweze kukaa kitako tuendelee na utaratibu, bado Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo leo simuoni, kwa sababu bado kwa mujibu wa Katiba tulizoapa hapa ndani, kuna mapato yetu ambayo tunapaswa tuyapate kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado mpaka leo hayapatikani.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kutoa indhari na ninawambo Waheshimiwa Wabunge kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wale tuliowachagua hapa Barazani pamoja na Wabunge wote wa Zanzibar itakapokuja Bajeti ya Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waikatae katakata, kwa sababu inadhumu mapato ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kwa kweli nilikuwa mtu wa mwanzo kuchangia baada ya Mwenyekiti wa Kamati, kwa hiyo nashukuru na mimi ndiye niliyesema natoa shilingi 100 katika Fungu hili la Idara ya Nishati. Lakini baada ya maelezo mazuri sana niliyoyapata, nakubali sasa kurudisha shilingi 80 bado 20. *(Kicheko/Makofi)*

Katika suala hili Mhe. Mwenyekiti, inaonekana Baraza lako lina misimamo miwili, kwa sababu katika hoja tuliyoichangia Baraza kongwe kuhusu hoja hii ya mafuta, tulizungumza na tukaikabidhi serikali jukumu la kwenda kulitoa suala hili katika mambo ya Muungano na taarifa tuliyopata kwamba Mhe. Waziri Kiongozi alifanyakazi hiyo.

Lakini Baraza hili Mhe. Mwenyekiti, linajuilishwa kwamba sasa kuna azimio jengine ya kulisubiria suala hili katika mchakato wa Katiba mpya. Sasa hiyo ni misimamo miwili tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima pamoja na utukufu wa chombo hiki, basi ilikuwa kwanza tupate taarifa ya hatua gani suala hili limefikiwa katika kutolewa kwenye Orodha ya Mambo ya Muungano kabla ya kwenda katika suala hili. Kwa kweli suala hilo ni muhimu kwa sababu kuwa Wazanzibari kadiri tunachokifanya, basi Wazanzibari pamoja na Baraza hili tuweze kujua nini kinachoendelea na hilo lina tafsiri pana katika nia ya wenzetu kwenye suala hili.

Kwa hivyo, nilitaka hapa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atuelezee lile agizo tulilompa na serikali ikachukua hatua. Je, suala lile limefikia hatua gani.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo katika suala la maandalizi. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wengi tumekubaliana kwamba kuelekea kwenye suala hili maandalizi ni kitu cha msingi sana. Kwa hivyo, katika Baraza lililopita tuliambiwa kwamba kuna Wazanzibari 10 tumewapeleka nje ya nchi na hata sisi Wawakilishi lilituhusu kwa sababu tulipewa agizo tuwahamasishe wanachi wetu majimboni.

Sasa tunataka kujua agizo lile lililotolewa na serikali kwamba kuna Wazanzibari 10 ambao wako nje ya nchi kuhusiana na hili kwa ajili ya kujitayarisha. Je, ukweli wenyewe ni upi.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri, taarifa kuhusu jambo hili maagizo yale yamefikia wapi na matayarisho kuhusu vijana kwenda kusoma.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, mtu mzuri wa kutoa taarifa hii ambayo ingekuwa *more authentic*, yaani yenye uzito zaidi ni swahibu yangu Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa sababu yeye alikuwa Waziri katika Ofisi ya Waziri Kiongozi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyozungumza pale nilisema Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Mhe. Mohammed Seif Khatib ndio waliokuwa wamebebeshwa hili jukumu la kuratibu hizi shughuli za viongozi wawili, yaani Waziri Kiongozi pamoja na Waziri Mkuu. Hata hivyo, kwa kuwa mimi ni mserikali basi natoa taarifa kwa sababu naijua.

Mhe. Mwenyekiti, mazungumzo kati ya Waziri Kiongozi na Waziri Mkuu kama kawaida yalipelekwa tena kwa maandishi matakwa ya Zanzibar, lakini yakalala sana na wala hayakujibiwa. Katika kikao chengine kilichofanywa Bwawani nilisimama kuliuliza suala hili, niliambiwa nikae kitako liko nje ya *agenda* na nililazimika nikae kitako.

Lakini najua kwamba limefika wapi saula hili, kwa kweli limekwama na ndio maana katika uongozi huu wa hivi sasa Makamu wa Pili wa Rais ameshakwenda kuzungumza na Waziri Mkuu, yaani amezungumzia suala hili tena na taarifa aliyopewa ni kwamba suala hili sasa kwa sababu liko kwa rais, sisi tena si wazungumzaji wa suala hili na tumuachie rais atupe maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti, maelekezo ya rais kwa juu juu nilivyoyapata mimi, yaani alisema Makamu wa Pili wa Rais ni kwamba suala hili Wazanzibari wasifanye haraka, kinachokuja hivi sasa ni wakati mzuri wa kulizungumza, kwa sababu tunakuja kurekebisha Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, Katiba si hoja nyengine, isipokuwa ni ushauri aliotoa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwamba suala hili litazungumzwa wakati huo, lakini bado kama sisi hatutaki kulizungumza wakati huo, basi tunao uwezo wa kupeleka *agenda* yetu katika Kikao cha Oktoba cha Bunge na likikubaliwa, basi linaweza kuzungumzwa katika Bunge.

Suala la pili ni kuhusu Wazanzibari 10. Mhe. Mwenyekiti, ulichokiandaa wewe Mwenyezi Mungu anakibadilisha kati ya Wazanzibari 10 tumeweza kumpeleka 1. Kwa hivyo, mikataba kati yetu sisi na *Ras-el-Khaima* katika suala hili bado haijakaa sawa.

Kwa hivyo, kwa taarifa ya Baraza hili tumedhamiri mwaka huu tupeleke watu 6, wawili tutawapeleka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam wakasome *Geology* ambayo ni chanzo cha kusomea mambo ya mafuta na wengine watatu watakwenda kusomea hasa mambo ya mafuta kwa *Second Degree*.

Kwa maana hiyo, tutapeleka watu 6 kwa mwaka huu na tunasubiri hiyo ahadi tuliyoahidiwa ya kupeleka watu 10, kwa sababu watu 10 bado wapo na tunashindwa kuwapeleka kwani mikataba bado haijakaa sawa.

Kwa mfano, huyu mtu mmoja tuliyempeleka amerudi kuja kufanya *research*, hakupewa fedha za kufanyia *research* na hizo fedha ziko kwenye mikataba. Kutokana na hali hiyo, sasa tunalazimika kuzitafuta kwa hali na mali tumpe shilingi milioni 5 au 6 kwa ajili ya kufanya *research* yake na baadaye arudi akafanye *dissertation* huko *UAE*. Kwa hiyo, hiyo ndio hali ya msimamo ulivyo mpaka hivi sasa, kwa sababu nia ya kupeleka tunayo na tutapeleka watu 6 mwaka huu.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa hilo. Lakini kama tulimsikia Mhe. Mansoor Yussuf Himid na sera, kwa mujibu wa sera tuliyoipitisha katika Baraza lako, tulikubaliana au sera ilikubali, kwamba katika suala hili la mafuta, basi chochote kitakachohusiana na mambo haya kuhusu mikataba, basi mikataba iletwe mbele ya Baraza hili, ili tuweze kui- *approve* mbele ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye *cover page* upande wa ndani ya kitabu cha hotuba ya wizara yake kuna picha ya Mhe. Ali Juma Shamuhuna amekaa na Mwarabu

sijui nani wakisaini mkataba na sijui mkataba unaohusiana na kitu gani. Sasa mbona taarifa hii hajaileta kwenye Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, sijasaini mkataba na kampuni yoyote. Kwanza sina mamlaka ya kusaini mkataba mpata nipate ushauri wa Mhe. Mwanasheria Mkuu, isipokuwa tulichosaini sisi ni *Memorandum of Understanding* ya Uchimbaji wa Mafuta na wala sio Mkataba wa Kusomesha Wanafunzi.

Kwa hivyo, *Memorandum of Understanding* si mkataba ni makubaliano ya jumla jumla ya utekelezaji na ndio maana nikaja nikazungumza ile ratiba tunayoizungumza hapa ya kuanza hivi sasa mpaka tukachimba mafuta, hivyo sikusaini mkataba na wala sitosaini mkataba bila ya kibali cha Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti, sisi si wanasheria, lakini kwa mimi ninavyofahamu *Memorandum of Understanding* ni mkataba, labda Mhe. Mwanasheria Mkuu atupe ufafanuzi katika suala hili.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, najua Mhe. Omar Ali Shehe hakukusudia turudi darasani. Lakini kwenye mkataba kitu kimoja cha msingi ambacho kitaufanya mkataba uwe halali ni kitu kinachoitwa consideration, yaani malipo. Hivyo, *Memorandum of Understanding* kwa kawaida haina malipo, yaani haina *give* na *take*. *(Makofi)*

Kwa kweli ni kitu ambacho mnasema tumezungumza vizuri na tumekubaliana, kwa hivyo tuweke *record* ya yale tuliyokubalina tutayatekelezaji na kwa kawaida *Memorandum of Understanding* ndio maana hufuatiwa na mkataba, kwa hivyo kisheria si mkataba, kwa sababu huwezi kwenda Mahakamani kui-*force Memorandum of Understanding*. *(Makofi)*

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika. *(Makofi)*

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0801 | Idara ya Nishati | 122,928,000/= |
| Kifungu 0901 | Idara ya Ardhi na Usajili | |

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru baada ya jitihada za mara nne na kunipa hii mara ya tano. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia hapa nilijenga hofu kwamba serikali inaweza kuingia hasara kubwa kwa ufutaji wa vibali na mikataba bila ya utaratibu, pia nilisema kwamba kwenye Idara ya Ardhi kuna matatizo makubwa ya ufutaji ovyo wa mikataba. Lakini Mhe. Waziri hakufika kutoa maelezo juu ya hoja hiyo kwa sababu ya muda.

Kwa hivyo, nilimwambia kwamba kuna mikataba ambayo imetolewa ambapo yeye mwenyewe binafsi ameifuta, bila ya shaka kwa kuzingatia Sheria ya Nam. 12 ya mwaka 1992. Lakini tukiangalia mikataba hii bado haijatimia muda wa kufutwa kwa maana ya miezi 30 kwa mujiu a sheria. Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anitoe hofu yangu.

Vile vile nilimwambia kwamba kuna haja ya Baraza kuunda tume kwa ajili ya kumsaidia, ili kugundua matatizo ya ardhi kwa Unguja na Pemba, kwa sababu kila siku hali hii inaongezeka. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anipe ufufanuzi.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakubalina na wazo lake la kuunda tume, ili kuangalia matatizo ya ardhi. Kwa hivyo, nitalazima kufanya hivyo kwa sababu matatizo ya ardhi ni mengi na yanahitaji kushughulikiwa. Kwa kweli mimi pamoja na wasaidizi wangu hatuwezi, yaani tumefika pahala lazima tutafute msaada na hivyo nalikubali kabisa wazo lake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kufutwa kwa mkataba ambao haujatimia miezi 30. Kwa kweli sina hakina, hivyo naomba anikumbushe, ili niweze kukiri kwamba ndio au sio. Lakini sikumbuki kwamba kuna mkataba ambao tumeufuta kabla ya kutimia miezi 30.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mhe. Waziri kukubali kuunda tume na bila ya shaka itakuwa kazi yako sasa. Lakini kuhusu mkataba na kwa kuzingatia muda uliopo, kwa sababu *copy* ninazo hapa ambazo zina jina lake pamoja na saini yake na inawezekana jina limebuniwa pamoja na saini.

Kwa hivyo, baadaye nitamtafuta na kuweza kumpa hiyo *copy*, ili aniambie ni saini yake halali au ni saini iliyobuniwa kwa niaba yake. Kwa maana hiyo, naomba hili anipokee na baadaye tutafanya mawasiliano zaidi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, labda tungepata ufafanuzi mzuri, maana imetajwa kitu tume ambayo kwa kawaida hapa Baraza huwa tunaita Kamati Teule. Sasa Mhe. Waziri ni tume ipi uliyokubali kwamba itatayarishwa.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, tume hii itaundwa nje ya Bazara hili lakini ndani ya wizara na wala haitoundwa ndani ya Baraza. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Hija Hassan Hija ndivyo alivyokusudia. *(Makofi)*

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana tukiangalia hoja yangu nilisema hivi, kwamba huwezi kumpa jukumu Mkurugenzi wa Idara

fulani akaharibu na baadaye ukamwambia yeye aunde tume kwa ajili ya kuhalalisha. Kwa hivyo, ninachokitaka kwamba Baraza liunde tume kama ni tume ya wizara, basi haina haja, kwa sababu tume ninayoitaka mimi ni ya Baraza ili inisaidie kazi kwa ajili ya kupeleka maovu ya wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama msimamo wake ni tume ya wizara basi haina haja ya kuharibu fedha za umma na haja yangu ni tume ya Baraza, ili tumsaidie kwamba kuna uovu unafanywa kwa niaba ya wananchi wa Unguja na Pemba. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri anayesimamia masuala ya ardhi ni kwamba tatizo la migogoro ya ardhi ni kubwa. Hivi sasa wizara hiyo husika inatengeneza waraka maalum kwa ajili ya kuwasilisha serikalini kuhusu namna ya kutafuta utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Kwa hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wavute subira, wakisubiri waraka ambao utawasilisha katika Baraza la Mapinduzi kutoka Wizara husika ya Ardhi, ili lizungumzwe na baadaye serikali itatoa ufafanuzi mzuri wa namna ya kushughulikia migogoro hiyo ya ardhi.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba serikali haitaki kuunda Tume ya Baraza. Kwa hivyo, hakuna haja ya kuunda tume nyengine yoyote kuharibu fedha za umma, kwa sababu serikali inaona hakuna haja Baraza kuchunguza kama wajibu wetu wa Katiba, basi tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, nadhani serikali iendelee na utaratibu wake wa kupata ufafanuzi juu ya hili na mkiona inafaa, basi nafikiri mnaweza kuleta taarifa Barazani. Sasa baada ya hapo tutajua kwamba tunaweza kutengeneza Kamati Teule au vyenginevyo. *(Makofi)*

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu jana wakati nilipokuwa nikichangia nilizungumzia juu ya suala la uvamizi wa ardhi katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii Maruhubi, pia nilielezea namna gani tulifikia hatua mpaka ya kutoka na Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa ajili ya kwenda kuangalia lile eneo la uvamizi na tukaona kwamba uvamizi umefanyika pale.
Mhe. Mwenyekiti, wakati suala hili lilikuja katika swali langu la msingi kuwa eneo lile limevamiwa, lakini Mhe. Naibu Waziri alijibu kwamba eneo halikuvamiwa. Vile vile baadaye Mhe. Asha Bakari Makame akatoa hoja tena kuwa lile eneo limevamia, kwa sababu tulikwenda kulikagua na tukaona uvamizi upo.

Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anipe maelezo juu ya uvamizi ule. Kwa hivyo, wizara imechukua hatua gani mpaka hivi sasa juu ya uvamizi ule, kwa sababu mtu yule ameshaandikiwa barua mara nyingi na bado hajatekeleza yale maagizo ya wizara kuhusiana na zile barua ambazo ameandikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua zile hatua ambazo zimechukuliwa na wizara juu ya uvamizi ule?

Vile vile ni hatua gani wizara imechukua kwa wale maafisa wake, ambao waliwatuma kazi kwenda kuangalia na kutoa jawabu kwamba hakuna uvamizi, kiasi cha kwamba wakaja wakamsababishia Mhe. Naibu Waziri kusema uongo katika Baraza. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, anipatie maelezo kuhusiana na suala hili.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, ninayo barua hii hapa ambayo niliyomuandikia bwana Khalifa Salum Suleiman, ambaye alikuwa analitumia eneo lile bila ya utaratibu.

Lakini kwa kuelewana na Mwalimu Mkuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Utalii Maruhubi. Kwa kweli ujumbe ulikwenda kwa ajili ya kwenda kuangalia na tuligundua kwamba kweli kuna *element* ya uvamizi. Kwa maana hiyo, ndipo alipoandikiwa barua hii ya kusitisha barua uvamizi, yaani asitishe kufanya jambo lolote mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, hatua nyengine zitafuata baada ya kuangalia tathmini ya uvamizi ule umegharimu kiasi gani na kadhalika au amesikiliza agizo letu ama hakusikiliza. Sasa hapa ndipo hatua nyengine zitachukuliwa na ikilazimika hatua za kisheria zichukuliwe basi zitachukuliwa. Lakini hatua tuliyochukua kwa kuanzia ni hii na pia juzi nimewatuma watu wangu, kwa ajili ya kwenda kuangalia na wala hakuna harakati yoyote inayoendelea hivi sasa pale pahala.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yake Mhe. Waziri hakujibu kile ambacho mimi nimeuliza, yaani anazunguka kidogo. Kwa kweli nilichouliza mimi kwa sababu sisi tumekwenda pale na hizo hatua anazozisema kwamba amesitisha si kweli, kwa sababu hiyo siku tuliyokwenda sisi ndio kwanza mawe nayamwagwa, kwa ajili ya kuendelea na hatua za ujenzi katika maeneo yale ya kule na ushahidi mzuri Mhe. Naibu Waziri tuliokwenda naye yeye anajua hilo, nafikiri Mhe. Waziri yeye atakuwa amepewa taarifa ambazo si sahihi sana.

Lakini nimetaka kujua hatua ambazo zimechukuliwa kwa wale wambao wametoa taarifa ambazo si sahihi na kuletwa hapa Barazani hapa. Mhe.

Mwenyekiti, swali langu la msingi ni kusema kuwa eneo lile limevamiwa, lakini Mhe. Naibu Waziri wakati alipokuwa akijibu swali la msingi hapa alisema kwamba si kweli kuwa eneo lile limevamiwa, yaani halikuvamiwa.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana Mhe. Asha Bakari Makame (Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari) alinyanyuka kwa sababu lile suala analifahamu. Kwa hivyo, tulipomaliza basi tulikwenda kukagua pale. Kwa hiyo, nataka hatua zilizochukuliwa kwa wale maofisa walimsababishia Mhe. Waziri aseme uongo katika Baraza hapa, sasa ni hatua gani zimechukuliwa na wizara juu ya maofisa wale. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, sijui Mhe. Mjumbe alitaka tuchukue hatua gani zaidi ya hii ya hatua ya awali. Kwa hivyo, nasema tumekubali kwamba eneo kula *element* ya kuvamiwa, kwa sababu kuna *structure* imebadilika pale. Lakini kwa mtazamo wa maofisa wetu wa mazingira wanasema mabadiliko yale hayana dhara.

Sasa kama ni kuchukua hatua nyengine kwa wale waliosema uongo, basi kuna mambo mengi ambayo uyafuatilie kwanza. Kwa mfano, ikiwa ni kumfukuza kazi mtu, basi huwezi kumfukuza kazi kwa kumvamia tu mpaka utafute *facts* zote na uridhike kwamba huyu alidanganya na amefanya makosa na hapo ndipo tutamuadhibu. Lakini hatua ya kwanza ndio hii tuliyoichukua ya kusimamisha haraka zozote pale pahala.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri bado hajanifahamu. Mhe. Mwenyekiti, ninachokizungumzia ni kuhusu lile suala la yule mwekezaji, kwamba yule mwekezaji amevamia eneo la chuo cha Utalii ndio suala langu la msingi lililokuwa hapa, jawabu alilopewa waziri ambalo alilisoma Naibu Waziri hapa ni kwamba hapakuvamiwa hakuna kitu hicho, ina maana kwamba kama si zile jitihada zetu za kusema twende tukaangalie tusingejua kama pamevamiwa ina maana kapewa jawabu la uongo, sisahihi jawabu ambalo kuwa alipewa ndicho ninachouliza wale ambao walikuwa wametayarisha yale majibu wakampa yeye Mhe. Waziri kuja kutoa jawabu lile hapa katika Baraza ni hatua gani zilichukuliwa. Achana na ule uvamizi uvamizi upo kwa sababu tumekwenda mipaka ile kavuka kwake kande kwenye sehemu ya chuo.

Nataka kujua ni hatua gani Wizara imechukua juu ya maofisa wale?

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri labda utwambie kama hujachukua hatua utafanya nini.

**Mhe. Waziri wa Ardhi Maji, Makaazi na Nishati:** Hatukuchukua hatua yoyote kwa sasa hivi kwa sababu lazima tufanye *investigation* kwanza tuwe na hakika na hili kosa lilifanywa, ndio tunaweza kuchukua hatua, serikali hii jamani haiendeshwi kibabe akifanya kosa akafukuzwa kazi hatwendi hivyo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mhe. Waziri anasema suala hilo atalifanyia utafiti ili kabla hajasema kwamba achukue hatua gani za kinidhamu za kumfukuza mtu, lazima taratibu zote zichukuliwe na hao waliomuelekeza huko basi wapate nafasi kujitetea.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kutaka ufafanuzi wa utaratibu, Mhe. Mwenyekiti siku zote unatuwasa hapa tunalolizungumza hapa Barazani linatakiwa liwe limefanyiwa utafiti na la ukweli na hapa kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kwamba Naibu Waziri alipokuwa akijibu suala kwa sababu Mheshimiwa Mjumbe alisema kwamba eneo limevamiwa, Mhe. Naibu Waziri akasema eneo halikuvamiwa.

Kwa hivyo je, Mhe. Naibu Waziri anaweza kututhibitishia kwamba alilidanganya baraza?

**Mhe. Spika:** Hivi tunataka zaidi ya jibu alilotoa Mhe. Naibu Waziri kwamba kweli kumevamiwa, maana hiyo ameshajibu Mhe. Waziri pale, kweli kumevamiwa sasa tusende kwenye hoja nyengine. Hoja hatua gani itachukuliwa ambayo waziri ameshajibu, hii hoja nyengine kuwa kasema uwongo vipi waziri amesema kama ilikuwa hakukuvamiwa waziri amesema kumevamiwa baada ya uchunguzi tena kwa bahati nzuri na yeye mwenyewe kathibitisha.

Mimi nadhani tuendelee kwa hapa.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0901 | Idara ya Ardhi na Usajili | 282,454,000 |
| Kifungu 1001 | Idara ya Upimaji na Ramani | 295,100,000 |
| Kifungu 1101 | Idara ya Nyumba na makaazi | |

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa vile sikubahatika kuchangiakwa maneno lakini nilichangia kwa maandishi na nilimuuliza Mhe. Waziri kuhusu haari ya nyumba za majenzi Kengeja, ambazo nyumba zile zimekaa kama chaka la wachawi sasa hivi. Je, Mhe. Waziri anazifikiriaje nyumba zile.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti nilipokuwa nafanya majumuisho nimeonyesha kitabu hiki na kuna mtu

nikamuahidi nitampa na nitampa kweli baada ya siku ya pili anirejeshee. Baada ya kupata kauli katika Baraza hili kamba hali za nyumba ni mbaya sana hususan Kengeja niliwatuma watu wangu kwenda Kengeja akiwemo Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Nyumba, wamekwenda wamefanya kazi nzuri sana wamepiga mpaka picha za vyooni, darini n.k kuona jinsi nyumba zilivyoharibika hawakuishia hapo tu lakini wamefanya mpaka makisio ya kila eneo lililochunguzwa na jumla ya fedha zitakazohitajika ni milioni 665,712,000.

Kasema lini tutachukua hatua ya marekebisho haya kwa kweli ni vigumu kusema sasa hivi kwa sababu kama tufanye marekebisho haya yote itabidi tufanye *reallocation* katika vifungu mbali mbali, sasa bado tunaangalia mchakato kama tufanye nusu nusu kwa kuangalia pesa zilizokuwemo kwenye makisio sawa la kama tufanye *reallocation* ili tufanye kazi kwa haraka sawa, lakini nia tunayo kazi ya uchunguzi imeshaanza Mheshimiwa muwakilishi anistahamilie na anipe muda hii kazi itafanywa.

**Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti namshukuru Mhe. Waziri kwa kufuatilia michango hata ile ya maandishi kwa hivyo naomba tuendelee.

**Mhe. Hijja Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilihoji kuwa serikali walikubali kuwasaidia wananchi wa Mtoni baada ya kuvunjwa nyumba kwa makosa, nikaonyeshwa barua hapa za Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi kwamba serikali ilikubali kuwasaidia angalau kifuta machozi, sasa ni miaka mingi suala lile halijafanyika.

Sasa naomba Mhe. Waziri anisaidie wapi ambapo wamekwama ili wananchi wale kupata fidia angalau ya kifuta machozi.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mheshimiwa Mjumbe atakubaliana na mimi kwamba hili suala ni la muda mrefu kidogo na mimi alipochangia nilistaajabu kwamba wale watu waliovunjiwa nyumba zao bado hawajalipwa fidia, sitaki niseme lini watalipwa lakini kwa sababu suala ni la muda mrefu nitaarudi kwa wenzangu nitafute rekodi na maamuzi yaliyofikiwa. Halafu litakuja barazani kama hili ni letu tena au nimuandikie yeye ataridhika nitafanya hivyo.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, kwa busara za Mhe. Waziri naomba tuendelee na bila ya shaka nitamfuatilia ili anisaidie majibu.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe. Mwenyekiti wakati nachangia nilisema kwamba moja kati ya dhamira kubwa ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964

yaliyoletwa na Sheikh Abeid Amani Karume ilikuwa ni mapinduzi ya kuwapatia wananchi makaazi bora na kwa kweli alifanya kazi hiyo kubwa, lakini bahati mbaya serikali haikuweza kuendeleza vizuri makaazi bora.

Sasa nilitoa rai ambayo kwa serikali sikupata jibu kwamba inaonekana mfumo wa kiidara wa kuzimamia nyumba hizi na kuendeleza makazi mengine hauwezi kutufikisha pahala, nikaishauri Wizara kwa nini haifikirii kuanzisha Shirika ambalo litakuwa na mamlaka ya kuweza kujenga nyumba mpya na kuzisimamia zile zilizopo. Mhe. Mwenyekiti hili sikupata jawabu naomba sasa Mhe. Waziri anijibu.

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli alizungumza suala hili Mhe. Omar Ali Shehe lakini sikupata kulijibu kwa sababu ya muda sio vyenginevyo, napenda nimjibu kwamba naukubali ushauri wake na nitazungumza na wenzangu kuangalia hivi kuunda mamlaka itaondosha tatizo hili, hivi sasa tunaangalia namna ya kubadilisha kodi za nyumba hizi za serikali, tunaangalia vile vile namna ya kufanya marekebisho hii bodi ya kodi za nyumba. Sasa tutaliangalia na hili tutalifanya kwa haraka lile ambalo linahitaji lifanywe kwa haraka na baadae tutafanya kama italazimika tutaunda ile taasisi aliyoizungumza ya Mamlaka ya Nyumba badala ya shirika au idara ya Nyumba.

**Mhe. Omar Ali Shehe:** Mhe: Mhe. Mwenyekiti baada ya majibu hayo mazuri kabisa naamua kurejesha shilingi mia katika bajeti yake. Ahsante.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 1101 | Idara ya Nyumba na makaazi | 153,663,000 |
| Kifungu 1102 | Bodi ya kudhibiti kodi za nyumba | 30,000,000 |
| Kifungu 1201 | Mahakama ya Ardhi | 116,258,000 |
| Kifungu 1301 | Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 495,956,000 |
| Kifungu 1401 | Msajili wa Ardhi | 125,423,000 |
| Kifungu 1501 | Idara ya Mipango Miji | 106,800,000 |
| | **JUMLA YA FUNGU** | **5,029,960,000** |

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu 0401 | Idara ya Mipango sera na Utafiti | 101,938,689,000 |
| **JUMLA YA FUNGU** | | **101,938,689,000** |

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Makaazi na Nishati:** Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza likubali makisio hayo.

**Mhe. Waziri wa Afya:** Mhe. Spika, nakubali.

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa wajumbe niwahoji basi wale wanaokubaliana na Makadirio hayo ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Spika, kwanza nikupongeze sana kwa uwezo wako na busara zako umekuwa ikiweka sawa kwa Mawaziri na hata wa *back bencher* na hizo ndio busara zilizotufanya tukuchague kwa asilimia mia moja, sasa naomba busara yako itumike kwa kanuni 23 ambayo inaendesha nyakati za kikao, kwa sababu leo ni siku ya Wizara ya Mawasiliano wizara ambayo ni muhimu sana na kwa sababu Wizara iliyopita imechukua muda mrefu naomba tuweke kanuni kando leo utuahirishie mpaka kesho kwa ajili ya kujipanga. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe makofi nimeyasikia na kwa kweli tumefanya kazi kubwa sana na kumbe bwana fedha ya wananchi kuipata hivi hivi sio rahisi, mpaka wajumbe hawa walioletwa na wananchi wakubali itumike ni kazi kubwa. Tatizo letu ni moja tu muda kwa kweli tuko nyuma ya wakati sasa mimi nilifikiri kwamba angalau badi tungekuja tukasoma michango ikaanza kwa siku ya pili yaani kesho, lakini tukiendelea kuahirisha zaidi ratiba hii itakuwa ni tatizo kubwa. Kama nilivoeleza jana kwamba tatizo letu ni kwamba Mwezi wa Ramadhani tunakubaliana kwamba kwa kawaida kila moja hupendelea akafutari na familia yake, na ratiba hii iko taiti mpaka tarehe 31/7/2011 ambapo inawezekana ikawa tarehe 1/8/2011 ikawa tunaanza ramadhani.

Lakini halafu isitoshe zaidi ya hivyo kuna muda maalum wa kupitisha bajeti hii na karibu zile siku za kawaida ambazo zimepangwa tushazimaliza kwa muibu wa katiba hii na nadhani tumeshaongeza siku moja, sasa tunaweza kufika pahala taratibu zinatwambia kwamba inapofika pahala muda umekwisha sasa mpitishe mafungu tu bila ya mjadala, sasa hiyo nayo bila ya wananchi kupitisha hiyo nayo sio utaratibu mzuri.

Kwa hivyo mimi nadhani tukubaliane kwamba tuje jioni tuwasilishe na Mhe. Waziri namshukuru aliniomba amesafiri lakini amehakikisha kwamba amekuwepo tena tangu jana akitegemea kwamba leo asubuhi alikuwa awasilishe, lakini kwa bahati mbaya ikawa haikuwezekana kwa sababu tuko

nyuma ya wakati. Sasa niwaombe sana waheshimiwa wajumbe kwa kweli kazi tumefanya kubwa nawapongeza sana na nawashukuru sana waheshimiwa wajumbe kutumia haki yenu ya kuuliza vizuri sana, nashukuru mawaziri nao wamejitahidi kutoa maelezo mazuri na kwa mashirikiano hayo ya pamoja basi tumefikia hapa.

Naomba tena tushirikiane kwamba jioni tuje kama tulivyopanga lakini ratiba hii tukiendelea kuimega mega na hatujui Wizara zinazokuja huko zitakuwa na mapana kiasi gani tunaweza kufika pahala tukapitisha mafungu kiujumla ambayo nayo haitokuwa vizuri, haitokuwa tunafanya haki kwa sababu hatukuweza kujadili lolote.

Waheshimiwa Wajumbe mimi nasema tufanye hivyo na nafikiri mnenifahamu.

*(Saa 8.20 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

## HOTUBA YA WAZIRI WA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO MHE. HAMAD MASOUD HAMAD KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2011-2012.

**UTANGULIZI.**

**Mhe. Waziri wa Miundombino na Mawasiliano:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu hotuba ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, kwa jina la Mwenyenzi Mungu, Mwingi wa Rehema na Ukarimu, naomba idhini yako kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kazi za kawaida na za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu, alietuwezesha kukutana hapa leo hii tukiwa wazima na wenye afya njema. Aidha nachukuwa fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Muhammed Shein kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar wa awamu ya saba yenye mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kuchaguliwa kwake kuiongoza nchi hii ni ushahidi tosha wa mapenzi na imani waliyonayo wananchi kwake. Naamini kuwa kwa busara, uadilifu na hekima zake

ataliongoza Taifa hili kwa ustawi na mafanikio makubwa. Namshukuru sana Mhe. Rais kwa ujasiri wake wa kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa lengo la kuendeleza muafaka wa kuwaunganisha Wazanzibari wote na kuhakikisha utulivu na mshikamano wa kudumu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda nimpongeze Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Seif Sharif Hamad na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kwao kushika nyadhifa hizo katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kwa mashirikiano wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu ya kazi katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kadhalika nachukuwa nafasi hii kukupongeza wewe Mhe. Spika kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza lako Tukufu kwa busara, hekima na uadilifu.

Mhe. Spika, napenda nitumie fursa hii, kukishukuru kwa dhati chama changu cha *"The Civic United Front"* (CUF-Chama cha Wananchi) kwa uamuzi wake wa kunipendekeza kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuwa miongoni mwa Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba yenye mfumo wa umoja wa kitaifa.

Mhe. Spika, naomba nimshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuniteua na kunipa wadhifa wa kuiongoza Wizara hii. Aidha, ninamshukuru Mhe. Rais kwa dhamira yake ya kukuza na kuendeleza miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano katika miaka ijayo ili iweze kutoa mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamiii.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Anayeshughulikia Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yusuf Mzee kwa hotuba yake ya tarehe 15 Juni 2011 iliyotoa mwelekeo wa kuimarisha miundombinu, maelezo ya hali ya Uchumi, Mipango ya Maendeleo ya nchi yetu na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2011/2012. Kadhalika naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk, Mwakilishi wa Jimbo la Kitope kwa maelekezo na ushauri unaosaidia kufanikisha shughuli za Wizara. Aidha kwa kuzingatia kuwa hiki ni kikao cha kwanza baada ya uchaguzi wa mwaka uliopita, napenda nichukuwe nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kwa kushinda uchaguzi mkuu na kuingia katika Baraza hili wakiwa na ari na moyo wa kuwatumikia wananchi wao na nchi yetu kwa jumla.

Aidha nawashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa michango yao kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Ni mategemeo yangu kuwa watakuwa karibu na mimi ndani ya miaka ijayo kwa kunishauri, kunikosoa na kunielekeza ili niweze kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

Pia namshukuru Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Mheshimiwa Issa Haji Ussa (Gavu), Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka kwa mashirikiano mazuri ya utekelezaji wa kazi za kila siku. Vile vile nawapongeza Katibu Mkuu Dr. Vuai Iddi Lila, Naibu Katibu Mkuu Nd.Msanif Haji Mussa, Wakuu wa taasisi na watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kutekeleza vyema majukumu yao.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kuishukuru familia yangu kwa kuniunga mkono na kunipa moyo katika utekelezaji wa kazi zangu. Aidha nachukuwa fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wa jimbo la Ole kwa imani yao kwangu ya kunichagua kwa kura nyingi katika uchaguzi uliopita. Ni matarajio yangu kuwa watanipa mashirikiano mazuri ili niweze kutekeleza majukumu yangu ya kuwatumikia wao na Taifa la Zanzibar kwa jumla.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikadiriwa kutumia jumla Tzs.4,067,000,000 kwa kazi za kawaida na Tzs.9,100,000,000 kwa kazi za maendeleo. Aidha Wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs.1,653,500,000. Hadi Machi 2011 jumla ya Tzs. 2,832,506,410 ziliingizwa, sawa na asilimia 70 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Tzs.6,331,024,159 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 71. Aidha Wizara ilikusanya Tzs.1,337,079,791, sawa na asilimia 81. (kiambatanisho namba 1. kinaeleza)

## UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2010–2011 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2011-2012.

### Matukio Muhimu

Mhe. Spika, kabla sijaelezea utekelezaji wa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka wa fedha 2011/2012 naomba nieleze matukio muhimu yaliyojitokeza kwa mwaka 2010/2011 katika sekta mbalimbali za Usafirishaji na Mawasiliano. Miongoni mwa matukio hayo muhimu ni pamoja na:-

i) Ziara za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamo wa Pili wa Raisi katika ukaguzi wa barabara, bandari na viwanja vya ndege.

ii) Kukamilika kwa rasimu ya miswaada miwili ya sheria ambayo ni uwanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(Zanzibar*

*Airport Authority Act) na "Aerodrome Act"* rasimu ambazo hivi karibuni zitawasilishwa mbele ya Baraza lako Tukufu.

iii) Shirika la ndege la Oman kurejesha tena huduma zake za safari baina ya Oman na Zanzibar.

iv) Kuanza rasmi ujenzi wa jengo jipya la abiria katika kiwanja cha kimataifa cha Abeid Amani Karume kilichopo Unguja.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina majukumu ya kuendeleza miundombinu na utoaji huduma za usafiri na mawasiliano. Majukumu yake yamegawika katika sekta kuu nne, ambazo ni:-

- Usafiri wa nchi kavu,
- Usafiri wa anga,
- Usafiri wa baharini, na
- Mawasiliano.

Katika awamu iliyopita Wizara hii ilijulikana kama Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ilikuwa na taasisi saba, hata hivyo baada ya mabadiliko ya uongozi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba muundo wa Wizara umebadilika. Katika muundo mpya majukumu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano yamegawika katika taasisi zifuatazo:-

1. Ofisi Kuu Pemba.
2. Idara ya Mipango, Sera, na Utafiti.
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
4. Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.
5. Idara ya Usafiri na Leseni.
6. Idara ya Mawasiliano.
7. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.
8. Mamlaka ya Usafiri Baharini.
9. Shirika la Meli na Uwakala.
10. Shirika la Bandari.

**OFISI KUU PEMBA**

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba inaratibu na kusimamia kazi zote za kisekta za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa upande wa Pemba.

Katika kipindi cha 2010/2011 Ofisi kuu Pemba imetekeleza kazi za kawaida nazo zi maendeleo zikiwemo:

- Matengenezo ya barabara,

- Kusimamia miradi ya maendeleo,
- Kusimamia utoaji wa leseni na ukaguzi wa magari,
- Uimarishaji wa huduma katika kiwanja cha ndege cha Pemba,
- Kuelimisha wafanyakazi kwa kuwapatia haki zao za msingi wanazostahiki.

Utekelezaji wa majukumu yataelezwa zaidi katika maelezo ya sekta husika.

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilikadiriwa kutumia jumla ya Tzs.1,100,418,000 kwa kazi za kawaida na kukusanya jumla ya Tzs.90,500,000 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato. Hadi Machi 2011 fedha zilizoingizwa ni Tzs.781,762,390 sawa na asilimia 71 na ilikusanya jumla ya Tzs.69,366,905 sawa na asilimia 77.

**Malengo kwa Mwaka 2011-2012**

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2011/2012 inatarajia kutekeleza majukumu yake ya kazi za kawaida za kuratibu na kusimamia miradi mbali mbali.

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka 2011/2012 inakadiriwa kukusanya jumla ya Tzs. 98,980,000 na inaombewa jumla ya Tzs.1,065,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI**

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera na mipango ya sekta za usafiri na mawasiliano. Idara inaratibu kazi zote za maendeleo za Wizara zikiwemo kubuni, kutayarisha na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Idara pia ina jukumu la kubuni na kufanya tafiti za mabadiliko ya miundombinu na huduma za usafiri na mawasiliano. Ili kutekeleza shughuli za utafiti, idara inakusanya takwimu mbali mbali zinazohusiana na sekta ya usafiri na mawasiliano.

Mhe. Spika, Bajeti ya mwaka 2011/2012 inafuata muongozo wa bajeti ya serikali ambayo pamoja na mambo mengine, unasisitiza bajeti ziandaliwe kwa kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II) kwa kuzingatia hali halisi ya uwezo wa serikali, dira 2020 (*vision* 2020), hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa tarehe 11/11/2010 alipolihutubia Baraza lako Tukufu na maelekezo yake kwa Wizara alipokutana na uongozi wa wizara huko Ikulu mwezi Desemba 2010.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 wizara iliendelea na hatua za utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri wa Zanzibar *(Zanzibar Transport Master Plan)*. Mradi huu una lengo la kuufanyia mabadiliko mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa sekta ya usafiri kwa kutenganisha majukumu ya sera na mipango ya

muda mrefu na shughuli za udhibiti (*regulations*) kuwa chini ya mamlaka zitakazoundwa na shughuli za utoaji huduma zitafanywa kwa ushirikiano baina ya serikali na sekta binafsi. Katika kipindi hicho wizara imeanza na kukamilisha awamu ya kwanza ya marekebisho ya muundo wa kitaasisi. Awamu hii ilihusisha utayarishaji wa wazo la muundo wa wizara na kazi hiyo ilifanywa na kitengo maalum kilichowashirikisha wataalamu kutoka taasisi mbali mbali. Hivi sasa wizara inafanya mashauriano na wafadhili (Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika) juu ya utekelezaji wa awamu ya pili na ya tatu ya mradi.

Mhe. Spika, Wizara imo katika taratibu za kukamilisha mpango mkuu wa kiwanja cha Ndege *(Airport Master Plan)* na sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Aidha Wizara imekamilisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini kama sheria namb. 5 ya mwaka 2006 *(Maritime Transport Act no. 5 of 2006)* inavyoelekeza.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Idara ya Mipango na Sera (ikijumuisha Kitengo cha Mrajis wa Meli) ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs. 82,000,000 na kutumia jumla ya Tzs. 748,118,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi Machi 2011 jumla ya Tzs. 81,785,692 sawa na asilimia 99.7 ya mapato zimekusanywa. Fedha iliyoingizwa kwa kazi za kawaida katika kipindi cha Julai 2010 hadi Machi 2011 ni Tzs. 528,614,010 sawa na asilimia 71.

**Malengo kwa Mwaka 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa 2011/2012, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usafiri, na Mpango Mkuu wa Usafiri wa Zanzibar *(Zanzibar Transport Masterplan)*, kuratibu na kufuatilia miradi yote inayotekelezwa na wizara, utayarishaji wa sheria na kanuni mbali mbali za udhibiti wa sekta za usafiri. Idara itaandaa sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Barabara, Sheria ya uanzishwaji wa Shirika la Meli na Uwakala, kuandaa sera ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kuimarisha vitengo vyake vikiwemo vitengo vya Mipango na Utafiti.

Mhe. Spika, idara hii imepanga kuanzisha taratibu za uanzishwaji wa Vyuo maalum vya kufundisha wataalamu wa fani ya Ndege na fani ya Ubaharia *(Establishment of Zanzibar Civil Aviation Academy and Zanzibar Maritime Training Institute.)*

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya Tzs.150,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI**

Mhe. Spika, idara hii ina jukumu la kusimamia na kutathmini utekelezaji wa kazi za uendeshaji wa wizara na kushughulikia maslahi ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na matatizo na nidhamu kazini. Aidha husimamia na kuandaa mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi wa wizara.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010 /2011 idara imeweza kutekeleza na kusimamia masuala ya kiutumishi na uendeshaji kwa kushughulikia masuala yanayohusu wafanyakazi.

Kwa upande wa mafunzo jumla ya wafanyakazi 38 wamepatiwa mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa viwango tofauti (Kiambatanisho Nam.2). Vile vile wizara inaendelea na jitihada za kuwaelimisha wafanyakazi wake umuhimu wa kujikinga na maambukizo ya virusi vya UKIMWI.

**Malengo ya Mwaka 2011/2012**
Mhe. Spika, idara itaendelea kutekeleza masuala ya kiutumishi na uendeshaji kwa kuyashughulikia masuala yanayohusu wafanyakazi.

- Idara inakusudia kutayarisha mpango kazi wa wizara kwa wafanyakazi wake,
- Kuandaa mfumo wa utumishi *(Scheme of service)* wa wizara,
- Kupanga upya majukumu ya wafanyakazi *(Job description),*
- Kusimamia mpango wa mafunzo na kuajiri wafanyakazi mbalimbali wa kada tofauti.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu kupitia muongozo wa serikali, inakusudia kujenga jengo jipya la ofisi katika kiwanja kilichopo Mazizini. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaombewa jumla ya Tzs.632,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**SEKTA YA USAFIRI WA NCHI KAVU.**
Mhe. Spika, katika sekta ya usafiri wa nchi kavu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inajukumu la kuwapatia wananchi huduma bora za usafiri wa barabara kwa kushughulikia ujenzi na utunzaji wa miundombinu ya barabara na madaraja na pia kusimamia shughuli za uendeshaji wa huduma za usafiri wa barabara pamoja na usalama barabarani. Majukumu hayo yanatekelezwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara pamoja na Idara ya Usafiri na Leseni.

**Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara**

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imezifanyia matengenezo barabara kadhaa za mjini na vijijini Unguja na Pemba kwa kutumia mfuko wa barabara. (kimbatanisho nam.3)

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs.6,000,000 kutokana na mapato mengineyo na ilitengewa jumla ya Tzs.1,070,683,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi Machi 2011 jumla ya Tzs.1,700,000 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 28 na fedha zilizotolewa kwa kazi za kawaida ni Tzs.681,555,940 sawa na asilimia 64 ya makadirio.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara inakusudia kutekeleza na kusimamia miradi mbali mbali ya ujenzi wa barabara iliyopangiwa. Aidha idara kupitia mfuko wa barabara itaendelea kuzitunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za mijini na vijijini Unguja na Pemba ili kuzifanya zipitike kwa muda wote kwa lengo la kuwarahisishia wananchi usafiri.

Mhe. Spika, Kwa upande wa kazi za maendeleo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 11 ya ujenzi wa barabara. Taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo na fedha inazoombewa kwa mwaka 2011/12 ni kama ifuatavyo:

**(i) Mradi wa Barabara Kuu za Zanzibar**:

Mradi huu unagharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB). Mradi huu unazihusisha barabara za Amani–Dunga jumla ya (km 12.7) Mfenesini-Bumbwini (km 13.2) na madaraja 4 katika barabara ya Mahonda-Donge-Mkokotoni. Hatua iliyofikiwa ni kuwa barabara ya Amani-Dunga jumla ya km 6.5 zimeshajengwa kwa kifusi na kutiwa lami. Kwa sehemu iliyobaki kazi za usafishaji zimekamilika na kazi za uwekaji kifusi zinaendelea. Aidha kazi za ujenzi wa daraja la Mwera unaendelea.

Kwa upande wa Barabara ya Mfenesini-Bumbwini jumla ya km 9.6 zimeshajengwa kwa kiwango cha kifusi *(sub base)* na mkandarasi anaendelea na kazi za usafishaji wa km 3.6. Aidha ujenzi wa Daraja la Maji Mekundu umeshakamilika. Kuhusu ujenzi wa madaraja katika barabara ya Mahonda-Donge-Mkokotoni kazi za ujenzi wa nguzo katika madaraja ya Mwanakombo na Kipange zimeshakamilika. Mradi huu unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu wa 2011.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mradi huu unaombewa jumla ya Tzs. 1.2 bilioni kutoka Serikalini.

**(ii) Mradi wa Barabara za Vijijini Kusini Pemba *(South Pemba Rural Roads)***

Mhe. Spika, Mradi huu unaofadhiliwa na Serikali ya Norway pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao unajumuisha ujenzi wa barabara sita (6) unaendelea. Aidha Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia mfumo wa nguvu kazi *(labour base)* kwa lengo la kutoa ajira kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopita barabara hizo. Mfumo huu unakwenda sambamba na malengo ya Serikali ya kupunguza umasikini.

Mhe. Spika, Hatua zilizofikiwa kwa mradi huu ni kuwa barabara ya Mtambile – Kengeja - Mwambe (km 9.4) na Mtambile – Kangani (6.4) zimekamilika kwa kiwango cha lami.

Aidha kwa upande wa barabara ya Mizingani- Wambaa (km 9.4) kazi za usafishaji zimekamilika na kuwekwa kifusi kwa tabaka la mwanzo (sub grade) na tabaka la pili *(sub base)* limefikia km 7.

Mhe. Spika, barabara ya Kenya-Chambani (km 3.2) kazi za usafishaji zimekamilika na jumla ya km 2.9 zimeshajengwa kwa kifusi. Aidha kazi za ujenzi wa "*culverts*" zimekamilika. Kwa upande wa barabara ya Chanjamjawiri-Tundaua (km11.0) ujenzi umeshaanza kwa kazi za usafishaji ambapo jumla ya km 5.5 zimekamilika, kazi za uwekaji kifusi zimefikia km 2.0 na ujenzi wa *culvert* 2 unaendelea. Ujenzi wa barabara ya Chanjaani-Pujini (km 5.2) utaanza mapema katika mwaka huu wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara inategemea kukamilisha mradi huu na jumla ya Tzs. 850 milioni zinaombwa kutoka Serikalini.

**(iii) Mradi wa Barabara tatu za Pemba**

Mhe. Spika, Mradi huu unaogharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (Saud Fund) unazihusisha barabara za Chake – Wete (km.24), Wete – Konde (km 15.0) na Wete – Gando (km.15.0) na kwa awamu ya kwanza umepanga kujenga barabara ya Wete Konde na Wete – Gando.

Mhe. Spika, Kwa upande wa barabara ya Wete–Konde jumla ya km 14 zimeshajengwa kwa kifusi. Aidha kwa barabara ya Wete-Gando jumla ya km 8 zimeshasafishwa kati ya hizo km 3 zimeshawekwa kifusi.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara hizo na jumla ya Tzs. 2.48 bilioni zinaombwa kutoka Serikalini.

**(iv) Mradi wa Barabara ya Ole-Kengeja**

Mhe. Spika, Mradi huu unagharamiwa na Jumuiya ya Nchi zinazosafirisha Mafuta kwa Wingi Duniani (OPEC) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao una lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Ole hadi Kengeja yenye urefu wa kilomita 35. Tathmini za zabuni za ujenzi kwa barabara hiyo na usimamizi zimeshakamilika. Hivi sasa wizara inaendelea na majadiliano na mfadhili wa mradi huo.

**(v) Mradi wa Barabara za Vijijini Kaskazini Pemba:**

Mhe. Spika mradi huu unagharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Marekani kwa kupitia kwa Mfuko wa Changamoto ya Millenia (MCC). Mradi huu una lengo la kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara za Kaskazini Pemba zenye jumla ya km 35 ambazo ni Mzambarauni/Pandani-Finya (km 7.9), Bahanasa-Daya-Mtambwe (km 13.6), Chwale-Kojani (km 1.9), Kipangani-Kangagani (km 2.7) na Mzambarauni–Mapofu (km 8.9). Hatua ya utekelezaji kwa sasa ni kuwa taratibu za kumpata mshauri muelekezi (*consultant*) kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi na Mkandarasi (*Contractor*) kwa ajili ya ujenzi huo zimo katika hatua ya mwisho. Katika mradi huu Wizara ya Miundombinu ni mratibu tu.

**(vi) Barabara ya Mgagadu-Kiwani**

Mhe. Spika, Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ulikuwa na lengo la kuijenga barabara inayoanzia Mgagadu-Kiwani kwa jumla ya km 7.6. Hadi Machi 2011 kazi za usafishaji zilishakamilika na jumla ya km 0.5 zimeshajengwa kwa kifusi ikiwemo kurekebisha sehemu zenye milima na mabonde. Wizara inakusudia kuendelea na ujenzi wa barabara hiyo kwa mwaka 2011/12 na jumla ya Tzs. 300 milioni zinaombwa kutoka serikalini.

**(vii) Barabara ya Pale-Kiongele**

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ulikuwa na lengo la kuijenga barabara inayoanzia Pale-Kiongele hadi Mkwajuni yenye urefu wa km 11. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni ukamilishaji wa ujenzi wa daraja 1 kati ya 2 ambayo yatahitajika.

Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na hakuna fedha zinazoombwa kutoka mfuko wa serikali kwa vile ujenzi wake utagharamiwa kupitia Mfuko wa Barabara.

**(viii) Barabara ya Mkanyageni-Kangani**

Mhe. Spika, Mradi huu unaendelea na unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ulikuwa na lengo la kuijenga barabara inayoanzia Mkanyageni hadi Kangani yenye urefu wa km 6.5 kwa kiwango cha lami. Hakuna hatua za utekelezaji kwani ujenzi wake unatarajiwa kuanzwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mgagadu – Kiwani.

**(ix) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Amani-Mtoni (Benjamin Mkapa)**

Mhe. Spika, huu ni mradi unaoendelea wenye lengo la kujenga sehemu ya pili

**Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano** (anaendelea) ilikuwa na lengo la kuijenga barabara inayoanzia Mkanyageni hadi Kangani yenye urefu wa km 6.5 kwa kiwango cha lami. Hakuna hatua za utekelezaji kwani ujenzi wake unatarajiwa kuanzwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Mgagadu – Kiwani.

**Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Amani-Mtoni (*Benjamin Mkapa Road*)**
Mhe. Spika, huu ni mradi unaoendelea wenye lengo la kujenga sehemu ya pili ya barabara ya Amani – Mtoni km 4. Hatua iliyofikiwa ni kuwa ujenzi unaendelea kwa usafishaji na kuweka kifusi, ambapo jumla ya 3 km zimekamlika.

**Barabara ya Maeneo Huru (*Fumba Ring Road*)**
Mhe. Spika, mradi huu unaendelea na unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi huu unakusudia kuijenga kwa lami barabara inayopita sehemu za Ukanda wa Maeneo Huru Fumba kwa urefu wa km 10.4. Utekelezaji wa mradi huu haukufanyika.

Mhe. Spika, kutokana na ukosefu wa fedha, mradi huu umeahirishwa hadi mwaka wa fedha 2012/2013.

**Mradi wa Upembuzi Yakinifu wa Barabara Zinazoingia Mjini (*Zanzibar Urban Entry Roads*)**
Mhe. Spika, huu ni mradi mpya unaogharamiwa na Benki ya Dunia ambao unazijumuisha barabara ya Bububu-Mtoni-Kinazini-Malindi *port* (km 19), *Creek road*-Mkunazini-Mnazi Mmoja (km 1.2), Tunguu-Fuoni-Magomeni-Kariakoo-Mkunazini (km 13.3), Welezo-Amani-Ng'ambo-Kariakoo (km 3.5), Mtoni-Amani-Kiembesamaki (km 8.5), Uwanja wa Ndege-Kiembesamaki-Kilimani-

Mnazi Mmoja (km 7) na Bububu-Mahonda-Mkokotoni (km 31). Hatua za utekelezaji ni kuwa Mshauri Mwelekezi wa kazi ya uchambuzi yakinifu, usanifu na utayarishaji wa zabuni ameshaanza kazi tokea mwishoni mwa mwezi wa April, 2011 na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi wa April, 2012.

**Mradi wa Barabara 3 za Vijijini Unguja**
Mhe. Spika, huu ni mradi mpya unaogharamiwa kwa pamoja baina ya Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi huu unazijumuisha barabara za Kizimbani-Kiboje (km 7.2), Koani-Jumbi (6.3) na Jendele-Cheju-Kaebona (km 11.7). Taratibu zakumpata Mshauri Mwelekezi wa kazi kwa ajili ya kazi ya usimamizi wa ujenzi na matayarisho ya zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi zimekamilika. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mradi huu unaombewa jumla ya Tzs. 757 milioni kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012, idara inaombewa jumla ya Tzs.1,004,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na pia kukusanya jumla ya Tzs.5,000,000 kama ni mapato mengineyo.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 wizara inakusudia kukamilisha ujenzi wa barabara zilizosalia katika miradi mbali mbali. Jumla ya Tzs. 9.387 bilioni zinaombwa kutoka Serikalini kwa utekelezaji wa mpango wa maendeleo (**Kiambatisho 4).**

Mhe. Spika, katika hatua za kutekeleza azma yake ya siku nyingi ya kuishirikisha sekta binafsi katika ujenzi na utunzaji wa barabara, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imeshaanza utaratibu wa kutoa baadhi ya kazi kwa kampuni binafsi, vikundi vya jamii na jumuiya zisizo za Serikali. Kwa sasa kazi zinazotolewa ni za ukataji majani, usafishaji wa misingi na *culverts,* matengenezo madogo madogo na nyenginezo. Hatua hii inajenga msingi mzuri wa utekelezaji wa sera ya ushirika wa umma na sekta binafsi. Wizara inakusudia kuweka mikakati ya kujenga uwezo wa kampuni hizo ili hapo baadae ziweze kushiriki katika miradi mikubwa ya barabara.

**Idara ya Usafiri na Leseni.**
Mhe. Spika, idara hii ina majukumu ya kusimamia usalama wa watumiaji wote wa barabara, kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, usimamizi wa mafunzo ya udereva, upasishaji madereva na walimu wa skuli za udereva, kusimamia utoaji huduma usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara. Aidha, idara inasimamia na kuendesha Karakana kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoko Chumbuni na sehemu ya mitambo iliyoko Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011 jumla ya vyombo vya moto 20,328 vilikaguliwa (**Kiambatisho Nam 5 a**). Aidha, idara iliwafanyia mitihani ya nadharia na vitendo jumla ya madereva wanafunzi 3,656 waliohitimu katika skuli mbali mbali za udereva, kati ya hao 2,568 walifaulu na 1,088 hawakufaulu, Vile vile Idara iliwafanyia majaribio ya vitendo madereva 3,656 kati yao 2,568 walifaulu na 1088 hawakufaulu. (**Kiambatisho Nam 5 b)**.

Mhe. Spika, katika kipindi hicho idara ilitoa ruhusa za njia kwa magari 1,806 Unguja na Pemba, kati ya hizo magari ya shamba 482, daladala 374, *private hire* 303, *taxi* 158, magari ya wanafunzi 19, magari ya wafanyakazi 25 na magari ya mizigo 345. Aidha, idara iliendelea na kazi ya uuzaji wa Bendera za Serikali. Idadi ya Bendera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizouzwa katika kipindi hicho ni 179 na za Muungano 141.

Mhe. Spika, Karakana Kuu ilizifanyia matengenezo jumla ya gari 552 katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 41.66 ya vyombo 230 vilivyotengenezwa katika kipindi kama hicho mwaka 2009/2010. Sehemu ya mitambo Pemba iliyafanyia matengenezo jumla ya gari 161 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.2 ikilinganishwa na gari 156 zilizotengenezwa katika kipindi kama hicho 2009/2010.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11 Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs.345,000,000 na kutumia jumla ya Tzs. 384,363,000 kwa kazi za kawaida. Hadi Machi, 2011 ilikusanya jumla ya Tzs.233,464,500 sawa na asilimia 68 na iliingiziwa jumla ya Tzs. 214,087,950 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 56 ya makadirio.

**Malengo kwa Mwaka 2011/2012**

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, idara itachukua hatua mbali mbali za kuimarisha usalama barabarani zikiwemo kuendelea kuwapatia elimu watumiaji wa barabara, na kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya moto. Aidha, hatua zitachukuliwa za kuhakikisha kuwa karakana kuu ya Unguja na Sehemu ya mitambo Pemba zinaimarishwa kwa kupatiwa vifaa na wafanyakazi wenye ujuzi na teknolojia ya kisasa ya vyombo vya moto.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara ya Usafiri na Leseni inatarajia kukusanya jumla ya Tzs. 280,600,000 na inaombewa jumla ya Tzs. 370,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

**SEKTA YA USAFIRI WA ANGA**

Mhe. Spika, Sekta ya Usafiri wa Anga ina majukumu ya kusimamia huduma za usafiri wa anga, kuimarisha usalama wa ndege, abiria na mizigo. Majukumu haya yanatekelezwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa

mashirikiano ya pamoja na taasisi mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na sekta binafsi.

**Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar**

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaratibu na kusimamia maendeleo ya usafiri wa Anga Zanzibar pamoja na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/11 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetekeleza kazi mbali mbali za kawaida za kuhudumia ndege, abiria na mizigo. Viwanja vya Unguja na Pemba vimehudumia jumla ya ndege 44,483 ikilinganishwa na ndege 33,392 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha 2009/2010 ikiwa ni ongezeko la asilimia 33. Kati ya ndege hizo, ndege 30,983 zilihudumiwa katika kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na ndege 4,050 zilihudumiwa katika kiwanja cha Pemba **(Kiambatanisho Nam.6 a).**

Mhe. Spika, idadi ya abiria waliohudumiwa katika viwanja vya ndege vya Zanzibar ilikuwa ni 510,942 kuanzia mwezi Julai, 2010 hadi Machi, 2011 ikilinganishwa na abiria 479,742 waliohudumiwa katika kipindi kilichopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 6.5. (**Kiambatisho Nam.6 b)**. Kati ya abiria hao, abiria 476,223 walihudumiwa katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na abiria 34,880 walihudumiwa katika Kiwanja cha Pemba. Aidha, abiria waliopita (*transit*) wamefikia 59,952. Takwimu hizo zinaonyesha kwamba kumekuwepo na ongezeko la idadi ya ndege na abiria waliohudumiwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2009/2010. Hii inatokana na kuimarika kwa miundombinu ya kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume na kuimarika kwa uchumi wa dunia ambapo watalii wameendelea kuja hapa nchini kwa kutumia usafiri wa anga.

Mhe. Spika, kwa upande wa mizigo (*freight*) jumla ya kilogramu 560,804 zilihudumiwa katika viwanja vyetu vya ndege vya Unguja na Pemba ikilinganishwa na kilogramu 624,140 zilizohudumiwa kipindi kilichopita, hii ni kutokana na kupungua idadi ya ndege za mizigo.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 Mamlaka ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs 1,130,000,000 na kutumia jumla ya Tzs 763,418,000 kwa kazi za kawaida.

Mhe. Spika, hadi Machi, 2011 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekusanya jumla ya Tzs.950,762,694 sawa na asilimia 84.15 ya makadirio. Mapato hayo yamekusanywa kutokana na ada za utuaji ndege kiwanjani (*landing fees*), kodi

za ofisi (*rents*), na mapato mengineyo. Na imeingiziwa jumla ya Tzs 626,486,120 ya kazi za kawaida sawa na asilimia 82 ya makadirio.

**Malengo ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa Mwaka 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaendelea kuimarisha huduma mbali mbali za viwanja vyetu kukidhi mahitaji ya watumiaji wa ndani na ya Kimataifa juu ya Usafiri wa Anga.

Mhe. Spika, kwa upande wa kazi za maendeleo Mamlaka inatarajia kuendeleza miradi iliyopangiwa kama ifuatavyo:

**Uendelezaji wa Ujenzi wa Uzio**

Mhe. Spika, ujenzi wa uzio unaozunguka kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume ni mradi unaoendelea baada ya kukamilika barabara ya kurukia na kutulia ndege. Hadi sasa kazi za ujenzi zimeshafikia urefu wa kilomita sita (6 km).

**Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria (*Terminal building*)**

Mhe. Spika, mradi huu unaendelea na una lengo la kujenga jengo jipya la abiria, maegesho ya ndege, maegesho ya magari pamoja na jengo la mitambo (*service building*) na uwekaji wa vifaa mbali mbali katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume. Mradi huu unagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Benki ya Exim ya China na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi za ujenzi zinaendelea vizuri.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara inaomba jumla ya Tzs. 1.5 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**Ujenzi wa Maegesho na Njia ya Kupitia Ndege (*extension of apron and taxiway*) Uwanja wa Ndege wa Kimataifa.**

Mhe. Spika, mradi huu ni mpya na una lengo la ujenzi wa sehemu ya maegesho (*apron*) na kuimarisha njia za kupitia ndege (*taxiways*) katika Kiwanja cha Ndege cha kimataifa Abeid Amani Karume. Mradi huu utagharamiwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wizara hivi sasa inakamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi na Msimamizi wa ujenzi huo.

Mhe. Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huu wizara inaomba jumla ya Tsh. 2.00 bilioni.

**Uimarishaji wa Huduma za Viwanja vya Ndege**

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na unalengo la kufanya ukarabati wa mitambo ya umeme, matengenezo ya jengo la sasa la abiria, kujenga ofisi za mashirika ya ndege, mikahawa na majengo mengine kwa huduma mbali mbali. Wizara inaomba jumla ya Tzs.300 milioni kugharamia mradi huu.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inatarajia kukusanya jumla ya Tzs.1,210,410,000. Ili kutekeleza shughuli zake kama ilivyopangiwa Mamlaka inaombewa jumla ya Tzs. 806,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

**Mashirika ya Muungano (Sekta ya Usafiri wa Anga)**

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2011/2012 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itaendelea kuratibu shughuli za usafiri na mawasiliano kwa kushirikiana na mashirika ya Muungano yaliyopo Zanzibar, na kwa upande wa anga Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itashirikiana na Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga (*TCAA*) pamoja na Mamlaka ya Hali ya hewa (*TMA*) Tanzania katika kutoa huduma za hali ya hewa hapa nchini.

**Mchango wa Sekta Binafsi**

Mhe. Spika, sekta binafsi inatoa mchango mkubwa katika kusadia juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha usafiri wa anga hapa Zanzibar. Mchango huu unaisaidia nchi yetu kwa kuingiza mapato yatokanayo na kodi mbali mbali na kutoa ajira kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 kampuni mbali mbali za ndani na nje ya nchi ziliendelea kutumia viwanja vyetu vya ndege. Kampuni hizo ni kama zionekanavyo (**Kiambatanisho Nam. 7)** wizara itaendelea kuongeza ushirikiano na makampuni ili kurahisisha huduma za usafiri wa anga.

**SEKTA YA USAFIRI WA BAHARINI**

Mhe. Spika, katika Sekta ya Usafiri wa Baharini Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya usafiri wa baharini katika Zanzibar kwa kuweka miundombinu ya bandari, kusimamia utoaji wa huduma za usafiri na kulinda usalama wa watu na mali zao pamoja na mazingira ya baharini yasichafuliwe. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini, Shirika la Bandari, Shirika la Meli, pamoja na kampuni za watu binafsi ambazo zimewekeza katika sekta hii.

**MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI**

Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri Baharini imeanzishwa chini ya sheria Nam. 3 ya mwaka 2009. *(Zanzibar Maritime Authority, Act No. 3 of 2009).* Kabla ya kuanzishwa Mamlaka, majukumu yake yalikuwa yakisimamiwa na kutekelezwa na Kitengo cha Mrajis wa Meli ambacho kilikuwa chini ya Idara ya Mipango na Sera katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri Baharini ni Mamlaka yenye jukumu la kusimamia usalama na ulinzi wa vyombo vya baharini. Majukumu mengine ni pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni

kwa vyombo vidogo vidogo, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya baharini, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia.

Vile vile Mamlaka hudhibiti safari za baharini, uchunguzi wa ajali baharini, usimamizi wa maslahi ya mabaharia, pamoja na utoaji wa leseni za manahodha na wahandisi wa vyombo vidogo vidogo.

Aidha, Mamlaka inasimamia utekelezaji wa kanuni ya kimataifa ya ulinzi wa meli na bandari (*ISPS Code*) na uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa maeneo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011 Mamlaka ilisajili meli 8 zenye uzito wa jumla *GRT* 1,600 kwa usajili wa ndani (*Tanzania Zanzibar Registry*) na meli 70 zenye uzito wa jumla *GRT* 367,144.63 kwa usajili wa nje (*Tanzania Zanzibar International Registry*) (**kiambatanisho Nam. 8).** Aidha, vyombo vidogo vidogo 35 vyenye uzito wa jumla ya tani 525 *GT* vilisajiliwa.

**Malengo ya Mamlaka kwa Mwaka 2011/2012.**
Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/12 Mamlaka itaendelea kujiimarisha katika utendaji wake wa kazi na kukuza vyanzo vyake vya mapato, kuandaa kanuni zilizobaki za Sheria ya Usafiri Baharini, kuongeza matawi mengine ya usajili wa kimataifa.

Pia Mamlaka inatayarisha kanuni za kusimamia makampuni na taasisi zinazotoa huduma katika bandari na meli, hatua hizo ni pamoja na kuwapatia leseni waendeshaji wa hudumu hizo na kudhibiti shughuli zao.
Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012 Mamlaka imepangiwa kukusanya jumla ya Tzs. 163,000,000 na inaombewa jumla ya Tzs. 128,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

## SHIRIKA LA BANDARI
Mhe. Spika, Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika Bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na usimamizi wa usalama ndani ya maeneo ya bandari hizo.

Vile vile Shirika linawajibu wa kuhifadhi mizigo na utunzaji wake katika bandari pamoja na kuvifanyia matengenezo madogo madogo vyombo mbali mbali vya usafiri wa baharini kwa kutumia Karakana yake Kuu ya Malindi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011, shirika liliendelea na kazi zake za kutoa huduma mbali mbali kama inavyoonekana katika (**kiambatanisho Nam 9).**

**Kazi za Kiufundi**
Mhe. Spika, **S**hirika katika kipindi hicho limefanya kazi mbali mbali za kiufundi zikiwemo matengenezo ya vyombo vya baharini vinavyomilikiwa na Shirika lenyewe, pamoja na vyombo vya kampuni binafsi vilivyohitaji huduma za chelezo.

Mhe. Spika, shirika limeweza kuufanyia matengenezo ukuta wa Forodhani, ambao uliathirika kutokana na mawimbi makubwa yaliyosababishwa na upepo mkali. Vile vile Shirika limekamilisha kazi za ujenzi wa chelezo (*ramp*) kwa ajili ya matumizi ya meli za *"landing craft"* karibu na eneo la Gati ya Abiria. Aidha, Shirika limejenga ukuta unaotenganisha baina ya Bandari Kuu ya Malindi na Bandari ya Majahazi (*dhow shed*). Pia barabara ya kuingilia Bandarini kutoka *"Round About"* ya Malindi mpaka mlango mkuu zimefanyiwa matengenezo na eneo la kuegeshea gari katika gati ya abiria limeimarishwa.
Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadiMachi, 2011, Shirika limetekeleza miradi ifuatayo:-

**Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani**
Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kuiimarisha Bandari ya Mkoani kwa kurekebisha eneo lililodidimia katikati ya gati. Hadi kufikia mwezi Machi, 2011 Shirika limekamilisha maandalizi ya kazi hiyo na matengenezo ya eneo hilo yanategemewa kuanza mwezi wa Julai, 2011.

**Matengenezo ya Meli ya *L.C.T* Jitihada**
Mhe. Spika, lengo la Mradi huu lilikuwa ni kuifanyia matengenezo makubwa Meli ya *L.C.T* Jitihada ambayo imekabidhiwa Shirika la Bandari kutoka Serikalini. Shirika tayari limeshakamilisha matengenezo yote ya meli hiyo na hivi sasa inafanya kazi.
**Ujenzi wa Sehemu ya Kuegesha Vyombo vya Mizigo aina ya *"Landing Craft"***
Mhe. Spika, mradi huu una lengo la kujenga ***"Ramp"*** kwa ajili ya kuegesha vyombo vya aina ya *"Landing Craft"* ambavyo vilikuwa vinahudumiwa Forodha Mchanga. Hadi kufikia Machi, 2011 kazi zote za ujenzi zimeshakamilika na wakati wowote eneo hilo litaanza kutumika.

**Ununuzi wa *Radio Base 2* (*GMDSS*)**
Mhe. Spika, radio hizo ambazo ni kwa ajili ya shughuli za mawasiliano tayari zimeshanunuliwa na zitaanza kutumika Unguja na Pemba kama ilivyopangwa.
**Ukarabati wa Mnara wa Mwana wa Mwana.**

Mhe. Spika, ukarabati wa mnara huo umekamilika.

**Ununuzi wa Tishali la Kuegesha Vyombo vya Abiria**

Mhe. Spika, lengo la mradi huu ni ununuzi wa tishali jipya la kuegeshea vyombo vya abiria ambalo linatumika wakati tishali kubwa lililokuwa likitumiwa hivi sasa limepelekwa chelezoni.

**Mapato na Matumizi**

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011 Shirika lilikadiria kukusanya Jumla ya Tzs.6,215,114,388.64 kutokana na mauzo ya huduma zake mbali mbali. Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Machi, 2011 Jumla ya Tzs. 7,354,041,435.79 zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 118.33 ya makadirio. Aidha, jumla ya Tzs. 4,650,392,372.45 zilitumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilima 101.15 ya makadirio ya matumizi kwa kipindi hicho.

**Malengo ya Shirika kwa Mwaka 2011/2012**

Mhe. Spika, Shirika la Bandari litaendelea kutekeleza majukumu yake. Shirika katika kipindi hicho linategemea kuteremsha na kupakia kiasi cha tani 100,000 za mzigo mchanganyiko pamoja na makontena 30,000

Mhe. Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo Shirika linatarajia kuendelea na uimarishaji wa huduma na rasilmali zake kwa kuikamilisha miradi iliyoanzishwa mwaka wa fedha unaomalizika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi bandarini na ununuzi wa taa za *solar* kwa minara na maboya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, Shirika limekadiria kukusanya jumla ya Tzs. 9.3 bilioni katika kipindi cha Julai, 2011 hadi Juni 2012. Aidha, katika kutekeleza malengo hayo Shirika limepanga kutumia jumla ya Tzs.6.5 bilioni kwa kazi za kawaida.

**SHIRIKA LA MELI**

Mhe. Spika, Shirika la Meli lina jukumu la kuendesha meli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kutoa huduma za uwakala wa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar. Kwa sasa Shirika linaendesha meli mbili za M.T Ukombozi na M.V Maendeleo na lina matawi mawili katika Bandari za Dar es salaam na Pemba.

**Mapato na Matumizi ya Shirika**

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011 Shirika lilikukusanya Jumla ya Tzs. 2,976,732,258.85 sawa na asilimia 107 ya makisio ya mwaka 2010/2011 ya Tzs.2,790,015,900 na kufanya matumizi ya jumla ya Tzs.2,923,706,489.95 sawa na asilimia 116 ya makisio ya mwaka 2010/2011 ya Tzs. 2,511,954,812.

**Uendeshaji wa Shirika**

Mhe. Spika, pamoja na Shirika kupata mafanikio, bado linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Uchakavu wa meli Maharibiko ya meli mara kwa mara, Kuongezeka gharama za matengenezo na uagiziaji vipuri, upandaji wa bei za mafuta mara kwa mara idadi kubwa ya wafanyakazi

Mhe. Spika, kutokana na matatizo hayo ni dhahiri Shirika linashindwa kufanya shughuli zake kibiashara, hivyo kuna haja ya kufanya maamuzi ya kubadili uendeshaji wa Shirika ikiwa ni pamoja na kufikiria ununuzi wa meli nyengine zitazoweza kuhimili ushindani ndani ya soko, kupitisha Sheria ya Shirika itakayotoa mamlaka kwa Shirika kumiliki vyombo (meli) ili umiliki huu uweze kutumika kukuza biashara za Shirika kwa kutumia fursa za mikopo ya benki nchini.

**Malengo ya Shirika kwa mwaka 2011/2012**

Mhe. Spika, Shirika limepanga mikakati ya kujiimarisha zaidi kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

1. Kufanya maamuzi ya kubadili meli tulizonazo ambazo zimepitwa na wakati kwa kuziuza na kununua meli nyengine zitazoweza kuhimili ushindani ndani ya soko.
2. Kuanzisha ajira ya mkataba *"Sign On/Sign Off"* kwa mabaharia wa meli zetu.
3. Kukamilisha Sheria ya uanzishwaji upya wa Shirika la Meli na Uwakala.
4. Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Uwakala wa meli za nje katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Shirika linategemea kukusanya jumla ya Tzs 3.6 bilioni kutokana na vianzio vyake vya mapato na kutumia jumla ya Tzs 3.4 bilioni.

**Mchango wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Usafiri Baharini**

Mhe. Spika, Sekta binafsi ni miongoni mwa mihimili mikuu ya maendeleo ya sekta ya usafiri wa baharini. Hivi sasa kuna zaidi ya kampuni 20 ambazo zimewekeza katika usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Unguja na Pemba na baina ya bandari za visiwa hivi na bandari nyengine katika mwambao wa Afrika Mashariki.

Mhe. Spika, mchango wa sekta binafsi unasaidia kujenga uchumi wetu kwa kutoa huduma bora zenye kufanikisha sekta nyengine kiuchumi na kijamii,

kuchangia katika pato la nchi na kutoa ajira kwa wananchi. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatambua na kuthamini mchango huo.

**SEKTA YA MAWASILIANO**

Mhe. Spika, Sekta ya Mawasiliano inatoa mchango mkubwa katika kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii na inajumuisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa njia za posta, simu na huduma za teknolojia ya habari.

**Idara ya Mawasiliano**

Mhe. Spika, Idara hii imeundwa kwa lengo la kuharakisha matumizi ya teknolojia ya habari katika sekta ya umma na binafsi na kuhakikisha kwamba jamii ya Zanzibar inanufaika na maendeleo hayo. Idara ina jukumu la kusimamia maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano na kuratibu masuala ya taasisi za mawasiliano za Serikali ya Muungano ziliopo Zanzibar. Katika maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano Idara itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano ikiwa ni pamoja na Mkonga wa Kitaifa na kudhibiti matumizi na utoaji wa huduma za teknolojia ya habari *(IT).*

Mhe. Spika, kwa mwaka 2010/2011 idara kupiitia Kamati ilifanya ukaguzi na usimamizi wa utumiaji wa minara ya mawasiliano ikiwemo ya simu, redio na *internet*. Kamati hiyo iliundwa mwaka 2009 baada ya kuonekana kuna ujenzi holela wa minara ambayo ilisababisha kero na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi. Katika kipindi chote hicho Kamati imekagua minara 121 kutoka makampuni mbali mbali yakiwemo *Zantel, Airtel, Tigo, Vodacom, TTCL* na Chuchu FM na hatimae kutoa hati.

**Malengo kwa Mwaka 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ina malengo ya kusimamia Mkonga wa Taifa, kusimamia Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT),* kusimamia *Transformation* ya Mawasiliano kutoka *Analogue* kwenda *Digital* na kushirikiana na wadau wengine kusimamia zoezi la uwekaji wa Simbo za Posta *(Postal Code).*

Mhe. Spika, Idara inakabiliwa na upungufu wa wataalam katika fani ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT)* na vifaa vya kufanyia kazi.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara inaombewa jumla ya Tzs 103,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

**Kampuni ya *Zantel***

Mhe. Spika, Kampuni ya *Zantel* imeasisiwa hapa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa ya asilimia 18.

Kampuni hiyo inatoa huduma za simu za mkononi Tanzania na inakusudia kuimarisha huduma zake kwa wateja kwa kuongeza vituo vya huduma kwa Zanzibar kwa mwaka 2011 kuanzia vituo 80 hadi kufikia vituo 130 ifikapo mwaka 2012. Vile vile kuwawezesha wananchi kupata mawasiliano ya simu kwenye yale maeneo ambayo mawasiliano ni magumu kupatikana.

*Zantel* inaanzisha huduma za teknolojia ya 3G ili kuwapatia wakaazi wa Zanzibar huduma bora na za kasi za data na *internet* na kutekeleza mradi mpya wa utanuzi ambao utaongeza vituo 75 katika mtandao.

Mhe. Spika, katika mwaka 2010/2011 Kampuni ya *Zantel* imeendelea kushikilia rekodi yake ya kuwa mchangiaji namba moja wa mapato kwa kulipa kodi mbali mbali Serikalini. Aidha, imechangia katika shughuli mbali mbali za kijamii. *Zantel* ni kampuni mojawapo ya simu ya kibinafsi inayoendelea kutoa ajira kwa wananchi wa Zanzibar.

**Taasisi za Muungano (Sekta ya Mawasiliano)**

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itaendelea kuratibu masuala ya mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi za Muungano zinazotoa huduma za mawasiliano, simu na posta zilizopo Zanzibar. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* Shirika la simu Tanzania *(TTCL)* na Shirika la Posta Tanzania *(TPC).*

**Maombi ya fedha kwa mwaka 2011/2012**

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutekeleza majukumu yake na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Tzs.13,645,598,000. Kati ya fedha hizo, Tzs. 4,258,000,000 kwa kazi za kawaida na Tzs.9,387,598,000 kwa kazi za maendeleo.

Aidha, naliomba Baraaza lako tukufu liiruhusu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kukusanya mapato ya jumla ya Tzs.1,757,990,000 kutokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya Wizara hii.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwako na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokuwa nikitoa maelezo ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa mchango ambao utaisaidia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutatua matatizo ambayo ilikumbana nayo katika kipindi cha mwaka 2010/2011 ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Aidha, kwa kuzingatia kuwa huu ni mwaka wa mwanzo wa awamu ya saba unaotokea kwenye mchakato wa uchaguzi mkuu uliopita na kuwa baadhi ya wajumbe wako ni wapya na wengine ni wakongwe Barazani, naomba nichukue fursa hii kwanza kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa ushirikiano wao kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na pia kuwatakia kazi njema katika kulitumikia Taifa kwa kipindi hichi cha miaka mitano.

Mhe. Spika, mafanikio ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo nimeyaeleza katika hotuba hii ni matokeo ya ushirikiano wa wadau mbali mbali wa ndani na nje. Napenda kuchukua fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza nchi, jumuiya na taasisi zifuatazo kwa misaada yao muhimu katika kuendeleza sekta mbali mbali za Wizara hii.

Nchi hizo ni Jamhuri ya Watu wa China, Norway, Uingereza, Iran, Ufaransa, Uholanzi, Ireland, Libya, Japan, Saudi Arabia, India, Misri, Marekani, Ujerumani, Uturuki, Oman, *UAE,* Kenya, Uganda, Ethiopia. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Benki ya Dunia *(World Bank), China Exim Bank,* Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* Mfuko wa Umoja wa Maendeleo ya Kimataifa wa Nchi zinazosafirisha mafuta kwa wingi ulimwenguni *(OPEC Fund), SAUDI Fund, NORAD,* Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP, IMO, ICAO.*

Mhe. Spika, kadhalika nachukua fursa hii kuyashukuru makampuni ya kibiashara ya kimataifa ambayo yamechangia katika sekta ya usafirishaji ni pamoja na *Oman Air, Kenya Airways, Ethiopian Airline, Air Uganda* na kwa upande wa baharini *Maersk, MSC, UAFL, Emirates Shipping* na *CMA CGM* pamoja na Kampuni ya *Danaos* inayotoa ajira ya ubaharia kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, niruhusu tena kupitia kwako kuwashukuru na kuwapongeza wamiliki wa ndani wa vyombo vya usafiri baharini, nchi kavu na anga ambao wanashirikiana na Serikali katika kutoa huduma za usafiri.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali na kwa kupitia Baraza lako Tukufu naomba kutoa wito kuwaomba wadau tuliowataja hapo juu na wengineo kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa huduma za usafirishaji.

Mhe. Spika, napenda nimalizie kwa kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali.

Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao.

Mhe. Spika, shukurani za pekee zimwendee Mpiga Chapa Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Kiwanda cha Upigaji Chapa kwa kufanikisha uchapaji wa vitabu mbali mbali pamoja na uchapaji wa hotuba hii, na wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za Wizara hii.

Naomba kuwashukuru wafanyakazi wote wa Taasisi za Serikali na Watu Binafsi pamoja na wananchi kwa jumla kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kufanya kazi kwa uaminifu, nidhamu na moyo wa kuipenda nchi yao na kazi yao.

Mhe. Spika, hotuba yangu haitokamilika kama sijatoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo langu la Ole kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokuwa mbali nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili. Nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya pekee.

Mhe. Spika, leo asubuhi tulipata faraja kubwa Mhe. Ali Mzee Ali ulipomwita ukamuapisha na kuungana na Baraza hili. Kwa kweli leo ni siku maalum Mhe. Ali Mzee Ali kwa ufahamu wangu mdogo ni muasisi, ni *pioneer,* ni *veteran* wa uanzishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ni miongoni mwa Wazanzibari waliojitolea ikifika muda tu, lakini kwa hali na mali kuhakikisha kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa inaundwa. Kwa hivyo, leo Mhe. Ali ameingia katika chombo ambacho yale ambayo alikuwa anayapigania atayatekeleza.

Mhe. Spika, Baraza lililopita tulimpa jina la Profesa. Nakuomba Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima ukubali Mhe. Ali Mzee Ali aendelee na jina la Profesa katika Baraza hili.

Michango yake kwa wale ambao ni wapya wataamini kwamba kipindi cha Baraza hili ambapo yeye hakuwepo tulikosa mengi, pia watakubali kwamba sasa tutapata mengi kwa sababu ni Profesa wa kweli. Mhe. Ali Mzee Ali karibu, tupo, tumefurahi na leo furaha yetu ni ile ya kuongeza muda kuanzia saa saba mpaka saa tisa.

Mhe. Spika, hotuba yangu hii ambayo nimeiwasilisha, mara baada ya kuiwasilisha ipo kwenye tovuti. Kwa hivyo, wale wote ambao hawana vitabu hivi waende kwenye tovuti www.prrp.ch, wakifungua sasa hivi hotuba hii wataikuta.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha hotuba ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ufasaha mkubwa na umetumia kama muda wa saa moja na dakika kumi.

Hoja imeungwa mkono na tulikubaliana mapema pale asubuhi kwamba labda kama tutasema vyenginevyo hotuba hii iwasilishwe na kuna shughuli moja ambayo ilitolewa hati mapema asubuhi ambayo ni kumsikiliza Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.. Baada ya hapo tena tukaamua kama tuendelee au tukapumzike mapema wakati wajumbe wanajitayarisha kuweka pointi zao vizuri kwa kesho kuanza mjadala mapema asubuhi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Rashid Seif Suleiman (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi):** Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kukutana hapa leo hii, kwa madhumuni ya kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nitumie nafasi hii adhimu kukushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuwasilisha maoni ya Kamati yetu ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa lengo la kuisaidia wizara na serikali kwa ujumla katika kuhakikisha kuwa maendeleo ya Zanzibar na watu wake yanapatikana.

Mhe. Spika, Kamati yetu haitoweza kuacha kumshukuru Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na watendaji wote wa wizara yake kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati. Mashirikiano hayo ndio ambayo kwa kiasi kikubwa yameiwezesha Kamati kufanya kazi yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, sina budi kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wenzangu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwa kazi kubwa walioifanya katika kipindi chote cha kupitia bajeti ya wizara. Kwa heshima naomba niwataje wajumbe wa kamati hii pamoja na makatibu walioisaidia kamati katika kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Rashid Seif Suleiman | - | Makamo Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Subeit Khamis Faki | - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Salum Amour Mtondoo | - | Mjumbe |
| 7. Mhe. Hassan Hamad Omar | - | Mjumbe |
| 8. Ndg. Mussa Kombo Bakari | - | Katibu |
| 9. Ndg. Aziza Wazir Kheir | - | Katibu |

Mhe. Spika, baada ya kuanza na utangulizi huo, naomba sasa nianze kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Spika, hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri imegusa mambo mengi muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Kamati yetu inapenda kutoa mchango wake katika baadhi ya maeneo kwa lengo la kusaidia katika juhudi za serikali za kuwaletea wananchi wa Zanzibar maendeleo. Sasa naomba niyataje maeneo ambayo Kamati hii kwa umuhimu wake imeona ni vyema kuyachangia kama ifuatavyo:-

**UKUSANYAJI WA MAPATO**

Mhe. Spika, hatuna budi kuipongeza Wizara kwa juhudi mbali mbali ilizozichukua katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011. Ni dhahiri kuwa bajeti hiyo ilitekelezwa vizuri na taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara hii. Kwa mfano, baadhi ya taasisi zenye mamlaka ya kukusanya mapato, zimeweza kufanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato hadi kufikia mwezi Machi, 2011. Baadhi ya taasisi hizo zilizofanya vizuri katika ukusanyaji huo wa mapato ni pamoja na Idara ya Anga ambayo sasa inajulikana kama Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambayo hadi Machi imekusanya asilimia 84 ya makisio, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini hadi kufikia Machi, 2011 ilishakusanya asilimia 99.74 ya makisio, Shirika la Bandari ambalo hadi Machi, 2011 limekusanya asilimia 118 ya makisio na Shirika la Meli ambalo hadi kipindi cha Machi, 2011 lilishakusanya asilimia 95 ya makisio.

Mhe. Spika, ukusanyaji huo wa mapato ni hatua muhimu ya kuimarisha uchumi wa nchi hasa ukizingatia kuwa fedha hizo husaidia katika bajeti ya Serikali. Kamati inazihimiza taasisi hizo na nyenginezo kufanya jitihada ya kuongeza makusanyo ya mapato kwa lengo la kukuza pato la taifa na hivyo kupelekea maendeleo ya nchi. Ni imani ya Kamati hii kuwa inawezekana kuongeza makusanyo hayo ikiwa kutakuwa na uwajibikaji zaidi na nidhamu na uadilifu katika masuala ya fedha. Kwa msingi huo, Kamati yetu inatumai kuwa ukusanyaji huo wa mapato katika mwaka wa fedha 2011/2012 utavuka malengo kwa kiasi kikubwa sana.

**UFUATILIAJI WA MADENI YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

Mhe. Spika, kwa kuzingatia kuongezeka kwa mahitaji ya serikali katika kuwahudumia wananchi katika sekta mbali mbali ikiwemo afya, elimu, maji na miundombinu, wizara haina budi kuchangia upatikanaji wa mapato zaidi ili kukidhi huduma hizo. Miongoni mwa vyanzo muhimu vitakavyotuletea mapato zaidi ni ufuatiliaji wa madeni ambayo taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara inazidai taasisi nyengine hasa zile zisizokuwa za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mfano kwa mujibu wa kitabu cha Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2010/2011, Idara ya Anga imeripotiwa katika ripoti ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *(P.A.C)* kuwa inalidai Shirika la Ndege la *A.T.C* zaidi ya shilingi milioni mia mbili na arobaini. Fedha hizo si kidogo na zinaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa katika bajeti yetu na hivyo kupelekea katika maendeleo ya nchi yetu. Kamati yetu inatoa wito kwa wizara kuhakikisha kuwa deni hilo na madeni mengine yanalipwa kwa wakati ili kuongeza mapato yetu ya ndani.

**UJENZI WA JENGO JIPYA UWANJA WA NDEGE WA KIMATAIFA ZANZIBAR**

Mhe. Spika, mojawapo ya eneo muhimu ambalo Kamati hii imeguswa nalo ni suala la ujenzi wa jengo jipya katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Zanzibar. Tunapenda kupongeza kwa dhati juhudi za serikali kwa kufikiria na kuanza hatua za utekelezaji wa ujenzi huo. Kamati inatoa pongezi hizo kutokana na umuhimu wa uwanja wa ndege kama chanzo muhimu cha mapato ambacho kwa kiasi kikubwa kinachangia bajeti yetu. Ni imani yetu kuwa ujenzi huo utaongeza kwa kiasi kikubwa mapato yetu ya ndani na hivyo kupunguza utegemezi na kuwaletea wananchi maendeleo.

Mhe. Spika, Kamati yetu ilifanya ziara mara kadhaa kuona maendeleo ya ujenzi huo. Pamoja na kwamba bado ujenzi huo upo katika hatua za awali, kwa

ujumla Kamati yetu imeridhishwa na hatua iliyofikiwa. Tunatoa wito kwa Wizara kusimamia kwa umakini zaidi ujenzi wa uwanja huo ili uweze kukamilika ndani ya wakati na kwa kiwango bora, kwa mujibu wa mkataba. Tunasisitiza suala la ubora wa ujenzi wa uwanja huo kutokana na ukweli kuwa fedha zilizopangwa kutumika katika ujenzi ni nyingi sana na iwapo ujenzi huo hautakuwa na kiwango kinachokubalika, utakuwa ni mzigo mkubwa kwa wananchi wetu.

**UWANJA WA NDEGE PEMBA**

Pamoja na pongezi hizo tulizotangulia kuzitoa, hata hivyo Kamati imehuzunishwa kuona kuwa uwanja wa ndege uliopo Pemba haukutengewa fedha katika bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kuufanyia matengenezo uwanja huo hasa katika uwekaji wa taa zitakazowezesha ndege kuruka na kutua katika uwanja huo wakati wa usiku. Kamati inasikitika kuona kwamba ahadi ya kuuwekea taa uwanja huu ambayo ni ya muda mrefu, imeshindwa kutekelezwa hadi sasa. Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi imekuwa kwa muda mrefu ikiishauri serikali kuuwekea taa uwanja huo kutokana na umuhimu wake katika masuala ya uchumi na kijamii kwa wananchi wa visiwa vya Zanzibar. Kamati yetu inaiomba Serikali ifikirie upya suala hilo kwa kujitahidi kuutengea fedha uwanja huo kwa ajili ya matengenezo ndani ya bajeti ya mwaka huu.

**UANZISHWAJI WA VYUO VYA UBAHARIA NA ANGA**

Mhe. Spika, Kamati yetu mara kadhaa imekuwa ikishauri kuanzishwa kwa chuo cha ubaharia hapa Zanzibar, kutokana na kuwepo kwa vijana wengi wanaotaka kusoma kozi ya ubaharia katika vyuo vilivyopo nje ya Zanzibar kikiwemo chuo kilichopo Tanzania Bara. Hata hivyo, baadhi ya vijana hawa wamekuwa wakishindwa kufanya hivyo kutokana na kushindwa gharama mbali mbali kama vile malipo ya ada, usafiri na gharama za malazi, gharama ambazo zingepungua sana kama chuo cha namna hiyo kingekuwepo hapa Zanzibar. Kamati yetu imefurahishwa sana kuelezwa kuwa wizara inakusudia kuanza mchakato wa uanzishwaji wa chuo cha fani ya Ubaharia pamoja na chuo cha kufundishia wataalam wa fani ya Ndege. Hiyo ni hatua muhimu sana katika kuhakikisha Zanzibar inakuwa na wataalam wa kutosha katika fani hizo, hatua ambayo inafaa kupongezwa.

Mhe. Spika, hata hivyo Kamati yetu ina wasi wasi mkubwa wa utekelezaji wa suala hili kutokana na Kamati kutoona fedha zilizotengwa kwa ajili ya kuanza hatua za awali za matayarisho ya ujenzi wa vyuo hivyo. Dhamira hiyo huenda ikawa ngumu kutekelezeka kama hakuna bajeti iliyotengwa kwa ajili hiyo. Kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Waziri, suala hili ni miongoni mwa malengo yanayopangwa kutekelezwa chini ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ambapo katika kasma zake, Kamati yetu haioni ni wapi suala hilo limetengewa fedha.

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kufikiria suala hilo kwa kutenga fedha zitakazosaidia hatua za awali za uanzishaji wa vyuo hivyo ambavyo tunaamini vitakuwa ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya mapato lakini pia nchi yetu kupata wataalam wa kutosha katika fani hizo.

**UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO**

Mhe. Spika, mapato makubwa yamekuwa yakipotea kutokana na kutokuwepo kwa chelezo kikubwa kitakachoweza kukidhi mahitaji ya vyombo vyetu vya usafiri wa baharini hapa Zanzibar. Badala yake, vyombo vingi vimekuwa vikipelekwa Mombasa, Kenya kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo na hivyo kuiingizia nchi hiyo ya Kenya fedha nyingi za kigeni, hasa ukizingatia kuwa matengenezo ya vyombo vya baharini nchini humo yamekuwa yakilalamikiwa kuwa ni ghali sana. Kwa mnasaba huo, kuna haja kubwa ya kuwashawishi na kuwaunga mkono wawekezaji ili wawekeze katika ujenzi wa chelezo kwa lengo la kuvifanyia matengenezo vyombo vyetu hapa hapa nchini, hatua ambayo itaokoa fedha nyingi za kigeni lakini pia kutoa ajira kwa wananchi wetu.

Pamoja na umuhimu huo wa kuvutia wawekezaji watakaowekeza katika ujenzi na uendeshaji wa chelezo, Kamati yetu inasikitishwa na hatua ya taasisi husika kutotoa msaada unaohitajika kwa muekezaji mzalendo aliyeazimia kuwekeza katika mradi wa chelezo huko Mangapwani, Zanzibar. Kutokana na kuguswa na suala hilo, Kamati yetu ilichukua hatua mbali mbali ili kuhakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi kwa ajili ya maslahi ya wazanzibari.

Hatua ya kwanza ambayo Kamati yetu ilichukua ni kutembelea eneo lilokusudiwa kwa ajili ya mradi huo na kupata maelezo kutoka kwa muekezaji huyo mzalendo. Kamati haikuishia hapo, kwani iliitisha kikao cha pamoja na taasisi mbali mbali za serikali zikiwemo Mamlaka ya Kuendeleza Uwekezaji Zanzibar (*ZIPA*), Idara ya Mazingira Zanzibar na Katibu Mkuu katika Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Muekezaji huyo.

Mhe. Spika, ingawa katika kikao hicho ilielezwa kuwa muekezaji huyo alionekana kutofuata baadhi ya taratibu za uekezaji, Kamati yetu ilisisitiza na inaendelea kusisitiza juu ya haja ya serikali kumuelekeza na kumsaidia muekezaji huyo taratibu zinazotakiwa kufuatwa ili kukamilisha mradi huo. Kamati yetu imechukua hatua zote hizi kutokana na umuhimu na uzito wa suala hili kwa kuzingatia kuwa iwapo mradi huu utafanikiwa, nchi yetu itaongeza wigo wa kukusanya kodi na kusaidia katika huduma mbali mbali.

Aidha, mradi huu utaweza kuajiri vijana wengi na hivyo kupunguza tatizo la ajira nchini, tatizo ambalo serikali ya awamu ya saba imeazimia kuliondoa kwa

kuunda wizara mahsusi inayoshughulika na uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa msingi huo, Kamati yetu inahimiza kuchukuliwa hatua za haraka kwa mujibu wa sheria, kumsaidia muekezaji huyo ili wananchi wa Zanzibar waweze kufaidika na mradi huo kwani kutofanikiwa kwa miradi kama hii, wanaoathirika zaidi ni wananchi.

**UTAFITI KATIKA WIZARA**

Mhe. Spika, Kamati inapongeza sana muundo mpya wa idara katika wizara za serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuingiza suala la utafiti katika idara ya Sera na Mipango na hivyo jina la idara hiyo kuwa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Suala la utafiti ni jambo muhimu sana katika maendeleo ya nchi yoyote na nchi nyingi zilizoendelea, zimekuwa zikiwekeza fedha za kutosha katika utafiti na maendeleo (*research and development*). Kamati yetu inaamini kuwa utafiti kwa wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni muhimu sana katika kuleta mageuzi ya kimaendeleo katika wizara hiyo na nchi kwa ujumla.

Pamoja na ufinyu wa bajeti uliopo, Kamati ilitegemea kuona kiasi cha fedha kinatengwa kwa ajili ya kuendeleza utafiti ili kuitekeleza azma ya serikali ya kufanya tafiti kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Katika hotuba ya bajeti ya Mhe. Waziri na katika kasma za Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ziliopo katika bajeti hii, hakuna viashiria vinavyoonyesha kuwa idara itaweza kufanya tafiti kwa kiwango cha kuridhisha, ambazo zitasaidia kuleta maendeleo ya taasisi ziliopo katika wizara hiyo na hivyo kuakisi jina la idara hiyo.

Kamati yetu ilitegemea kuona bajeti ya idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaongezeka ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha uliopita kutokana na kuongezeka kwa suala zito la utafiti katika idara hiyo. Lakini bajeti hiyo imeshuka kwa kiwango kikubwa kutoka zaidi ya shilingi milioni mia saba kwa mwaka 2010/2011 na kufikia shilingi milioni mia moja na hamsini tu kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, miongoni mwa gharama zilizosababisha kushuka kwa makisio ya bajeti ya idara hiyo ni kupungua kwa makisio ya gharama za mtandao (*internet*) ambayo katika bajeti hii imetengewa shilingi milioni moja tu (TZS 1,000,000/-) ukilinganisha na zaidi ya shilingi milioni tatu na laki tano zilizotengwa katika bajeti iliyomalizika. Katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia ambapo mawasiliano ya habari na teknolojia (ICT) yana nafasi kubwa katika masuala ya utafiti, ingekuwa vyema makisio kwa ajili ya mtandao (*internet*) yakaongezwa ili kuimarisha tafiti katika wizara hiyo.

Pamoja na ukweli kwamba Idara hii ilijumuisha ofisi ya Mrajis wa meli kwa mwaka wa fedha uliomalizika, bado bajeti ya idara hiyo imeshuka sana kwa

ajili ya utekelezaji wa kazi za idara hiyo. Ili kutekeleza azma nzuri ya kuimarisha tafiti katika wizara hii, kamati yetu inashauri idara hii kuwezeshwa ili iweze kutekeleza kazi za utafiti badala ya dhana hiyo kubaki katika jina la idara pekee.

**MAFUNZO KWA WATENDAJI**

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Kamati yetu inapenda kutoa maoni yake ni suala la mafunzo kwa wafanyakazi wa taasisi mbali mbali za wizara. Mhe. Waziri ameeleza katika hotuba ya bajeti, azma ya wizara kuajiri wataalam mbali mbali kama vile katika fani ya *ICT*, Wahandisi na wataalam wa fani nyengine pamoja na kuwaendeleza watumishi hao. Kamati imefarijika kwa kauli hiyo ambayo bila shaka itakapotekelezwa, itapelekea kuongezeka kwa ufanisi wa wizara.

Hata hivyo, Kamati yetu inadhani kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya mafunzo kwa taasisi mbali mbali za wizara hii ni ndogo mno kuweza kutekeleza azma hiyo, kuliko hata bajeti iliyotengwa kwa mwaka uliopita. Katika kuthibitisha hilo, Kamati yetu imefanya rejea katika Idara ya Anga na Ofisi Kuu, Pemba ambapo katika mwaka wa fedha uliomalizika, zilitengewa fedha nyingi zaidi kwa ajili ya mafunzo kuliko inavyoonekana katika makadirio ya bajeti ya mwaka 2011/2012.

**UJENZI NA UTUNZAJI WA BARABARA**

Mhe. Spika, miongoni mwa maeneo ambayo Kamati yetu inaipongeza wizara na serikali kwa jumla ni suala la ujenzi na utunzaji wa barabara. Hii inajumuisha miradi ya barabara mbali mbali inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo na serikali pamoja na barabara zinazofanyiwa matengenezo chini ya usimamizi wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara (*UUB*) kwa fedha kutoka Mfuko wa barabara. Wizara na Serikali kwa ujumla imefanya kazi kubwa ya kuyaunganisha maeneo kadhaa ya Zanzibar kwa mtandao wa barabara, hatua ambayo inachochea maendeleo ya nchi na kurahisisha huduma za kijamii. Ni dhahiri kuwa hivi sasa maeneo mengi ya Unguja na Pemba yanafikika kwa urahisi baada ya kazi nzuri ya Wizara na serikali kwa ujumla.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati yetu imekuwa na inaendelea kusisitiza juu ya ubora wa viwango katika ujenzi wa barabara hizo hasa pale ambapo mkandarasi binafsi anapopewa kazi ya ujenzi wa barabara. Aidha, Kamati inasisitiza umakini katika uingiaji wa mikataba ya ujenzi wa barabara ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa barabara unamalizwa kwa wakati na kwa kiwango bora kitakachowezesha barabara hizo kudumu kwa muda mrefu na hivyo kuokoa fedha za serikali kwa kutojenga barabara hizo mara kwa mara.

Ni vyema mikataba inayofungwa baina ya serikali na wajenzi wa barabara ikapitiwa kwa umakini mkubwa kwa kuishirikisha kwa karibu zaidi ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ili kuhakikisha maslahi ya serikali na nchi kwa ujumla yanalindwa katika mikataba hiyo. Kamati inatoa wito kwa serikali kuhakikisha mikataba ya aina hiyo inaheshimiwa na pale wajenzi hao wanaposhindwa kuheshimu au kutimiza masharti ya mkataba ikiwemo ubora wa viwango vya ujenzi pamoja na kushindwa kumaliza ujenzi kwa wakati, kuchukua hatua mara moja dhidi ya mjenzi husika.

**ULIPAJI FIDIA KATIKA MIRADI YA UJENZI WA BARABARA**

Mhe. Spika, Kamati yetu pia inasisitiza juu ya haja ya serikali kuhakikisha nayo inatimiza wajibu wake katika miradi ya barabara ikiwemo suala la ulipaji wa fidia kwa nyumba na mali nyengine zinazoondoshwa kupisha ujenzi wa barabara. Tunaishauri serikali kutenga fedha mapema kwa ajili ya malipo ya fidia ili kuharakisha hatua za ujenzi na pia kuondoa manung'uniko kutoka kwa wananchi na hata taasisi nyengine kama Shirika la Umeme, Mamlaka ya Maji na Kampuni ya Simu kwa kuondosha miundombinu yake wakati wa ujenzi wa barabara.

**USHIRIKISHAJI WA SEKTA BINAFSI KATIKA UJENZI WA BARABARA**

Mhe. Spika, Wizara inastahili pongezi za dhati kwa jitihada zake za kushirikisha Sekta Binafsi katika ujenzi wa barabara hasa vikundi vya kijamii viliopo maeneo ambayo ujenzi huo unafanyika. Kamati yetu imefarijika sana na hatua hii ambayo itasaidia sana katika kuwasaidia wananchi wetu kupata nafasi za ajira angalau za muda mfupi. Tunashauri jitihada hizi ziendelezwe kila inapowezekana kwa lengo la kutimiza azma ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba ya kuwawezesha wananchi kiuchumi.

**UIMARISHAJI WA KARAKANA YA SERIKALI**

Mhe. Spika, Kamati yetu inaamini kuwa Karakana ya Serikali ni kitengo muhimu kwa madhumuni ya kuokoa fedha ya serikali kwa ajili ya matengenezo ya magari ambayo hugharimu fedha nyingi zaidi yanapotengenezwa na taasisi binafsi. Lakini pia Karakana hiyo inaweza kuingiza fedha nyingi zaidi endapo itaimarishwa na kuwa na zana za kisasa kwa ajili ya matengenezo ya magari. Kwa bahati mbaya Kamati yetu ilipotembelea Karakana ya Serikali, ilibaini kuwa vifaa vingi kwa vinavyotumika kwa ajili ya matengenezo ya magari na vifaa mbali mbali, vimeharibika na baadhi ya vifaa havitumiki kwa kuwa hakuna wataalam wanaoweza kutumia vifaa hivyo baada ya wataalam waliokuwepo kufariki au kustaafu.

Kamati yetu inasisitiza haja ya kuimarishwa kwa Karakana ya Serikali kwa kuipatia vifaa vya kisasa na pia kuvifufua vifaa vilivyoharibika pamoja na

kufundisha wataalam watakaoweza kutumia vifaa hivyo. Katika hotuba ya bajeti ya Wizara inaonyesha kuwa miongoni mwa malengo ya Idara ya Usafiri na Leseni ambayo Karakana ya Serikali ipo ni pamoja na kuimarisha Karakana ya Serikali kwa kuipatia vifaa na wataalam. Hata hivyo, katika bajeti hii ya mwaka 2011/2012, Kamati haioni kama lengo hili linaweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kutokuwepo kwa fedha za kutosha zilizotengwa moja kwa moja kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa lengo la kufanya mageuzi makubwa katika karakana hiyo.

**HAJA YA KUWA NA BANDARI MPYA**

Mhe. Spika, miongoni mwa vyanzo muhimu sana katika uchumi wetu ni pamoja na bandari. Bandari zetu zimekuwa zikikusanya mapato kutokana na vyombo na mizigo mbali mbali inayopitishwa katika bandari hizo lakini muhimu zaidi, bandari hizo zimekuwa mlango unaotumika kama chanzo cha kukusanyia mapato kwa idara nyengine kama vile Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*).

Mhe. Spika, pamoja na jitihada za Shirika la Bandari kuchukua hatua mbali mbali ili kwenda sambamba na ongezeko la vyombo na bidhaa zinazoshushwa katika bandari zake hasa ile ya Malindi, bado ukweli unabakia kuwa bandari hiyo ya Malindi sasa imeelemewa sana na inahitaji kusaidiwa. Kwa msingi huo, Kamati yetu inashauri serikali kuongeza jitihada ili kuhakikisha wazo la ujenzi wa bandari mpya katika eneo la mpigaduri linafanikiwa mapema zaidi. Kamati inaamini kuwa ujenzi huo wa bandari mpya utasaidia sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu hasa ukizingatia kuwa kuna fursa nzuri kwa meli nyingi zaidi kuingia nchini kupitia bandari hiyo pale tutakapokuwa na bandari yenye nafasi zaidi.

Aidha, tunashauri serikali kuwekeza katika suala la ununuzi wa zana za kisasa zaidi ambazo zitasaidia katika kuharakisha upakiaji na ushushaji wa mizigo katika bandari zetu, jambo ambalo bila ya shaka litawavutia wafanyabiashara wengi zaidi kuzitumia bandari zetu na hivyo kuongeza mapato yetu ya ndani.

**KUZOROTA KWA SHIRIKA LA MELI KATIKA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI**

Mhe. Spika, Kamati yetu ina wasi wasi mkubwa na hali ya maendeleo ya Shirika la Meli na Uwakala hasa katika upande wa huduma za meli. Hivi sasa meli zinazoendeshwa na shirika hilo ni mbili tu ambazo pia ni za zamani sana na hivyo kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara yanayosababisha hasara kwa shirika. Kwa sasa mapato yanayotegemewa hasa na Shirika ni kutokana na huduma za uwakala. Bila ya shaka hiyo si hali nzuri kwa shirika na hivyo juhudi za makusudi za serikali zinahitajika, ili kuliimarisha shirika hilo kwa

kulisaidia ili kupata meli mpya na za kisasa ambazo zitasaidia katika kuliimarisha shirika kimapato lakini pia meli hizo zitawasaidia wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba katika suala la usafiri.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba Serikali imelikataa wazo la kukopa meli kutoka nchini Afrika ya Kusini kutokana na mkopo huo kuwa wa gharama kubwa kwa serikali, Kamati inashauri serikali kufanya jitihada kubwa ili kuhakikisha inapata meli nyengine zitakazoweza kuongeza mapato ya shirika na kusaidia sekta ya usafiri wa bahari hasa baina ya Unguja na Pemba. Kamati yetu inaiomba serikali ionyeshe ndani ya bajeti yake ni kwa namna gani imedhamiria kwa dhati kabisa kutimiza azma hii ya kuwa na meli mpya hapa Zanzibar.

**UANZISHWAJI WA IDARA YA MAWASILIANO**

Mhe. Spika, Kamati yetu inaipongeza kwa dhati serikali kwa kuanzisha idara mpya ya mawasiliano yenye jukumu kubwa la kusimamia maendeleo na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano hapa Zanzibar, ikiwa ni pamoja na matumizi ya tovuti (*website*) kwa wizara zote za serikali. Ni dhahiri kuwa huu ni mwanzo mzuri wa kuelekea katika mafanikio kwani maendeleo katika zama hizi yanategemea kwa kiasi kikubwa teknolojia mbali mbali ikiwemo ile ya habari na mawasiliano (*ICT*). Ni matarajio ya Kamati yetu kuwa idara hii itaimarishwa kwa kupatiwa wataalam wa kutosha na nyenzo za kufanyia kazi pamoja na mafunzo yatakayowawezesha watendaji wa idara hii kukabiliana na changamoto za ukuaji wa teknolojia ulimwenguni.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, pamoja na mipango mizuri ya wizara katika bajeti ya mwaka 2011/2012, mafanikio ya wizara hii yatategemea sana uwajibikaji wa watendaji na umakini, nidhamu na uadilifu katika kusimamia rasilimali zetu ambazo serikali imewapa mamlaka watendaji hao kuzikusanya na kuzizimamia. Hivyo Kamati yetu inamuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake, kujitahidi katika kuhakikisha rasilimali chache tulizonazo kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano zinakusanywa na zinatumika vizuri kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake.

Mhe. Spika, Kamati yetu inatarajia kuwa serikali itayazingatia kwa dhati maoni haya ya Kamati kadri itakavyowezekana ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa malengo tuliyojipangia na hivyo kuchochea maendeleo ya nchi. Aidha, Kamati yetu inaahidi kutoa msaada kwa wizara kila inapowezekana ili kuhakikisha kuwa azma ya serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo inatimia. Napenda kumthibitishia Mhe. Waziri kuwa Kamati ipo tayari kutoa mawazo na fikra za kuisaidia wizara katika utekelezaji bora wa malengo yaliyowekwa katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mwisho, kwa kuwa lengo kuu, baada ya maridhiano yaliyopelekea kuwa na serikali yenye muundo wa umoja wa kitaifa ni kuleta maendeleo kwa nchi yetu, tunawaomba Wajumbe wenzetu wa Baraza hili nao waichangie hotuba hii wakiwa na dhamira ya kuiimarisha zaidi ili tuweze kufikia maendeleo tuliyoyakusudia.

Mhe. Spika, sasa napenda kutamka kuwa kwa niaba ya Kamati yangu, naiunga mkono hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Ahsanteni kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa na mimi ni mjumbe katika Baraza la Wawakilishi, nimeshamaliza kutoa hotuba ya kamati, naomba dakika mbili niweze kutoa mchango wangu mdogo kwa jimbo langu.

Kwanza napenda niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Ziwani kwa ushirikiano wanaonipa. Kwa niaba yao napenda niiambie Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano jambo moja tu. Jimbo la Ziwani njia zake ni sawa sawa na kuti, kuti lina njia moja tu, lakini makuti mengi na halirudi. Sasa naomba watu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano waifahamu Ziwani, kila njia unayoichukua ya ndani inafika pwani haiungani na mwenzake. Kwa sababu njia hizi ni sawa sawa na makuti yalivyo zinasahauliwa mara nyingi kwa sababu wakubwa hawazitembelei sana. Kwa hivyo, naomba sana wazitizame na hakuna tope kuna nta. Ikinyesha mvua gari zinanasa, kwa hivyo, naomba sana wazitizame.

La mwisho, kwa niaba ya kamati napenda kumkaribisha mzee wetu na kaka yetu Mhe. Ali Mzee Ali. Mimi siwezi kumpa sifa zaidi aliyopewa na Mhe. Hamad Masoud, isipokuwa nataka nimwambie jambo moja tu. Sisi kambi yetu ya *backbenchers* imepata *encyclopedia* sasa hivi. Pamoja na uwezo wake mkubwa tunamuomba Mhe. Rais atuachie kidogo tupate elimu kabla hajamtwika jukumu jengine. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

**Mhe. Spika:** Nakushukuru sana Mhe. Makamo Mwenyekiti kwa kuwasilisha hotuba hiyo ya Kamati. Waheshimiwa Wajumbe tulikuwa na ahadi ya baada ya kuwasilisha hotuba hiina pia kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti, basi tuamuwe tukapumzike. Kama hivyo ndivyo mpaka sasa hivi, basi ingawa tayari nimepata majina kama 15 hivi ya Waheshimiwa Wajumbe. Lakini ni juu yetu kuona kama tukapumzike, tuna muda kama wa dakika 50 tu kufikia wakati wa kwenda kupumzika. Sasa kama tukapumzike sana na kama vyenginevyo sawa.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa hoja kwamba kwa sababu Baraza hili lilichukua muda mrefu wakati wa asubuhi katika kujadili hoja na kuipitisha na kwa sababu ya umuhimu wa hotuba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na ingekuwa vizuri kwa Waheshimiwa Wajumbe kupata muda wa kuipitia kabla ya kuichangia. Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu litenge kando kanuni ili liweze tuweze kukiahirisha kikao kabla ya muda wake mpaka kesho. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

**Mhe. Spika:** Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujaahirisha kikao kuna tangazo dogo. Tangazo hili ni la Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, kwamba kesho mnamo saa 8:00 mchana kutakuwa na tamasha la utamaduni wa Oman wakishirikiana na wizara hiyo kuendesha tamasha hilo, ambalo litakuwa pale Beit el Ajab. Inawezekana wengi wetu tumealikwa kwenda huko na litaanza saa 8:00 mchana.

Tunaweza tukaenda huko tukikumbukia kwamba pia kikao cha jioni saa 11:00 Mwenyezi Mungu akipenda kitakuwepo na kwenye tamasha inawezekana kukawa na utamu fulani hivi, ukatuvutia Waheshimiwa Wajumbe tukasahau kwamba pia kuna majukumu ya kuhudhuria masuala ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano, tukikumbuka kuwa kumbe tuko nyuma ya wakati.

Kwa hivyo, naomba niwape taarifa hiyo kuwa kutakuwa na tamasha pale Beit el Ajab kesho saa 8:00 mchana, lakini bila kusahau kama saa 11:00 kuwa tutakuwa na shughuli yetu ya kuendelea na wizara hii. Baada ya hayo basi Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 13/07/2011 saa 3:00 za asubuhi.

*(Saa 12:50 jioni Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 13/07/2011 saa 3:00 za asubuhi)*